# FUMBO LA UHAI NA KIFO KATIKA RIWAYA ZA EUPHRASE KEZILAHABI *NAGONA* NA *MZINGILE*

NA

GLADYS WANJIRU NJOGU

TASNIFU HII IMETOLEWA KATIKA IDARA YA KISWAHILI NA LUGHA ZA KIAFRIKA KATIKA CHUO KIKUU CHA KENYATTA KWA AJILI YA KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJI YA KUTUNZWA SHAHADA YA UZAMILI KATIKA KISWAHILI

2014

Kenyatta University
Kiswahili Resource Centre

# UNGAMO

Kazi hii ni yangu mwenyewe na haijawahi kutolewa katika chuo kikuu kingine kile.

27/10/2014

**Njogu Gladys Wanjiru** **Tarehe**

Pendekezo hili la utafiti limewasilishwa kwa idhini yetu kama wasimamizi wa kazi hii wa chuo kikuu.

29/10/2014

**Profesa Kitula King'ei** **Tarehe**

27/10/14

**Bwana J.M Mukobwa** **Tarehe**

Kenyatta University
Kiswahili Resource Centre

# TABARUKU

Naitabaruku kazi hii kwa mume wangu Harrison Thuo kwa kugharamia masomo yangu. Pia watoto wangu Peris na Cecilia kwa kunivumilia wakati huo wote.

# SHUKRANI

Kwanza, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa baraka zake hadi nikaweza kumaliza kazi hii. Siwezi kuwasahau wasimamizi wangu Prof. G. King'ei na Bwana M. Mukobwa kwa kunitia hamasa ya kutia bidii kama mchwa ili kufanikisha kazi hii. Kutokana na mwongozo wenu wa busara pamoja na ushauri wa mara kwa mara, niliweza kumaliza kazi hii kwa wakati ufaao. Msaada wenu, maoni, fikra, maarifa, mapendekezo na mwongozo katika kila hatua niliyopiga ulinisaidia sana katika kufika kiwango hiki. Ahsanteni sana kwa kunivumilia.

Nawashukuru sana wahadhiri wote wa Idara ya Kiswahili na lugha za Kiafrika kwa mwongozo mlionipa wakati wa kutetea pendekezo langu la utafiti. Ushauri wenu ulinifaa zaidi. Shukrani za kipekee zimwendee Dkt. Masinde, ushauri wake ulitilia rutuba utafiti wangu. Mungu ambariki na amzindishie maisha hapa ulimwenguni. Siwezi kumsahau Festo Haule mzamili mwezangu aliyenijulisha kwa Athman Ponera kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma. Usaidizi alionipa Athman Ponera ulinifaa sana kuhitimisha tasnifu hii.

Wazamili wenzangu walinifaa sana kwa mengi kuliabiri jahazi hili la elimu. Motisha walionipa hauna kifani na maombi yangu ni kuwa kila mmoja wetu atatimiza ndoto yake ya kufika upeoni kimasomo. Siwezi kumsahau mzamili mwenzangu Sophie Okwena aliyenipa motisha hata wakati nilipokuwa nimelemewa. Mungu akubariki dada kwa ushauri ulionipa.

Nawashukuru wazazi wangu Cecilia Waithera na Daniel Njogu ambao walinilea na kunipeleka shuleni. Isipokuwa ni juhudi zao za kunipeleka shule umbali huu singeuona. Mungu awabariki na awazidishie maisha.

Mwisho nawashukuru Tenya Nyambura na Beth Wamuhu walionisaidia sana katika kupiga chapa na kuipanga kazi hii.

# IKISIRI

Utafiti huu umechunguza dhana ya uhai na kifo katika riwaya teule za Kiswahili *Nagona* na *Mzingile*. Ili kuafiki hili, tumeongozwa na maswala matatu ya kimsingi. Kwanza, utafiti huu umechunguza jinsi Kezilahabi ametumia dhana ya uhai na kifo kama fumbo. Pili, umechunguza matokeo ya uhai na kifo katika riwaya ya *Nagona* na *Mzingile*. Hatimaye, mitazamo mbalimbali ya uhai na kifo imechunguzwa na kubainishwa. Misingi ya Nadharia ya Kikale na ya Uhalisiaajabu inayohusika imetumiwa . Nadharia hizi zimetumika ili kufanikisha lengo kuu la utafiti huu ambalo ni kubainisha kuwa maisha ya mwanadamu ni safari iliyo duara. Data ya Utafiti huu ilipatikana maktabani. Data hiyo ilipatikana kupitia usomaji wa vitabu, majarida na usomaji mpana wa makala mbalimbali. Utafiti umegawanywa katika sura tano. Sura ya kwanza ni utangulizi wa kazi nzima na ndiyo kiini cha Utafiti huu. Sura ya pili imechunguza historia, maandishi na falsafa za E. Kezilahabi. Sura ya tatu imechunguza maudhui ya uhai na kifo katika riwaya ya *Nagona* kupitia ishara mbalimbali. Sura ya nne imechanganua maudhui ya uhai na kifo katika riwaya ya *Mzingile* pia kupitia ishara mbalimbali. Sura ya tano imehitimisha utafiti huu kwa kutoa muhtasari, mchango, matokeo na changamoto za utafiti. Utafiti umebainisha kuwa maisha ya mwanadamu sio mstari ulio na kikomo bali maisha ya mwanadamu ni duara.

**ABSTRACT**

These research is about the concept of life and death in selected Kiswahili novels *Nagona* and *Mzingile.* The research has been guided by three basic questions. First, we have researched on how Kezilahabi has used the concept of life and death as a mystery. Two, the research has looked at the outcome of life and death in the two novels and astly, we have researched on different ways of viewing life and death. The tenets of archetypical and magical realism theories were used so as to meet the objectives of the research. Data analysis was done in the library through intensive reading of books and different materials. These research has been divided into five chapters. The first chapter gives the summary of the whole research. The second chapter gives the history and the philosophies of E. Kezilahabi. The third chapter has looked at different themes of life and death in in *Nagona* through different images. The fourth chapter gives the themes of life and death in *Mzingile.* The fifth chapter concludes these research by giving the summary, contribution, outcome and problems of the research.The outcome of the research is that life is not a straight line but is cyclic.

## UFAFANUZI WA ISTILAHI

**Metafizikia**

Falsafa ya kuchunguza chanzo cha uhai na maarifa; mazungumzo ya hewani,udhanifu.

**Ishara/Taswira**

Dhana inayoleta picha katika akili ya msomaji na huwa imeficha ujumbe fulani.

**Mwingilianomatini**

Kuwepo kwa sifa mbalimbali za matini moja au zaidi katika kazi ya kifasihi,

**Fantasia**

Kazi ya kifasihi ambayo ina sifa  ambazo zinakiuka uhalisia.

# YALIYOMO

## SURA YA KWANZA

## MSINGI WA UTAFITI

1.0 Utangulizi ........................................ 1
1.1 Suala la Utafiti ........................................ 3
1.2 Maswali ya Utafiti ........................................ 3
1.3 Malengo ya Utafiti ........................................ 3
1.4 Sababu za Kuchagua Mada ........................................ 4
1.5 Upeo na Mipaka ya Utafiti ........................................ 5
1.6 Yaliyoandikwa Kuhusu Mada ........................................ 6
1.7 Misingi ya Nadharia ........................................ 9
1.8 Mbinu za Utafiti ........................................ 14
1.8.1 Mahali pa Utafiti ........................................ 14
1.8.2 Uteuzi wa Sampuli ........................................ 15
1.8.3 Ukusanyaji data ........................................ 15
1.8.4 Uchanganuzi data ........................................ 16
1.9 Uwasilishaji wa matokeo ya Utafiti ........................................ 17

## SURA YA PILI

## HISTORIA, MAANDISHI NA FALSAFA ZA E. KEZILAHABI

2.0 Utangulizi ........................................ 18
2.1 Kumhusu Mwandishi Euphrase Kezilahabi ........................................ 18
2.1.1 Maisha yake ........................................ 18
2.1.2 Kazi zake ........................................ 19
2.1.3 Tajiriba yake ........................................ 21
2.1.4 Watunzi waliomwathiri ........................................ 22
2.2 Mawazo katika Riwaya zake ........................................ 27
2.3 Dhana ya Uhai na Kifo ........................................ 30
2.4 Hitimisho ........................................ 37

## SURA YA TATU

## MAUDHUI YA UHAI NA KIFO KATIKA RIWAYA YA NAGONA

3.0 Utangulizi ........ 38

3.1 Uhakiki wa riwaya ya *Nagona* ........ 41

3.1.1 Hadithi ya "mimi" ........ 41

3.1.2 Hadithi ya babu ........ 46

3.1.3 Safari ya "mimi" ........ 48

3.1.4 Matatizo ya ulimwengu ........ 50

3.1.5 Mwanamke na paa wa ajabu ........ 52

3.1. 6 Uvumbuzi ........ 57

3.1.7 Ugonjwa wa babu ........ 58

3.1.8 Mjadala wa ungamo ........ 61

3.1.9 Ngoma kuu ........ 62

3.2 Uhakiki wa riwaya ya Nagona ........ 67

3.3 Maana ya Anwani ........ 68

3.3.1 Ishara ya maji ........ 68

3.3.2 ishara ya msitu ........ 72

3.3.3. Ishara ya mzee ........ 75

3.3.4 Ishara ya duara ........ 77

3.3.5 Ishara ya mwanga ........ 80

3.4 Hitimisho ........ 81

## SURA YA NNE

## MAUDHUI YA UHAI NA KIFO KATIKA RIWAYA YA MZINGILE

4.0 Utangulizi ........ 83

4.1 Uhakiki wa riwaya ya *Mzingile* ........ 86

4.1.1 Kakulu ........ 86

4.1.2 Safari ya Msimulizi ........ 90

4.1.3 Kichaa ........ 99

4.1.4 Mzee Kipofu ........ 104

4.1.5 Msichana Afrika ........ 117

4.1.6 Amani ........ 123

4.2 Fumbo la Uhai na Kifo ........ 145

4.3. Ishara ya Mwanga ... 147
4.4 Ishara ... 147
4.4.1 Ishara ya Mwanga ... 148
4.4.2 Ishara ya mzee ... 149
4.4.3 Ishara ya maji ... 150
4.4.4 Ishara ya Mwanamke ... 151
4.4.5 Ishara ya Giza ... 152
4.4.6 Ishara ya Rangi Nyeusi ... 153
4.5 Hitimisho ... 154

**SURA YA TANO**

**HITIMISHO, MATOKEO NA MAPENDEKEZO**

5.0 Utangulizi ... 155
5.1 Muhtasari wa Utafiti ... 155
5.2 Changamoto za Utafiti ... 158
5.3 Mchango katika Utafiti ... 159
5.4 Matokeo ya Utafiti ... 159
5.5 Mapendekezo ... 160
5.6 Hitimisho ... 161
Marejeleo ... 162

# SURA YA KWANZA

# MSINGI WA UTAFITI

## 1.0 UTANGULIZI

Utangulizi wa utafiti huu umeshughulikia; Suala la utafiti, maswali ya utafiti, malengo ya utafiti, sababu za kuchagua mada, misingi ya nadharia, yaliyoandikwa kuhusu mada, upeo wa utafiti, mbinu za utafiti na uchanganuzi wa data.

Masimulizi katika riwaya za *Nagona* na *Mzingile* sio ya moja kwa moja. Riwaya hizi zimechukua dhima ya uchunguzi wa jamii huku zikibeba silaha mpya za njia za utunzi na njia za majadiliano. Fasihi ya Kiafrika inahusu fasihi simulizi na mwandishi amezama katika uchunguzi wa filasafia na saikolojia. Riwaya ya *Nagona* imewekewa msingi na fasihi simulizi ya Kiafrika na "fasihi simulizi haina mipaka." Mwandishi huyu ametumia utamaduni, elimu ya mila na desturi kama suala kuu la kimaudhui.

Maudhui makuu ambayo ni changamani katika riwaya hii yanasawiriwa kupitia taswira. Riwaya ya *Nagona* na *Mzingile* ina maumbile mengi ikiwa ni pamoja na utafutaji wa chanzo cha uhai, maarifa na ujifunzaji.

Oestigaard (2004), ameeleza kuwa kifo ni dhana kongwe kama maisha yalivyo hapa ulimwenguni. Mtu anapozaliwa hali yake ya kufa polepole huanza na huwa hana uwezo wa kifo chake. Mwandishi wa riwaya ya *Nagona* na *Mzingile,* Euphrase Kezilahabi ameandika riwaya kama vile, *Rosa Mistika, Kichwa Maji, Dunia Uwanja Wa Fujo na Gamba La Nyoka.*

Kezilahabi ameathiriwa na uchawi, ushirikina, ukale na usasa miongoni mwa masuala mengine. Jamii ya Wakerewe hukumbuka wahenga kupitia matambiko mbalimbali kama vile, kumwaga pombe wakati wa sherehe za unywaji pombe au kuacha chombo kidogo kilichowekwa pombe mahali maalum kama tambiko kwa wahenga.

Aristotle katika *Poetics* aliweka amana kuwa katika futuhi, mwandishi hujenga ploti kulingana na welekeo halafu anaingiza sifa za majina lakini mwandishi wa tanzia hutumia majina halisi ya kihistoria. Uchaguzi wa majina ya wahusika katika riwaya ya *Nagona* na *Mzingile* unatuelekeza katika jamii ya Wakerewe. Riwaya hii inahusishwa na epistemolojia ya mtiririko asilia wa uzoefu wa maisha ya mwanadamu.

Kifo kimesawiriwa kwa njia mbalimbali na jamii za kiafrika. Kwanza, kifo kimesawiriwa kama safari, pumziko, adhabu au laana na baada ya tukio la kifo maelezo huzingatiwa sana ili kuondoa ule ukali wa kifo. Hata hivyo, vipo visaasili ambavyo hueleza chanzo cha kifo.

Kifo kilisawiriwa kwa njia mbalimbali. Kifo kilichotokea wakati wa mchana katika jamii ya Wajaluo hakikutangazwa hadharani, kilitangazwa wakati wa jioni kabisa. (Miruka 2001). Jamii ya Abanyole iliamini vifo vilitokana na nguvu za uchawi na ushirikina. (Mbiti 1969). Kwa hivyo, uhusiano kati ya wanaoishi na wafu umekuwa ukiendelea katika historia ya mwanadamu (Barley 1997).

## 1.1 SUALA LA UTAFITI

Utafiti huu umebainisha kuwa dhana ya uhai na kifo cha mwanadamu katika riwaya za Euphrase Kezilahabi*Nagona* na *Mzingile* ni kama safari inayoashiria maisha mapya na mazuri. Mtafiti amechunguza jinsi Kezilahabi ametumia taashira ya uhai na kifo kubainisha kuwa maisha ya mwanadamu ni mviringo Hivyo, utafiti huu umechunguza jinsi dhana ya uhai na kifo imesawiriwa kama duara kamili..

Riwaya hizi zimeonyesha kifo kama mwanzo wa uhai na zimesawiri maisha ya hapa duniani na maisha baada ya kifo. Hivyo, kifo sio mwisho wa kuishi lakini mwanadamu anaendelea kuishi maisha mapya hata baada ya kufa. Mwandishi ameonyesha ufungamano wa uhai na kifo katika jamii.

## 1.2 MASWALI YA UTAFITI

Ili kuafiki lengo la utafiti huu, tumeongozwa na maswali matatu ya kimsingi

1. Kezilahabi ametumia dhana ya kifo katika riwaya ya *Nagona* na *Mzingile* kwa dhamira gani?
2. Je, matokeo ya uhai na kifo katika riwaya ya *Nagona* na *Mzingile* ni yapi?
3. Je, mitazamo ya uhai na kifo katika riwaya ya *Nagona* na *Mzingile* ni ipi?

## 1.3 LENGO LA UTAFITI

Kuchunguza fumbo la uhai na kifo katika riwaya za Euphrase Kezilahabi *Nagona* na *Mzingile* ili kubainisha kuwa maisha ya mwanadamu ni mviringo na sio mstari ulio na kikomo.

## 1.4 SABABU ZA KUCHAGUA MADA

Utafiti huu umejikita katika uhakiki wa riwaya ya *Nagona*(2011) na *Mzingile*(2011) ambazo zimesawiri dhana ya uhai na kifo. Utafiti huu umeangazia maudhui ya uhai na kifo katika riwaya za Kiswahili. Riwaya hizi zimeendelea kusawiri dhana ya maisha. Sio rahisi kuelewa riwaya hizi kwa sababu ya mtindo na kunga za kifasihi alizotumia mwandishi na kwa hivyo zinawapa wahakiki changamoto katika kuzifafanua. Mwandishi ametalii juhudi za mwanadamu za kufahamu asili na hatima ya maisha yake na kwa sababu ya wazo hili, amepiga darubini uozo ambao umesambaa katika maisha ya mwanadamu kama vile mauaji yanayotokea duniani, unafiki na vifo vinavyotokana na binadamu kutofahamu mantiki yake ya kuishi. Euphrase Kezilahabi ametalii juhudi za mwanadamu za kufahamu utu wake. Riwaya hizi zina mtindo mpya wa kusawiri maudhui katika fasihi ya Kiswahili. Usimulizi umekwepa mtiririko wa moja kwa moja na sahili wenye kufuata mantiki. Falsafa ambayo imetumika katika riwaya hizi ni tatanishi na haieleweki kwa urahisi; Metafizikia, ambayo ni bunifu sana (Wamitila 1999).

Riwaya za hapo awali za Euphrase Kezilahabi zimesawiri uhalisia. Huu ni ufafanuzi wa vitu vilivyo ulimwenguni, dunia halisi na mambo ambayo yanaweza kudhihirika kihistoria na zina utamaushi wa hali ya juu. Riwaya ya *Nagona* na *Mzingile* imesawiri mambo ambayo yamevuka mipaka ya dunia halisi. Kifo ni jambo linalotokea kwa mwanadamu kutokana na majaliwa na linaondoa juhudi za mwanadamu za kutafuta na kufahamu asili ya maisha (Wamitila1997).

Riwaya ya *Nagona* ni ya kifalsafa. Imejaribu nadharia ya mwandishi na jinsi ya kuikabili fasihi ya Kiafrika ya wakati huu. Kimaudhui riwaya imelijadili suala gumu linalohusu kweli kamilifu. Kweli hii kamilifu imo katikati mwa duara ya maisha na kila mtu katika maisha wakati mmoja au mwingine huvutwa na kweli hii na pale kweli ilipo uwongo umejitenga. Mwandishi wa riwaya hii ameonyesha kuwa katika maisha mtu asidai kuwa na kweli mikononi mwake kwa sababu kweli haikubali mtu aimiliki peke yake, ni ya kila mtu.

Ili kuzielewa na kuzihakiki ipasavyo riwaya hizi mbili inabidi mhakiki ajifahamishe na nadharia na falsafa mbalimbali kama udhanaishi, metafizikia, fenomenolojia, uhalisiamazingaombwe miongoni mwa zingine. Mwandishi amejenga udadisi wake na kutumia masimulizi na itikadi kutoka sehemu mbalimbali za dunia kama vile Afrika, Asia, Ulaya huku akichanganya tamaduni za zamani na za sasa.

## 1.5 UPEO NA MIPAKA YA UTAFITI

Utafiti huu umejikita katika uchanganuzi wa riwaya mbili, *Nagona* na *Mzingile*. Kwa kuzingatia mitindo yake ya uandishi, Kezilahabi hajatumia uhalisia pekee lakini ametalii nyanja mbalimbali Gromov (1996), na Bertoncini (1999). Utafiti umeshughulikia dhanaya uhai na kifo cha mwanadamu kama duara. Ijapokuwa kuna maswala mengine mengi katika riwaya hizi hatukujishighulisha nazo kwa sababu lengo kuu la utafiti huu ni kubainisha kuwa maisha ya mwanadamu ni duara na sio mstari mrefu.

Mwandishi amepiga darubini juhudi za mwanadamu za kujaribu kufahamu asili ya maisha, amejaribu kutafakari uozo uliosambaa katika jamii, mauaji na vifo

vinavyotokana na mwanadamu mwenyewe. Mtafiti amechunguza na kudhihirisha athari na mitazamo ya dhana ya uhai na kifo katika riwaya ya *Nagona* na *Mzingile*.

## 1.6 YALIYOANDIKWA KUHUSU MADA

Riwaya ilizuka kutokana na maendeleo na mageuzi ya kitamaduni na viwanda. Kulingana na Wamitila (1984), njia kuu ya usimulizi wa riwaya ya *Nagona* ni ile ya kuyamwaga na kuyafululiza matukio, mawazo, falsafa na siasa ya mwandishi na kuyaacha yashikamane na mtiririko wa hadithi bila ya kiungo bayana cha ploti. Matokeo ya mpiko huu wa mawazo ya falsafa, siasa na matukio ya hadithi yanayofululiza, ndiyo hatimaye yanakuwa kiini cha maudhui ya uhai na kifo miongoni mwa maudhui mengine katika riwaya ya *Nagona* na *Mzingile*. Matukio ya kila kipengele cha jamii ya Kiafrika na matatizo ya kimataifa yamesimuliwa vipandevipande. Mbinu ya mwingilianomatini imetumika katika riwaya ya *Nagona* na *Mzingile*. Kezilahabi mara kwa mara ameazima dhana ya visaasili vya Kiafrika na ngano za kifasihisimulizi. Mambo mengi ya kiajabu na ya kimiujiza yametokea katika simulizi zinazoegemea mbinu ya uhalisiamazingaombwe.

Riwaya hii imetumia mkarara na marudiorudio kama inavyodhibitishwa katika riwaya ya *Mzingile*. Tumepata mfululizo mkubwa wa vikundi vya maneno vinavyoifanya kazi iwe ya kiistiari, ishara na vitajwa. Katika mfululizo na mkarara maneno kama ukweli, mshumaa, vichaa, vicheko, ungamo kuu, ukimya, njia, barabara, mto, paa, ndege, msitu, milima, mabonde, duara, vitabu, ndoto na mengine mengi yamefanya kazi iwe ya kutilia mkazo dhamira kama mapuuza, uharibifu wa mazingira, unyonyaji, upumbavu, unafiki, vifo na falsafa za urasimu. ( Bertoncini 1989).

Riwaya ya *Nagona* na *Mzingile* haina mipaka ya mahali na wakati. Kuna mipaka midogo sana ya maisha ya duniani na ya mbinguni na hakuna mipaka ya wanaoishi na waliokufa. Maisha ya mbinguni yanasawiriwa kiistiari na yanafananishwa na maisha ya hapa duniani, maisha yaliyojaa suitafahamu za kiitikadi, kidini, kisiasa, uonevu, unyonyaji, uongo, unafiki, ugomvi na vita (Bertoncini 1992).

Kezilahabi ameandika riwaya hii katika mtindo usiokuwa wa kawaida, mtindo wa uhalisiamazingaombwe na mwanzo wa riwaya ya *Nagona* na *Mzingile* ni wa kushtukia tu. Riwaya hii ni kielelezo cha kuibuka kwa mtindo mpya katika fasihi ya Kiswahili (Khamis 2005). Isitoshe, ni ya kimajaribio na imechukua mtindo wa ujumi wa kisasabaadaye na inaafiki kusawiri ukosefu wa uthabiti katika michakato ya kijamii. Uhalisia unawakilishwa kwa njia tofauti kabisa na unamruhusu mwandishi kuandamana na mtindo wenye fujo na haiba. Kupitia usimulizi wa vitendo vya mhusika mkuu tumeonyeshwa kuporomoka kwa jamii zetu na maafa yanayoelekea kuikumba dunia nzima. Wahusika wamepewa nguvu za kichawi na za kiujiza. Wanafalsafa Plato, Socrates, Aristotle, Hegel, Darwin, Marx, Freud na Nietszche tunajua wameshakufa lakini katika riwaya hii wamefufuliwa (Khamis 2003). Riwaya ya *Nagona* na *Mzingile* ni riwaya changamano. Kimaudhui riwaya ya *Nagona* ina mikondo miwili, mkondo wa kutazama maisha ya kimwetu na mkondo wa kujishughulisha na matatizo ya kimataifa. Mara kwa mara tunaonyeshwa uozo ambao tumeuzoea na kuujua vizuri.

Riwaya ya *Mzingile* ina mitazamo mbalimbali inayosimuliwa na wahusika tofauti na ni vigumu kujua mazingira ya hadithi yenyewe. Baadhi ya visehemu ni kama vipo katika ng'ambo ya pili ambapo ni wafu tu wanaweza kufikia. Sifa kuu ya kimaudhui

miongoni mwa sifa kadhaa kama umoja wa wahusika, utofauti wa hali za akili na hali ya kujitambulisha, ni ile ya kushughulikia kwa kina matatizo yanayoukabili ulimwengu. Riwaya hii imekiuka mipaka ya kitaifa na kieneo. Riwaya za hapo awali za Euphrase Kezilahabi zimejikita kwenye uhalisia mkavu usiotalii na kukaidi mipaka.

Kulingana na historia, suala la uhai na kifo limekuwepo tangu zamani. Katika riwaya ya *Bina-Adamu!*, kuna dhana ya fikra kuwa binadamu hafi lakini anapita tu katika dunia nyingine ya kutoonekana na anakuwa mzuka. Kutokana na ndoto ya Bina-Adamu, hana hakika kama yupo au hayupo, anaishi au amekufa. Pia katika riwaya hii kuna miujiza ya aliye hai, ana uwezo wa kujiua, kijifufua tena, kujigeuza na kuwa mchwa na kurejea tena katika umbo la binadamu, kuzama chini ya ardhi, kuibuka baharini na ghafla kukanyaga nchi kavu. Riwaya ya *Nagona* na *Mzingile* imechunguza ukweli unaosawiriwa kupitia nyuso nyingi. Kuishi, kuwepo na kifo ni aina moja ya usawiri huu.

Riwaya ya *Babu Alipofufuka* na *Bina-Adamu!* zina motifu ya safari, jasira na tendi za ulimwengu kama ilivyo katika riwaya ya *Nagona* na *Mzingile.* Riwaya hizi zinahusu matatizo yanayoukabili ulimwengu wote. Kazi hizi zote zimewekewa msingi na fasihi simulizi ya Kiafrika na fasihi simulizi haina mipaka.

Mose (2005), alitafiti kuhusu taashira ya kifo katika fasihi ya Kiswahili. Mtafiti huyu alitafiti tamthilia nne na kufikia sasa ni wazi kuwa hakuna utafiti uliofanywa kuhusu fumbo la uhai na kifo katika riwaya za Kiswahili.

Kwa kuzingatia kazi tulizorejelea, ni wazi kuwa waandishi wa riwaya *Bina-Adamu!*, *Babu Alipofufuka*, *Nagona* na *Mzingile* wamo kwenye tapo moja la sanaa za kimajaribio zinazojaribu kufaulu pale uhalisia umefeli katika kuwepo kwa mwanadamu. Riwaya hizi ni ikirari ya ukosefu wa uthabiti wa kijamii, kisiasa na kiuchumi na zinatia mchanga kitumbua cha imani kwamba kuna *uasilia* katika kutunga kazi za kubuni. Riwaya hizi zimeandikwa kwa kuzingatia kaida na kunga za uhalisiamazingaombwe ambao umejenga jumuiya pana na inayoendelea kupanuka kote duniani kila uchao. Isitoshe, zina mvuto wa hali ya juu na zinaonyesha kuibuka kwa mitindo mipya ya kusawiri maudhui katika fasihi ya Kiswahili.

Kutokana na maoni ya wataalamu na waandishi hawa ni wazi kwamba kuna haja ya utafiti unaoongozwa na nadharia mwafaka kuhusu suala la uhai na kifo. Utafiti wetu utashirikisha maelezo haya yote tuliyopitia ili tuweze kuelewa kwa mapana na marefu jinsi dhana ya uhai na kifo ilivyosawiriwa katika riwaya ya *Nagona* na *Mzingile*.

## 1.7 MISINGI YA NADHARIA

Utafiti huu umetumia nadharia mseto. Nadharia ya kikale iliyoasisiwa na Northrop Frye (1912-1991) na nadharia ya uhalisiamazingaombwe iliyoasisiwa na Franz Roh (1925).

Kulingana na Frye (1957) na Wafula (2007), vikale ni picha kongwe zinazotokea mara kwa mara katika kazi ya fasihi.Vikale hivi vinaweza kuwa taswira, wahusika, miundo ya usimuliaji na kadhia nyingine zinazopatikana popote pale ulimwenguni. Nadharia hii hudhihirisha bayana visasili na vikale ambavyo vimeenea kote

ulimwenguni. Kazi ya Northrop Frye *Anatomy of Criticism* (1957) ilitambulisha nadharia hii ya kikale.

Nadharia ya kikale hufafanua matini kwa kuchunguza kiini cha visasili vinavyorudiwarudiwa katika hadithi, ishara na taswira. Pamoja na kutumia wahusika, wahakiki wamefuata mkabala wa kikale kuzungumzia fasihi kwa kuzingatia maudhui yanayopatikana katika fasihi. Maudhui haya ni kama kikale cha mauti, uwezo wa kufufuka, uwezo wa kufasiri ndoto, kuwaasa wanaoishi, wema na uovu na kutumia hali ya angani kuzungumzia hali ya maisha ya mwanadamu.

Kulingana na Northrop Frye, fasihi ndiyo "kiini cha upanuzi wa visasili vya kubuniwa"… kila jamii ya mwanadamu inamiliki visaasili ambavyo huwa anuwai. Kuna kategoria mbili za msingi katika muundo wa Frye, futuhi na tanzia. Ulimwengu wa futuhi unasawiri matamanio yaliyotimizwa na kuwa na usawa lakini ulimwengu wa tanzia ni wa utengano, uonevu na maanguko ya nguli (Abrams 1993). Kwa hivyo utendakazi wa visaasili na fasihi huwa katika dunia moja iliyo bunifu ambayo imetawaliwa na makubaliano ya hali za kipekee.

Uhakiki wa nadharia ya kikale una misingi yake katika kazi ya Carl Gustav Jung iliyoanza miaka ya 1930s na imehusiana sana na dhana ya ung'amuzibwete jumuishi. Hii ni sehemu ya akili ya binadamu ambayo ina sifa zinazofanana katika binadamu wote na inahusiana kwa kiasi kikubwa na sehemu ya uridhi wa kimaumbile. Mtaalamu huyu anasema kuwa katika sehemu hii hupatikana vikale. Vikale havijitokezi waziwazi bali hujitokeza kwa njia ya motifu na ishara fulani.

Kulingana na Jung, binadamu wote huwa na ung'amuzibwete jumuishi na jambo hili hudhihirishwa kupitia ndoto, visaasili na fasihi. Ndoto na visaasili ni kundi la taswira ya kikale na binadamu huogopa na amekataa kuwepo kwa ndoto na visaasili. Huu umekuwa mwelekeo wa mwanadamu wa kisasa, mwanadamu anayetaka kuishi maisha ambayo ni razini na aliyodhibiti kupitia kwa ufahamu wake.

Kulingana na Jung ruwaza za vikale zimo ndani ya "ung'amuzibwete jumuishi" na huhusisha kumbukumbu za jamii mbalimbali, matukio na uhusiano wao tangu zama za kale. Uhakiki wa vikale unahoji kuwa kuna ishara, taswira, wahusika na motifu za pamoja ambazo hudokeza mwitikio sawa kwa binadamu wote. Jung aliamini kuwa vikale ni nguvu za asili ambazo zina utendakazi wa lazima katika uumbaji wa ulimwengu na katika akili ya mwanadamu.

Fasihi ya kikale huwa na mabadiliko makubwa ya visaasili vinavyojirudiarudia (muhula mzima) katika ruwaza ifuatayo; nguli anaanza maisha mahali pa raha (kama shamba), nguli anahamishwa kutoka mahali pa raha (utengano), nguli anavumilia wakati wa majaribu na taabu na mara nyingi huwa mizunguko (safari), nguli anapata utambuzi wa nafsi yake kutokana na mapambano ya safari hiyo, nguli anarudi mahali pa raha (pengine mahali pale pa asili au mahali pazuri zaidi). Sura ya vikale ambayo hupatikana sana ni uchunguzi wa nguli ambaye ni lazima atoke nyumbani, asafiri hadi eneo asilolifahamu, akutane na kiongozi, avumilie hali ngumu, afikie alichokuwa akitafuta, apate ujuzi mpya na arudi nyumbani na ujuzi huo ili agawane na wengine.

Tamaduni zote huwa na hisia mgawanyo za misingi ya ishara.Visasili huakisi muundo wa kitamaduni wa jamii inayohusika. Kuna kisasili ambacho huonyesha muhula

mzima wa maisha ya mwanadamu. Maisha huwa na ruwaza ya kuzaliwa na ujana, kukua, utu uzima na kifo. Huu ni muhula mzima usio na mwisho.

Frye anafasiri mtazamo wa Jung kwa njia tofauti. Frye anaamini kuwa kazi ya kifasihi huwa na misuko au ruwaza ambazo kimsingi hutokana na visasili. Frye anasema ruwaza za taswira zinazopatikana katika kazi ya fasihi zinaweza kuonekana katika visasili kupitia matambiko ya mwanadamu kutoka zama za kale. Matambiko haya ni mwitikio wa muhula mzima wa kiumbehai. Frye alipanua nadharia ya kikale ili kuweka dhana na hali za tamaduni nyingi. Jinsi vikale vilikuja kuwepo sio hoja kwa Frye lakini hoja ni utendakazi na athari ya vikale.

Mihimili ya nadharia ya vikale ambayo imeongoza utafiti huu ni;

1. Misingi ya miundo ya fasihi ya vikale ina uhusiano mkubwa na visasili na matatizo makuu yanayokumba jamii mbalimbali ulimwenguni.
2. Sanaa ya ubunifu inatoka kwa visasili na vikale na kwenda kwa wigo wa jazanda ambazo zinafikia kiwango kinachowakilisha hali halisi ya maisha.
3. Uhalisia huanza kwa uchunguzi wa visasili na vikale vilivyo katika mipaka ya matamanio asilia ya walimwengu.

Nadharia ya uhalisiamazingazombwe imejadiliwa na Shannin Schroeder (2004). Kulingana na Schroeder Franz Roh ndiye alivumbua matumizi ya neno 'Magischer Realismus' mnamo (1925) kwa maana ya uhalisiaajabu katika kazi yake juu ya mtindo wa sanaa ya kisasa ya ulaya enzi zile.

Kulingana na D'Haen (2005), Roh alilibuni neno hili kuelekeza michoro iliyo na uhalisia kama ya picha ya kamera lakini ambayo iliibua hisia za kutokuwa halisi kwa

Kiswahili Resource Centre

kuchanganya uhalisia na uajabu. Anaeleza kwa usahihi kwamba uhalisia mazingaombwe ni tawi la usasabaadaye linaloonyesha sifa kama kujirejearejea, uziada uliopindukia, uanuwai, mseto wa vitu, mwingilianomatini, kuchezea na kuyumbisha uthabiti wa wahusika, kumchanganya msomaji kwa maksudi na hali kadhalika kufuta mipaka ya dhana, vitu au hali tofauti. Uhalisiamazingaombwe ni mtindo au aina ya fasihi ambamo mambo ambayo hayafanani na ya kawaida na yaliyozoeleka kwa hadhira hutokea sambamba na yale ambayo ni ya kawaida.Yote haya hutokea katika mandhari au mazingira ambayo kwa kiasi kikubwa sana yana uhalisi tunaoujua. Istilahi hii imetumika kwa wingi sana katika fasihi, sanaa na filamu.

Stretcher (1999) anasema, uhalisiamazingaombwe ni yale mambo ambayo hutokea pale ambapo mandhari na matukio ya kihalisi yanavamiwa na jambo ambalo ni la ajabu mno na ni vigumu kuaminika. Istilahi hii ilitumiwa hapo mwanzo na mhakiki wa sanaa wa Kijerumani Franz Roh alipokuwa akitoa maelezo ya picha iliyoonyesha *uhalisi uliopindwa.*

Uhalisiamazingaombwe ni mkabala wa kuuwakilisha uhalisia kwa kukiuka mipaka, kuhujumu au kuvuruga usimulizi mbali na kukaidi kaida za lugha. Na ingawa ni mkabala wa kifasihi, unaonasibishwa zaidi na uandishi wa Amerika kusini, umepenya kwingi duniani huku fasihi za janibu mbalimbali zikizungumziana kwa dayolojia hii. Hivyo, uhalisiamazingaombwe unaafiki, kutalii na kukaidi mipaka, si hoja kama mipaka hiyo ni ya kiontolojia, kisiasa, kijiografia au kiutanzu (Zamora 2005).

Nadharia ya uhalisiamazingaombwe mwaka wa (2008) ilifafanuliwa katika fasihi kama aina ya usasa wa kubuniwa ambapo matukio ya ajabu na ya fantasia yanawekwa pamoja katika masimulizi. Riwaya ya sasa imekiuka mipaka ya uhalisia na inatumia hekaya au ngano fupi, vijihadithi na visasili huku ikisawiri wakati uliopo. Sifa za fantasia zinazopewa wahusika katika riwaya za aina hii kama, uangamo, safari ya angani na telepathia ni njia mojawapo ambapo uhalisiamazingaombwe hufuata ili kujumuisha siasa za kweli za karne ya 20.

Nadharia ya uhalisiamazingaombwe hunuia kueleza fumbo la vinyume na inatofautiana na fantasia kwa sababu matukio yake yanapatikana katika ulimwengu halisi na wa kisasa unaosawiri binadamu na jamii kwa jumla. kulingana na Angel na Flores, uhalisiamazingaombwe unahusu mambo halisi lakini yamejaa fantasia.

Mihimili ifuatayo imeongoza utafiti huu,

1) Usawiri wa matukio ya kiajabuajabu, ya kushangaza na ya kuogofya.
2) Ukiukaji wa mipaka ya uhalisia, ndoto na wakati.
3) Kuonyesha uhusiano wa wakati na mahali.
4) Usawiri wa mbinu za usimulizi, visasili na hadithi.
5) Usawiri wa uhai na kifo.

## 1.8MBINU ZA UTAFITI

### 1.8.1 MAHALI PA UTAFITI

Utafiti umefanywa maktabani ambayo ndiyo njia kuu ya utafiti huu. Ili kupata data faafu kwa mada ya utafiti, maandishi mbalimbali yamepitiwa maktabani ikiwa ni pamoja na majarida, vitabu, makala na mtandao. Aidha, vitabu vya fasihi

vilivyoteuliwa kwa minajili ya mada hii, *Nagona* (2011) na *Mzingile* (2011) vya Euphrase Kezilahabi vilichanganuliwa kwa kina ili kupata data iliyofaa. Kazi zingine za mwandishi zimesomwa ili kumwongoza mtafiti katika kuiweka kazi hii katika mkabala wake.

Katika maktaba tulipata data kutoka vitabu kama vile *Anatomy of criticism:Four Essays*, *Africans and Philosophy*, *Arhetypal Critism* miongoni mwa vingine. Pia tumepata makala mbalimbali katika mtandao yanayoeleza zaidi juu ya nadharia ya kikale na uhalisiamazingaombwe.

### 1.8.2 UTEUZI WA SAMPULI

Mbinu ya sampuli iliyotumiwa ya uteuzi ni ya kimaksudi. Riwaya za *Nagona* (2011) na *Mzingile* (2011) zimeteuliwa kutokana na uchunguzi wa mtafiti kupitia usomaji wa kina na uchambuzi, riwaya hii imechukua dhima ya uchunguzi wa jamii na imejishughulisha na mada mbalimbali za kimaudhui kuhusu matatizo yanayoikabili dunia yote. Kuna matambiko yayohusiana na miungu na uhalisia mpya ambao una ukweli wa aina nyingine kabisa; uhalisia wenye mkanganyiko na utata. Riwaya ya *Nagona* imejishughulisha mno na suala la kutafuta ukweli. Riwaya hii ina miketo ya kifilosofia, dini, saikolojia, maneno ya mitume waliofufuka na wahusika wengine wenye uwezo wa kuishi maelfu ya miaka. Miketo hii imepachikwa kimbambizoviraka juu ya matini kuu ya *Nagona*.

### 1.8.3 UKUSANYAJI DATA

Data ya utafiti huu imekusanywa maktabani kupitia usomaji mpana ambapo mtafiti amesoma vitabu, tasnifi na majarida mbalimbali. Maandishi yanayolenga nadharia ya

kikale na uhalisiamazingaombwe yamesomwa pamoja na riwaya zilizoteuliwa *Nagona* (2011) na *Mzingile* (2011). Mtafiti amesoma riwaya hizi kwa kina kwa kuyatenga na kuyaandika mambo yote yaliyo muhimu ili kutosheleza mahitaji ya utafiti. Mambo yaliyotengwa ni pamoja na jinsi dhana ya uhai na kifo ilivyotumika katika riwaya ya *Nagona*, athari za uhai na kifo na mitazamo ya uhai na kifo katika riwaya ya *Nagona* na *Mzingile*..

### 1.8.4 UCHANGANUZI WA DATA

Data iliyokusanywa imechanganuliwa ili kuafiki malengo ya utafiti. Mtafiti amechanganua maudhui ya uhai na kifo, athari za uhai na kifo na mitazamo ya uhai na kifo katika riwaya ya *Nagona* na *Mzingile* katika mkabala wa nadharia ya Kikale na ya Uhalisiaajabu. Utafiti huu umebainisha mifano ya uhai na kifo na kuichanganua kwa kutumia nadharia ya Kikale na ya Uhalisiaajabu. Tumetumia mifano mbalimbali kudhihirisha matumizi ya vikale na uhalisiaajabu

Utafiti ulioanisha mihimili ya nadharia ya kikale na uhalisiamazingaombwe na matukio mbalimbali katika riwaya ya *Nagona* na *Mzingile*. Matukio ya uhai na kifo yamesawiriwa na kuelezwa bayana kwa kufuata hatua zifuatazo, kudondoa sehemu matukio ya uhai na kifo yamesawiriwa, kuonyesha jinsi dhana ya uhai na kifo imesawiriwa na kuonyesha athari ya uhai na kifo katika riwaya ya *Nagona* na *Mzingile*.

Mwisho, tumeonyesha mafanikio ya utafiti, matatizo tuliyokumbana nayo katika ukusanyaji na uchanganuzi wa data, mchango na baadaye tumetoa mapendekezo ya nyanja za kufanyia utafiti zaidi.

## 1.9. UWASILISHAJI WA MATOKEO YA UTAFITI

Matokeo ya data yamewasilishwa kwa njia ya maelezo. Maelezo haya yamezingatia maudhui yanayotumiwa kusawiri dhana ya uhai na kifo, athari za uhai na kifo na mitazamo ya uhai na kifo katika riwaya ya *Nagona* (2011) na *Mzingile* (2011). Uwasilishaji wa data umefanywa kwa kuongozwa na malengo ya utafiti.

Matokeo yamewasilishwa katika sura ya tatu, nne na tano.

# SURA YA PILI

# HISTORIA, MAANDISHI NA FALSAFA ZA E. KEZILAHABI

## 2.0 UTANGULIZI

Sura hii inahusu muhtasari wa maisha, tajriba na maandishi ya Kezilahabi amabayo tumetumia kama dira ya kuangazia riwaya zake mbili *Nagona* na *Mzingile* na kubainisha falsafa na kunga za kifasihi katika uandishi wake. Utafiti umeanza kwa kutoa ufafanuzi wa dhana ya fumbo.

Fumbo hutumika kueleza jambo ambalo haliwezi kueleweka waziwazi kwa mantiki au chochote kinachokosa ufafanuzi. Kila mwandishi anajaribu kuonyesha uhalisia kama unavyojidhihirisha katika uthabiti wa maisha yetu na hawezi kufanya hivi bila kupewa talanta kama chombo cha kutumia. Kila mwandishi ana mtindo wake wa uandishi na matumizi ya mafumbo ni mojawapo ya mitindo. Mtindo ni jinsi ya kujieleza na msanii hueleza mambo ya kawaida kisanii ili yalete maana ya ndani. Hivyo basi uteuzi wa tamathali na msamiati hutegemea mtindo wa msanii binafsi.

Mtindo sio yale mwandishi anaandika lakini ni jinsi anavyoyaandika na kuyawasilisha. Ni mbinu ya mwandishi ya kipekee ya kuwasilisha mawazo. Mwandishi huchagua mtindo wake kwa kutumia maneno na hurekebisha mitindo ya uandishi wake kupitia uzoefu wake wa kuandika kazi mbalimbali.

## 2.1 KUMHUSU MWANDISHI EUPHRASE KEZILAHABI

### 2.1.1 MAISHA YAKE

Euphrase Kezilahabi ni mmojawapo wa watunzi na wasomi wa fasihi ya Kiswahili ambao wanajitokeza kwa ukomavu wao katika utunzi na uhakiki wa kazi za fasihii.

Anajulikana kwa kujaribu mitindo mipya katika uandishi wake na tukisoma kazi zake tunakutana na chembechembe za upya katika maudhui na kunga za kifasihi anazotumia

Kezilahabi alizaliwa mwaka wa 1944, Ukerewe katika kijiji cha Namagongo kilichoko ziwa Victioria Tanzania. Alisoma shule ya msingi ya Nakasayenge halafu tangu 1957 seminari ya Kikatoliki ya Nyegezi aliyomaliza mwaka wa 1966. Mwaka wa 1967, alijiunga na chuo kikuu cha Dar es Salaam akasomea ualimu na fasihi hadi akahitimu mwaka wa 1970. Alifundisha katika shule mbalimbali nchini Tanzania kabla ya kujiunga na chuo Kkikuu cha Dar es Salaam alikofuzu kwa shahada ya uzamili mwaka wa 1976. Baadaye alijiunga na Chuo Kikikuu cha Wisconsin Madison, Marekani alikopata shahada ya pili ya uzamili 1982 na baadaye akapata shahada ya uzamifu.

Profesa Kezilahabi alikuwa mhadhiri wa Kiswahili kwa miaka mingi katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na amewahi kuwa mkuu wa idara ya Kiswahili. Aidha, amewahi kuwa mwenyekiti wa umoja wa uandishi wa vitabu wa Tanzania na mwanachama wa Baraza la Kiswahili la Taifa. Hivi sasa yeye ni Profesa wa lugha na fasihi katika Chuo Kikuu cha Botswana.

### 2.1.2 KAZI ZAKE

Kezilahabi ni mwandishi wa mashairi, hadithi fupi, riwaya na tamthilia. Katika kazi hizi, Kezilahabi anataka wasomaji wake wadadisi nafsi zao, mazingira yao, siasa yao, ujitambuzinafsi wao, ulimwengu wao na hata maisha kwa jumla. Mwandishi amezungumzia maswala mengi yakiwemo, utawala mbaya, umuhimu wa kuelimisha

jamii bila ya ubaguzi wa misingi ya kijinsia, dini, maisha na hali ya kuwako kwa binadamu ulimwenguni na kifo. Motifu ya safari ni muhimu katika kazi zake za hivi karibuni ambapo binadamu yupo kwenye safari ya maisha yake ulimwenguni. Binadamu anapaswa kuichunguza jamii yake kwa jicho la upembuzi kama mtembeaji mzuri anayeijua njia anayoitumia. Uhai na kifo ni mojawapo ya kunga za kifasihi anazotumia kuelezea maana na utata wa maisha.

Sifa moja ya kifani ambayo wasomaji wote wa Euphrase Kezilahabi wanahusisha na uandishi wake ni ucheshi. Mwandishi humchochea msomaji wake ajicheke lakini amalizapo kufanya hivyo akereke kwa kuutambua ulimwengu wake. Ucheshi ni nyenzo muhimu na kubwa ya tashtiti inayotokea katika sanaa ya mwandishi huyu na huubuliwa kupitia taswira. Taswira zinazotawala uandishi wa Kezilahabi zimekitwa kwenye maisha ya mtu wa kawaida. Msomaji havutiwi na udhati na uzito wa yanayozungumziwa pekee, bali pia jinsi yanavyozungumziwa pamoja na uteuzi wa sitiari na taswira zisizouakisi Uafrika pekee.

Kimya ni kichocheo cha ubunifu katika utunzi wa Euphrase Kezilahabi. Kuna kimya cha usomaji, kimya cha uhakiki na muhimu zaidi kimya cha ufu. Ni katika kimya ambako mengi yanaibuka.

Kezilahabi anabainish maana na utulivu katika ulimwengu unaotawaliwa na uhalisi wa fujo na dhuluma. Anabainisha dhima hiyo kwa kumchochea msomaji ajichunguze kwa kina.

### 2.1.3 TAJRIBA YAKE

Kezilahabi alizaliwa na kulelewa katika mazingira ya ukulima na ufugaji. Hii ndiyo sababu kazi zake zinajishughulisha na maisha ya shamba. Baba yake alikuwa mkuu wa kijiji na alileta maendeleo katika kijiji chake. Pia, ni mwanafasihi na mwandishi mashuhuri wa kisasa. Ni msomi na mtaalamu aliyefunza fasihi katika vyuo vikuu kwa muda mrefu. Hivi sasa ni Profesa wa lugha na fasihi katika Chuo Kikuu cha Botswana,

Maisha ya mwanadamu ni swala moja analojishughulisha nalo sana katika kazi zake za sanaa. Analiangalia swala hili katika mikabala miwili, mkabala wa mtu binafsi na wa jamii. Anamchunguza mtu katika hatua zake zote kama vile kuzaliwa, ujana, malezi, ndoa, uzee hadi kifo huku akitathmini fumbo lililoko katika kila mojawapo ya hatua hizi. Maswala haya ndiyo yamemwathiri mwandishi huyu katika kazi zake hasa riwaya.

Maisha ya Kiseminari pia yamemwathiri Kezilahabi katika uandishi wake. Riwaya ya *Rosa Mistika* ni dhihirisho ya athari hizi. Athari hizi pia tunaziona katika riwaya ya *Gamba la Nyoka* ambapo anaonyesha Uafriti na unafiki wa mapadri kupitia kwa mhusika Padri Madevu na ngoma zake na mama Tinda. Katika riwaya ya *Kichwamaji* mwandishi anatalii maswala ya kifalsafa, ya maana ya maisha, kutokuweko au kuweko kwa Mungu, ukengeushi, ukoloni na elimu ya ukoloni pamoja na athari zake kwa msomi Mwafrika.

Baada ya kuandika riwaya nne za kihalisia miaka ya sabini, Kezilahabi ametalii nyanja nyingine kabisa. Riwaya zake mbili za hivi karibuni *Nagona* na *Mzingile* zimewakanganya wahakiki wa maandishi ya fasihi. Kwa hakika ni mkusanyiko wa kazi mbalimbali kama zile za uhalisia, uhalisiamazingaombwe, sayansi ya kubuni, fumbo, na visasili vya kale kupitia njia ya uchunguzi. Kezilahabi amefaulu katika kuvuruga msomaji kuhusu utambuzi wa mhusika mwenye fumbo *Nagona.*

### 2.1.4 WATU WALIOMWATHIRI

Kezilahabi ameathiriwa sana na waandishi wa udhanaishi kama Martin Heidegger (1889-1976) na Friedrich Nietzsche (1879-1888) hata kama yeye mwenyewe anaeleza kuhusu falsafa nyingine kabisa anayoita falsafa ya Kiafrika.

Fikra za Heidegger zimechangia katika uwanja wa finolojia, hameniutiki, nadharia ya siasa, saikolojia na elimu ya dini. Uhakiki wa Heidegger wa utamaduni wa metafizikia, upinzani wa falsafa umbile na dunia ya teknolojia inayotawala umekubaliwa na wananadharia wa usasabaadaye. Jambo lililomvutia sana Heidegger ni ontolojia. Alikosoa utamaduni wa kimagharibi ambao aliona kuwa ukataaji wa dini na sheria za ubinadamu zote, kwani anasema swala la mwanadamu limetokana na maswala haya. Mwanadamu hujipata kila wakati katika hali ya kiroho au ya mwili. Jambo hili huwakilisha tukio la awali kama lilikuwa. Uhai huwa kati ya wanadamu wote na umoja halisi wa wakati wa baadaye, uliopita na wakati uliopo.

Heidegger anasema katika utamaduni wa falsafa kwa jumla imekubalika kuwa mwanadamu mwenye uhai ni dhana ya kila mahali, dhana ya nafsi, dhana isiyoweza kufafanuliwa kwa kutumia dhana zingine. Heidegger amedai kuwa, hata kama

tunaonekana kuelewa mwanadamu mwenye uhai, mwanadamu bado yumo gizani. Anaendelea kusema kifo ni kifunguo cha uhai. Anashikilia wazo kuwa wanadamu wenye uhai na wanadamu wenye uhai pekee ndio wanaoishi kikamilifu. Heidegger anasema,

> *Tunazaliwa katika dunia ya kufuatana. Kwanza, kila jambo tunalosema, kufanya, kufikiri na kuamini limefanywa, limesemwa na kufikiriwa. Mambo tunayoona yakiwa na maana ya wakati wetu, misingi ya thamani na maana tunayofuata, mitindo na njia tunayofuata imetokana na jamii zetu mbalimbali*

Kulingana na Kezilahabi, Heidegger ni mmoja kati ya wanafalsafa wa kimagharibi ambao wamechunguza kwa njia ya makini sana ulimwengu wa kimagharibi na kwa hivyo kumwona kama mtu anayeondoa ukungu. Kezilahabi ameathiriwa na Heidegger katika wazo kuwa kuwepo kwa mwanadamu ni kweli inayohitaji kugunduliwa.

Nietzsche ni mmoja wa wanafalsfa ambao hawaeleweki na ni mwanafalsafa mwenye ushawishi mkubwa kwa wasomi tangu wakati wa Aristotle na Plato. Aliandika kuhusu falsafa ya Ugiriki, hali ya ukweli na ujuzi, thamani na maadili ya kisasa na maana ya kuwa mwanadamu. Alibuni dhana ya kurudi milele. Uhakiki wa kazi nyingi za Nietzsche kwa ulimwengu wa kisasa umeenea na maandishi yake ni kama ya kinabii. Nietzsche amekataa dini na sheria zi ubinadamu zote. Alikuwa mtetezi wa nguvu za nafsi.

Campbell anasema, Nietzsche amegundua kuwa mwanadamu yuko peke yake katika uumbaji wa maana ya maisha yake bali maana kama hii hapo awali ilkuwa maumbo ya pamoja kama methodolojia na dini. Nietzsche mwenyewe amesema,

> *Jaribio la kutoroka dini na sheria za ubinadamu bila ya kuwacha thamani ya hapo awali inaleta tu kinyume cha kutoroka. Jambo hili linatatiza Zaidi.*

Kutoka mwanzo wa karne ya ishirini, falsafa ya Nietzsche imekuwa na ushawishi kwa wasomi ulimwenguni kote. Kurudi milele ni dhana inayosema kuwa ulimwengu umekuwa ukijirudiarudia na utaendelea kujirudia na ni kurudi kwa mwanadamu mwenye uhai kwa mwili uleule. Anaendelea kusema dhana ya kurudi milele kwa mambo yote ni alama ya kuonyesha uhai.

Mbinu ya F. Nietzsche ya uhakiki imeathiri waaandishi wengi wenye mawazo ya kisasa akiwemo E. Kezilahabi. Nietzsche amekataa kuwepo kwa ukweli kamili. Anasema, "*wanadamu wote ni sawa.*" Alieleza kuhusu umakini wa "tatizo la ukweli" wakati usasa umefikia kilele chake. Anaendelea kusema,

> *Kila kitu kinachotofautisha mwanadamu na mnyama hutegemea uwezo wake wa kufukiza utambuzi wake wa sitiari katika upangaji ratibu na kwa hivyo kuyeyusha taswira kuwa wazo.*

Katika mahojiano na Gwachi Mayaka tarehe 5 machi 1991, Kezilahabi amekiri kuwa katika uandishi wake ameathiriwa sana na wanafalsafa Samuel Beckett na Albert Camus ambao ni wanafalsafa mashuhuri wa Ulaya, athari hizi ni bayana katika riwaya yake ya *Kichwamaji*

Falsafa ya kiafrika imewakilisha mikondo yote ya falsafa kutoka Afrika nzima. Ni mazungumzo ambayo yana uwezo wa kupata mawazo ya kifalsafa kutoka Afrika na kuendeleza ujuzi wake na pia uwezekano wa kuakisi uhakiki wa methodolojia yake na maendeleo ya vifaa vya utambuzi. Kama mazungumzo ya jumla, falsafa hii ina uwezo wa kuingiliana.

Kulingana na utamaduni wa kigeni, kurejelea maandishi sio tu kutafsiri isimu, lakini kuweka ubunifu katika muktadha mwingine .Mawazo ya Kezilahabi ya kuweka athari za falsafa za kimagharibi katika masimulizi yake na kuyapa nafasi katika lugha ya Kiswahili ni ya kuelimisha sana. Riwaya za Kezilahabi ni tahakiki ya dhana za msingi za falsafa ya kimagharibi.

Kama mijadala ya Plato ya wahusika kutoa maoni tofautitofauti, ndivyo yalivyo mawazo ya falsafa yanayoelezwa katika majadiliano ya kazi za kubuni kwa njia zinazowakilisha uhuru wa mwandishi na kejeli. Mawazo haya ya dhana mahsusi ya falsafa yanaanzishwa katika uwanja wa wasomi.

Suala la "asili" limeelezwa katika riwaya ya *Mzingile* wakati wa kukutana kiistaajabu na mhusika "mimi" na mwanasayansi anayekula mijusi. Mwanasayansi anaeleza mawazo yake kupitia mjadala na mhusika mkuu.

Mwanasayansi: *Binadamu kama angekuwa anatumia muda wake kuwaza na kufanya majaribio mengi, angekuwa amekwisha kishinda kifo. Angekuwa amepata mbinu za kujiumba kwa utashi wake mwenyewe au kuumba binadamu wengine kwenye maabara. Tunashindwa kugundua mchanaganyiko wa chembe hai? Wazo la kuwako kwa*

*chanzo cha mambo limetupumbaza muda wa karne nyingi, nalo wazo la ajali halikutusaidia Kutatua kitendawili* (Kezilahabi 2011).

Mjadala huu umeanzisha utofauti wa dhana kati ya fikra zinazochunguza asili ya vitu na fikra zinazochunguza utendakazi wake. Fikra za chanzo ni fikra za kimetafizikia, vyanzo huamua asili ya vitu na asili huleta athari kwa vitu hivyo. Fikra za kimetafizikia za chanzo ziliruhusu falsafa za kimagharibi kutoka kipindi cha Socrates hadi karne ya kumi na tisa. Jambo linalotatanisha katika wazo la metafizikia ni fikra inayohusu falsafa ya Kiafrika. Kezilahabi anasema katika hitimisho la tasnifu yake iitwayo "*Errata or a tragedy of errors,*"

*Afrika imejaa maadili potovu ya falsafa za vyanzo. Katika ulimwengu wa Kimagharibi, hii falsafa ilitokana na Nazi Germany. Falsafa iliyo kongwe siyo lazima iwe karibu na utu wetu wala haina mamlaka ya kuongoza wakati uliopo. Haijalishi ama sisi ndio waridhi wa kweli wa "hiba iliyoibiwa". Kinachojali ni sisi ni nini. Falsafa ya vyanzo ni jambo kubwa la kifashisti. Falsafa za vyanzo ni makosa mengine* (Kezilahabi 1985).

Hiba iliyoibiwa imetokana na kitabu kilichoandikwa na George G.M James mwaka wa 1954 kinachodai kuwa ustaarabu wa Misri ulikuwa wa Waafrika weusi na pia falsafa ya Kigiriki ilikuwa imeibiwa kutoka Misri ya kale. Kezilahabi amekubaliana na mwanafalsafa kutoka kameroon Marcien Towa anayesema,

*Kugundua falsafa halisi ya Mwafrika mweusi itaonyesha kwa hakika ya Kwamba wahenga wetu walikuwa wanafalsafa bila kutuondoa kwenye wajibu wa kujipa ufalsafa sisi wenyewe {...} Falsafa huanza na uamuzi wa kutegemea ufalsafa na uridhi uliosanifiwa na*

*binadamu kwa uhakiki usio na huruma* (Kezilahabi 1985).

## 2.2 MAWAZO KATIKA RIWAYA ZAKE

Historia ya E. Kezilahabi kuhusu uandishi wake imejidhihirisha wazi hasa kutokana na vitabu alivyowahi kuandika. Kazi za mwanzo za Kezilahabi zimesheheni vifo na maudhui haya ndiyo kiini cha kazi zake. Msomaji anapata picha finyu ya mwanadamu hata kama inahusu kuleta utambuzi wa yale yote yaliyo kwenye giza na yaliyojaa maswali kuhusu kuishi na kuweko.

Diegner amegawa riwaya za Kezilahabi katika vipindi viwili bunifu. Kipindi cha kwanza kimebeba riwaya zake za hapo mwanzo *Rosa Mistika* (1971), *Kichwamaji* (1974), *Dunia Uwanja wa Fujo* (1975), *Gamba la Nyoka* (1979) na sifa moja ni mtindo wake rahisi ambao unajulikana kama "uhalisia." Ameandika kwa uhalisi ili aweze kuwasilisha maudhui magumu kwa njia rahisi ili aweze kueleweka na watu wengi.

Maudhui ya kifo yamechukua nafasi muhimu sana katika kazi zake za mwanzo. Kezilahabi anasema,

> *Ni vile ninavyoona tanzia, kifo huweka mpaka wa ustawi wa tanzia mahali ambapo binadamu anaweza kupata utambuzi wa matukio ya hapo awali* (Bertoncini 1989).

Sifa nyingine katika kazi ya Kezilahabi ambayo imefika katika upeo wa juu kabisa ni ile ya kujihusisha na maswala ya falsafa na maana ya maisha. Kushika siku ya leo na kutoamini kesho sana ni wazo ambalo limeshikwa vizuri kitaswira na kwa mapana yake.

Falsafa ya Kezilahabi inaenda kiwango kingine katika riwaya ya *Kichwamaji*. Riwaya hii inachunguza dhana ya utengano na kuambatana na athari zake kuna migongano ya mielekeo ya vizazi. Pia,anajishughulisha na suala la maisha, maana yake au kutokuwa na maana, nafasi ya nafsi na dhana ya furaha isiyoepukika.Wahusika katika riwaya hii wanapitia bwawa la maisha. Vijiji vimesambaa uchawi, ulipizaji kisasi kuhusu mambo madogomadogo, wivu, usherati na uozo wa maadili. Maisha duniani yamesawiriwa kama jambo lisilopendeza kwa mwanadamu lakini kama jambo la wakati mfupi. Dunia imejaa ufisadi na ni ziwa lililojaa maovu ya kila aina. Kikale cha ndege katika riwaya hii ni kiwakilishi cha hali ya maisha duniani. Kezilahabi anaonya wasomaji kuhusu dunia iliyoharibika na anasema ni ziwa lililo na gadhabu. Maisha ya mwanadamu yameonyeshwa kama mchanganyiko wa mambo mengi yasiyokamilika

Riwaya ya *Gamba la Nyoka* inaonyesha ukatili na ukosefu wa utu unaoonyeshwa kupitia utekelezaji wa ujamaa nchini Tanzania. Riwaya hii pia inaendeleza unafiki ulioenea na kusambaa katika Ukristo kupitia kwa Padri Madevu na mfuasi wake mama Tinda. Mwandishi anateka unafiki wa dini kwa njia ya ubeuzi na ya ucheshi.

Riwaya ya *Dunia Uwanja wa Fujo*, imesawiri dunia kama pahala pabaya , pa fujo na vurumai ambapo binadamu hupatwa na matatizo mengi katika uhai wake wote. Kezilahabi anasema,

> *Lakini dunia ngumu kueleweka. Hakujatokea nukta moja bila mwanadamu fulani kuwa msibani, mtu mmoja anapokunywa pombe anakufa, mwingine anapokimbia asipigwe na mvua mwingine analilia tone la maji* (Kezilahabi 1981).

Hii ndio picha ya dunia. Vijiji vimejaa maovu ya kila aina; ulipizaji kisasi, uchawi, wizi na ghasia za watu wenye fujo.

Falsafa ya Kezilahabi inafika kilele katika riwaya zake mbili *Nagona* na *Mzingile*. Mawazo katika kazi hizi mbili ni tofauti na kazi zake za hapo mwanzo kwa njia mbalimbali. Kwanza, njia ya masimulizi ni tofauti kabisa, sio ya moja kwa moja na pia ni vigumu kuwatambua wahusika wake. Pia, mwandishi amepiga hatua katika kusawiri maudhui ya maisha yanayoashiriwa kwa kujaribu kuingia kwenye duara. Analenga kuonyesha maovu katika maisha ya mwanadamu kama vile, mauaji, unafiki wa kidini na vifo duniani. Kezilahabi amezama katika masomo yake ya falsafa na saikolojia na amebadilisha mtindo wake kabisa hivi kwamba kazi hizi ni ngumu kueleweka. Kutokana na upangaji wa Diegner tunapata kujua kwamba tasnifu ya Kezilahabi iliyoandikwa mwaka wa (1985) iko katikati ya vipindi hivi viwili. Mwandishi anatwambia kuwa itikadi zote duniani zinaelekea kwa jambo moja; kufasili uhalisia na kuelewa asili ya mwanadamu.

Riwaya ya *Mzingile* inaendeleza wazo hili la kutafuta maana ya uhai na asili likiashiriwa na mwanamke mwenye utelezi, ishara ambayo imeombwa kutoka kwa Friedrich Nietzsche. Pia, imesawiri dunia iliyojaa unafiki, mapinduzi, vurumai, maumivu ya hapa na sasa, unyang'anyi, ukosefu wa mipango na mapenzi. Mambo haya yanatikisa kitovu cha ulimwengu ambacho mwanadamu ameshikilia. Matokeo yake ni uoga wa kuhofia maangamizo ya maisha ya mwanadamu. Katika riwaya ya *Nagona* mwandishi ametaja unyang'anyaji wa uchumi duniani na jukumu la nchi za Kibepari, chama kilichoanzishwa na Hitler ambacho kilikuwa kigezo cha rangi au kabila, Waamerika wekundu, kafara kutoka India, ubeberu na ujumi.

Matini ya riwaya ya *Nagona* na *Mzingile* imejengwa kwa lugha faragha ya mwandishi mwenyewe anayejificha nyuma ya wahusika wake, lugha ambayo imo katika mkondo simulizi lakini kila mara inaingiliwa kati na miketo ya kifalsafa, dini, saikolojia, maneno ya mitume waliofufuka na wahusika wengine wenye uwezo wa kuishi maelfu ya miaka. Aidha, utafiti wetu umechunguza fumbo la uhai na kifo katika riwaya ya *Nagona* na *Mzingile*.

## 2.3 DHANA YA UHAI NA KIFO

Kifo ni suala ambalo limeenea mahali pote, ni tukio la asili, linaendelea kuwepo, haliepukiki, haliwezi kutorokwa na haliwezi kukataliwa. Uoga wa kifo husababisha wasiwasi. John Mbiti anasema maneno mengi hutumika nchi za Afrika wakati wa kurejelea tukio la kifo. Waafrika wanarejelea kifo kama, kurudi nyumbani, kuondoka, kuitwa, kuwa mali ya Mungu na mengine mengi. Maneno haya yote yanaonyesha kuwa tukio la kifo sio ukamilifu wa kuangamiza mwanadamu. Maisha huendelea hata baada ya kaburi kwa hivyo binadamu hushirikisha huzuni na imani kuwa kifo sio mwisho wa maisha na aliyeenda huendelea kuishi baadaye. Mbiti anaeleza kuwa mwanadamu huathirika wakati kifo kinapotokea katika familia au jamii zao. Kifo husawiri utengano wa mtu na wanadamu wengine na huonyesha mabadiliko yaliyo wazi kwa hivyo kuna uangalifu mwingi katika matambiko na sherehe za mazishi. Utamaduni wa Kiafrika unahitaji uangalifu sana wakati wa matambiko ya mazishi ili kuondoa makosa yasiyostahili kwa aliyeaga. Kisaikolojia mazishi katika tamaduni za waafrika huonyesha heshima na taadhima. Kwa hivyo mazishi ya Waafrika huwakilisha juhudi za kudhibitisha nafsi na kupata utambuzi hata kama ni baada ya mwanadamu kufa.

Kenyatta University
Kiswahili Resource Centre

Uelewa na uzoefu wa jamii za Kiafrika umeelezwa kupitia kanuni zifuatazo. Kanuni ya uwili mmoja ambayo hutumika kama kiini cha wazo. Tukiwa na uwili mmoja, kingamo ni kinyume. Ni kama mfano wa mchana na usiku, wafu na wanaoishi na jinsi wanavyotazamwa wakiwa na umoja. Hii ina maana kuwa hata kama kifo huonyesha nafsi imetoka kwa mwili, bado kifo kina uhusiano na uhai na sio kinyume cha uhai. Kifo ni mtazamo mwingine wa uhai.

Msimamo wa pili una uhusiano na ule wa kwanza. Dhana hii inasema nafsi na mwili haziwezi kutenganishwa. Katika utamaduni wa Kiafrika dunia ya mwili huonekana kuwa ufunuo wa ulimwengu wa kiroho. Kwa hivyo uhai na kifo, roho na mwili sio mgao wa sehemu mbili.

Kulingana na Mbiti, katika utamaduni wa Kiafrika wanajamii walioaga dunia hubaki kama kumbukumbu za wanajamii kama wafu wanaoishi. Kwa mujibu wa Mbiti, mwanadamu anakuwa na ufahamu wa uhai wake na majukumu yake yeye mwenyewe na wengine kupitia uhusiano wake na watu wengine. Kulingana na fasili hii, jambo linalofanyika kwa mtu binafsi linafanyika kwa kikundi chote na chochote kinachofanyika kwa kikundi chote hufanyika kwa mtu binafsi. Mbiti anasema "Niko kwa sababu tuko, na kwa sababu tuko, kwa hivyo niko." Imani ya msingi kutoka tamaduni za Kiafrika ni kuwa kifo ni uhai unaoendelea.

Waafrika huamini kuwa kifo cha mwili sio mwisho wa uhai lakini sherehe rasmi ya uhai katika umbo lingine. Umbo la maisha katika nchi ya wafu lina uhusiano na umbo la maisha ya hapa duniani. Uhusiano huu ni wa kuvutia hivi kwamba uhusika wa maisha haya kama ya "dunia" ni mazungumzo ya chanzo cha uhai yasiyofaa.

Afrika ya kimagharibi ina maelezo dhahiri kuwa mabadiliko kutoka maisha haya hadi hayo mengine ni safari ya nchi kavu na kwa hakika tukisafiri kutoka sehemu moja ya dunia kwa kutumia nchi kavu tutafika tu katika sehemu nyingine ya dunia.

Katika tamaduni za Kiafrika mipaka huwekwa kwa kutumia mito. Sio jambo la kushangaza kwamba kilele cha safari hii ni kule kuvuka mto. Mara baada ya kuvuka mto *mwanadamu* anaingia nchi ya walioaga na kujiunga na jamii ya wahenga, jamii ambayo hurudufu siasa za jamii iliyokuwepo hapo awali hivi kwamba viongozi wa dunia halisi wanaendelea kuwa viongozi katika jamii hiyo nyingine.

Wahenga huangalia shughuli za wanajamii wa familia zao huku wakisaidia wanaohitaji kusaidiwa na kuadhibu wenye hatia. Jukumu la wahenga ni kuonea wanaoishi mazuri. Wanaoishi wanatakiwa kuwafanyia wahenga kazi na mambo mazuri kama inavyostahili. Wahenga hawahitaji uangalifu mkubwa, jambo linalohitajika ni kuwapa chakula usiku kucha katika sehemu zinazofaa mara kwa mara. Kupitia matambiko, wanaoishi wanaonyesha uhakika wa heshima zao kwa wahenga na kuomba usaidizi kwao kuhusu mambo tofauti tofauti. Kupitia njia hii kuna udumishaji wa uhusiano unaoendelea na walioaga. Wahenga lazima wawe na akili kwa sababu wanafanya kazi ya *kuangalia* matendo ya jamaa zao na kuwapa baraka wakati unapostahili. Kutokana na haya yote ni dhahiri kuwa nchi ya wafu kijiografia sio tofauti na yetu na pia idadi ya watu ni kama yetu.

Mwanadamu ni "*kiumbe imara cha kifo*",Martin Heidegger alisema (Dubois 1965). Kifo hiki kiwe ni cha mtoto au mtu mzima ni cha kila mtu na huja wakati wake. Kifo cha kila mtu kimegubikwa na fumbo na hakiwezi kuepukika. Kwa sababu ya imani hii kifo ni hakika kwa mwanadamu anayeishi ingawa tunajaribu sana kukiepuka. Licha

ya kuwapo mahali pote ni jambo linalofahamika kwa njia mbalimbali kutegemea utamaduni, itikadi na desturi.

Hata kama kifo hakiepukiki, Waafrika hukikataa na wakati huohuo hukikubali kifo katika maisha yao ya kila siku. Mtazamo huu wa uwili unaweza kupatikana katika seti ya imani za wahenga. Waafrika wengi wanaamini roho ya mfu inabaki duniani na kwamba aliyekufa anaweza kurudi tena kama amevalia mwili wa mtu mwingine.

Suala la kifo ni mwiko katika jamii nyingi. Hali hii inatokana na ugumu wa kukubali na kuvumilia kifo cha mpendwa. Wakati binadamu anaporejelea kifo kama 'kuondoka' 'kwenda mbele' ama kwenda mahali pazuri wanaficha ukweli wa kifo kupitia lugha yenye maneno ya staha. Watu wengi wanaishi kwa kuamini kuwa tusipoongea kuhusu kifo, kitapita tu bila uchungu unaohusishwa na kifo. Jinsi watu wanavyoomboleza na kuhuzunika hutegemea mambo kadhaa katika maisha yao yakiwa ni pamoja na jinsia, imani kuhusu kifo na mitazamo ya kumpoteza mmoja wao. Kifo kinapotokea, wanadamu wenye msimamo wa kutarajia mazuri huoboleza na kusikitika lakini kwa njia tofauti na wanadamu wasiotarajia mazuri.

Waafrika waliamini kila jambo lilifanyika likiwa na sababu na sio kutokana na jingine. Pia waliiona familia kama kitu kimoja kilichoishi wanaoishi, eneo la uyakinifu na vitu visivyoonekana lakini halisi, dunia ya kiroho. Jamii ilivuka mipaka ya kifo. Kwa binadamu kifo ni hatua moja katika hatua kadhaa zinazoanza wakati wa kuzaliwa. Wanajamii wa familia moja waliokufa wana mvuto usiokoma na wana nguvu za kuathiri maisha ya wanajamii wanaoishi. Haja ya wahenga ilikuwa utamaduni ufuatwe na udumishwe. Kama wamekasirika na hawajatosheka wahenga waliachilia mambo mabaya kufanyika kama vile magonjwa. Kuwaweka wahenga

katika hali ya furaha kulihitaji kufuata tamaduni na sherehe kikamilifu. Pia wahenga walitambuliwa kila wakati katika mambo na sherehe zenye umuhimu sana kama wakati wa kuzaliwa, kupashwa tohara hadi utu uzima. Utoaji kafara kwa wahenga ulisaidia watoto kuishi au kuwasaidia kukumbana mambo magumu maishani.

Sisi sote lazima tukumbane na mambo mawili makuu; kwanza tuwe na utambuzi kuwa maisha ni yenye mipaka. Hatutaendelea na umbo letu la sasa milele. Pili, hakuna njia za kuipa dunia maana; ni dunia isiyokuwa na maana. Ni lazima tuyape maisha yetu maana.

Katika jamii ya watu kutoka jamii ya Juda kifo sio tanzia hata kikitokea mapema maishani au kupitia mambo yasiyopendeza. Kifo kama maisha yetu kina maana na kimetokana na mpango wa Mungu. Pia wale wanaoishi maisha mazuri hapa duniani watalipwa. Njia za kuomboleza katika jamii hii ni za kina lakini sio za kuleta uoga au kudharau kifo. Kuomboleza huwa kuna sababu mbili; kuwaheshimu waliokufa na kuwaliwaza walioachwa na wapendwa wao.

Mambo haya hutimizwa kupitia matambiko ya pekee yanayofanywa kwa undani na pia kupitia njia zingine za mawasiliano na walioaga. Jamaa wa mfu huamini kuwa hata kama roho ya mmoja wao imeenda juu mbinguni au karibu na Mungu, inabaki pia karibu na wao na inaweza kukaribiwa kupitia kwa maombi na matambiko mbalimbali. Ni kutokana na imani hii John Mbiti anasema "*kwa Waafrika kifo ni utengano lakini sio maangamizo*". Aliyekufa hutengana na jamii ya mwanadamu na bado madaraka ya pamoja bado yanamng'ang'ania.

Jamii mbalimbali hukataa kutafakari chochote kuhusu kifo. Mwelekeo huu wa kukataa kifo huchunguzwa kupitia maswali ya jinsi Waafrika husawiri kifo. Neno mabadiliko au mageuzi hutumiwa kurejelea waliokufa. Ni jambo lisilo la kawaida kuwasikia watu wakisema fulani amekufa. Kusema mtu amegeuka katika muktadha wa Kiafrika humaanisha mtu ameenda katika ulimwengu unaofuata. Neno mabadiliko huonyesha huyo aliyekufa hajatuacha, amebadilisha tu umbo lake hadi maisha ya kiroho. Pia neno "kupita" hutumiwa kuonyesha mageuzi.

Waafrika walipendelea kifo cha polepole kilichotokana na ugonjwa wa muda mrefu. Jambo hili lilimfanya mfu awe na amani, aseme kwaheri kwa marafiki na jamaa huku akitoa maagizo kwa watu wa nyumba yake. Hata kama kifo hakiepukiki, Waafrika wote hukataa na pia hukubali kifo katika maisha yao ya kila siku. Mtazamo huu unaweza kuonekana kupitia seti ya imani inayojulikana kama "ibada ya wahenga" ama imani kuwa roho ya marehemu huingia katika mwili wa mtu mwingine na anaweza kurudi akiwa na mawazo ya mtu huyo.

WaIgbo husawiri kifo kama wizani asilia ya maisha. Kuna hadithi inayoeleza chanzo cha kifo inayosema, wakati mmoja hakukuwa na kifo.Watu walifurahishwa na wazo la kuishi milele na waliomba miungu ili waendelee kuishi. Hatima ya kifo iliachiwa mbio za masafa marefu kati ya chura na mbwa. Kama Chura angeshinda, kifo kingeingia duniani na kama mbwa angeshinda mwanadamu angeishi milele.Watu walifurahia jambo hili wakiwa na imani kuwa mbwa angeshinda mbio hizo. Wakati mbio zilianza chura aliendelea kwa mwendo wa polepole bila kusimama. Mbwa alitimka mbio lakini kila wakati alisimama kula takataka. Mwendo wa Chura wa

polepole lakini wa uthabiti ulishinda. Mbwa alishindwa mbio hizo na huo ukawa ndio mwanzo wa kifo

Katika nyumba ya watawa ya Carmelite Waterford, Ireland kuna fikra zinazoonyesha wazi mtazamo huu wa Waafrika kuhusu mabadiliko baada ya kifo. Zinasema,

> *Kifo sio kitu chochote kile. nimeteleza katika chumba kingine. Vile tulivyokuwa bado tupo. Niite kwa jina langu ninalolielewa. Ongea nami jinsi ulivyokuwa ukiongea nami. Cheka tulivyokuwa tukicheka pamoja kutokana na mizaha tuliyopenda, cheza, tabasamu, nifikirie niombee* (mwandishi hajulikani).

Maisha baada ya kifo humaanisha yote yaliyokuwepo hata kabla ya kifo hubaki na ni yaleyale, yana mfululizo usiovunjika. "*Mwanadamu ni "kiumbe imara cha kifo*" Martin Heidegger alisema. Kifo hiki kinatatanisha, ni fumbo na ni kweli ambayo imepita utambuzi wa mwanadamu. Kwa sababu ya imani hii ya Waafrika, wao huhuzunika kwa miongo mingi kwa sababu ya wapendwa wao walioaga. Imani ya Waafrika kuwa wahenga kwa kweli hawajafa imeenea kote duniani na ili kuweka roho zao karibu na kuziheshimu, stuli walizokalia wakiwa hai huwekwa katika madhabahu ya wahenga.

Kwa hivyo, hata kama ni wakati wa mafadhaiko mmoja wao anapoaga, jamii nyingi hupata faraja kutokana na imani kuwa hata kama wapendwa wao kimwili hawapo, kiroho wapo. Kuna maliwazo ya uhai wa baadaye na uhai huu una uhusiano na maisha ya sasa. Utamaduni wa Kiafrika una uwezo wa kushikilia utakatifu wa uhai na

uoga wa kifo kwa sababu kifo ni adui wa uhai. Uoga wa kifo huongoza watu kutoka jamii mbalimbali kutumia hirizi na juju ili kujikinga kwa sababu hata kama kifo hakionekani kinaweza kuepukwa.

Mtazamo kutoka Irish ni mkongwe, ni wa kila mahali na umenata maisha ya jamii nyingi za Kiafrika. Mila na desturi za Mwafrika zinaonyesha kwamba, mwanadamu anazaliwa, anakufa na anaendelea kuishi katika ufalme mwingine. Mviringo huu wa kuzaliwa, kufa na kuendelea kuishi mara nyingi hutumiwa kiishara katika sanaa ya Kiafrika na kama picha ya maelezo ya sura ya dunia. Aliyekufa hayuko katika mbingu ya mbali lakini anabaki kuwa na wanaoishi

## 2.4 HITIMISHO

Sura hii imeshughulikia historia ya mwandishi, wasomi waliomwathiri, tajiriba yake , mawazo yake, ufasili wa uhai na kifo katika jamii mbalimbali na dhana ya uhai na kifo. Mambo haya yamewekea utafiti wetu msingi imara. Aidha, tumebainisha jinsi vipengele hivi vimechangia katika matumizi ya uhai na kifo kimafumbo. Pia, tumeonyesha namna mazingira ya mwandishi yamechangia pakubwa katika matumizi ya dhana ya uhai na kifo.

Sura hii imejadili fumbo la uhai na kifo katika riwaya ya *Nagona*. Aina ya mafumbo yanayopatikana katika riwaya hii yamefafanuliwa huku tukihakiki jinsi mazingira ya mwandishi yanavyomwathiri. Aidha, tumedhihirisha jinsi fumbo la uhai na kifo limeathiri msuko na maudhui ya mtunzi. Hatimaye, katika sura hii tumehakiki jinsi fumbo la uhai na kifo limekwamiza usawiri wa wahusika wa mtunzi.

# SURA YA TATU

## MAUDHUI YA UHAI NA KIFO KATIKA RIWAYA YA *NAGONA*

### 3.0 UTANGULIZI

Sura hii ya tatu imedhihirisha jinsi dhana ya uhai na kifo imesawiriwa katika riwaya ya *Nagona.* Hadithi katika riwaya hii imetokana na fasihi simulizi ya Ukerewe ambapo Kezilahabi amezaliwa. Ni sehemu ya kwanza ya riwaya tatu za mfululizo za Kezilahabi lakini kufikia sasa ni sehemu mbili pekee zimechapishwa, ya pili ikiwa ni *Mzingile*. Riwaya hii ina sitiari ya safari ambayo ina uhusiano wa karibu na tukio la kweli. Ni masimulizi yanayohusu kukabiliana na jambo na kumsifu anayeweza kukabiliana nalo mpaka akalitatua. Staili ya mwandishi ni hasahasa na masimulizi yake yanazungumzia matukio ya watu wengi katika historia. Riwaya hii ilichapishwa nakala chache kwanza mwaka wa 1987 na ikatolewa tena mwaka wa 1990.

Sura hii imebainisha kwamba maisha sio mstari mrefu ambao una kikomo bali maisha ni duara na yanaendelea hata baada ya kufa. Katika maisha halisi, kitu duara hakina mwanzo wala mwisho hivyo, riwaya ya *Nagona* imesawiri maisha katika nyakati na hali zote, maisha halisi na maisha ya utohalisi. Isitoshe, riwaya ya *Nagona* imeonyesha kuwa mwanadamu hafi lakini anaendelea kuishi katika maumbile mengine hata baada ya kufa na kuzikwa. Baada ya kufa kuna uhai na mahitaji ya utashi pekee. Khamis (2003) katika kueleza riwaya mpya ya Kiswahili anaieleza riwaya hii kwa kusema "*riwaya ya Nagona ni riwaya ya siku zijazo-riwaya inayokimbiza kanuni zilizowekwa na jamii*". Katika kulifafanua hili anaeleza kuwa *Nagona* ni riwaya iliyovuka usasa na kuingia katika usasabaadaye. Utafiti wetu

umedhihirisha jambo hili na pia umeonyesha kuwa mwanadamu huanza kufa tangu kuzaliwa kwake.

*Nagona* ni riwaya iliyojaa mbinu za kiutunzi za fasihi simulizi za Kiafrika kwa kuwa ina vijenzi vya ploti ambavyo ni visasili vya masimulizi ya ngano za majagina wa Kiafrika na yanawakilisha ulimwengu wote. Kezilahabi amesawiri maisha ya mwanadamu kutoka kuzaliwa kwake ulimwenguni, kufa na hata baada ya kifo. Kulingana na riwaya hii, kifo ni daraja anayopitia mwanadamu anapovuka ng'ambo ya pili na kuanza maisha mapya. Utafiti huu umedhihirisha kuwa"*Nagona*" inasawiri dhana ya ukweli kuhusu masuala muhimu kama uhai na kifo katika maisha ya wanadamu wote ulimwenguni.

Riwaya ya *Nagona* inaanzia gizani na kuishia gizani. Hii ni kwa sababu mara kwa mara mwandishi anaanza sentensi kwa "*sijui nilikuwa wapi na nilikuwa si-, nilkuwa si-*" yaani kuna ule utusitusi. Si giza kwa macho tu, ni giza pia kwa zile dhana zilizomo mle ndani (Khamis 2001). Lile giza limo, kote liko giza na hakuna uwazi katika riwaya hii. Hakuna mwanga kwenye *Nagona*, ni giza kutoka mwanzo hadi mwisho. Katika riwaya hii mwandishi anaonyesha maisha ni utusitusi na sio dhahiri. Pia, hakuna mfululizo wa matukio katika hadithi yenyewe. Masimulizi ni kupitia ploti zisizounganishwa na vijisehemu vya hadithi vimeunganishwa kwa njia tatanishi. Riwaya ya *Nagona* kwa hivyo ni mkusanyiko wa vijihadithi ambavyo havina mshikamano. Ina motifu ya safari na dhana ambazo ni za kifalsafa, sosholojia, saikolojia, historia na dini. Uzi unaounganisha sehemu za hadithi na matukio ya hapa na pale katika kipindi chote cha safari ya utambuzi wa wahusika wakuu unakatikakatika. Safari inaendelea na kupindapinda huku ikileta pamoja matukio

yaliyotapakaa na kuelea kote. Safari yenyewe ina wahusika wasiotambulika kwa uwazi. Kwa hakika Kezilahabi ameathirwa na masomo yake ya falsafa kutoka Ugiriki wa kale na saikolojia.

Sifa ya kwanza ya riwaya ya *Nagona* ni kule kugawika vijisehemu kwa utaratibu wa usimulizi ambao unaendeshwa kwa sauti ya msimulizi. Sauti inahusishwa na kujirejelea kwa nafsi kupitia ubunifu ulio huru kupitia ndoto zinazotoa changamoto kwa uhalisia wa dunia ya kila siku. Mchezo huu wa lugha unaonyesha matukio yaliyopita nguvu za uwezo wa kufikiri kirazini na shida ya uhusiano wa nafsi iliyovunjwavunjwa na jamii. Kezilahabi katika riwaya hii anaacha kuwa kielelezo cha uhalisia na inatalii nyanja zingine kabisa.

*Nagona* ni riwaya inayoashiria safari ambayo ni ngumu na ndefu. Pia anayesafiri hupitia nchi kavu na ya kusikitisha, isiyokuwa na watu na tunapata uzoefu wake wa ukweli. Anakutana na wanafalsa wanaojulikana wakiwemo Marx, Nietzsche na Freud wameketi katika duara wakiongea na nafsi zao ambazo wamezitapika mikononi mwao. Nguli anaanza kumfuata paa wa ajabu na ili aweze kumshika ana majukumu matatu magumu ya kutimiza. Anaweza kuyatatua kwa usaidizi wa wazee wanne ambao wana nguvu za kiajabu lakini hatimaye anakosa kumshika. Hatimaye, yule paa anatokea kuwa mwanamke mrembo. Pia, nafsi inatubu dhambi za karne mbili zilizopita ambazo zinahusishwa na mwanadamu. Hatimaye kuna "Ngoma kuu" ambayo imengojewa kwa muda mrefu. Wakati wa ngoma hii nguli anacheza densi katika kikundi cha vichaa. Msichana kwa jina *Nagona* anazaliwa mwishoni mwa riwaya hii na nguli anamfuata. Katika sura hii tutaangalia hadithi zilizomo katika

hadithi kuu ya *Nagona.* Aidha, tutaonyesha jinsi matukio ya uhai na kifo yamesawiriwa katika riwaya ya *Nagona.*

## 3.1 UHAKIKI WA RIWAYA YA *NAGONA*

### 3.1.1 HADITHI YA "MIMI"

Hadithi ya "Mimi" ndiyo kiini cha riwaya ya *Nagona* na hatimaye inaunganishwa na hadithi za wahusika wengine. Mfululizo wa hadithi hii, matukio na hata maafikiano yanatoka kwenye mandhari ya Afrika na hatimaye kuwa ya ulimwengu wote. Mhusika mkuu "Mimi" yuko safarini kutoka sehemu isiyojulikana hadi sehemu inayotatanisha ili kutimiza misioni ya kutafuta paa wa ajabu. Safari hii hatimaye inampeleka hadi kwa mkombozi wa pili ambaye ataokoa dunia kutoka kwa maangamizo na maanguko.

Hadithi inaanzia gizani, msomaji hajui ni wakati upi unaorejelewa kwani msimulizi anaanza kwa kusema "*yaelekea ilikuwa jioni*" (uk 1). "Mimi" anaona na kusikia mrindimo wa mto na anatembea kuelekea usawa wa mto huo ulikotoka na hajui ama huo unakuwa mwanzo wa safari yake. Amechoka na kichomi kimeanza kumuuma ubavuni. Anatembea kwa magoti kuelekea asipokujua. Anastukia anapigwa viboko matakoni na mgongoni na hatimaye anaishiwa na nguvu, fahamu na mwili wake unakufa ganzi. Anapozinduka anaona msitu mkubwa nyuma yake ingawa umefunikwa na ukungu. Anasimama karibu na mto na anapata matumaini anapoona makazi yanayofanana na mji mdogo. Mji huu ni kimya na una barabara moja kuu iliyo wazi na haina lami lakini una kumbikumbi walioanguka usiku na ndege wachache. Hakuna kiumbe hata kimoja kinachoweza kuonekana. Nyumba ni mbovu na hali ya ukame inaonekana kusambaa kwa muda mrefu. Upepo umesukuma nyuma

vituta vya mchanga na hakuna unyayo wowote unaoonekana. Anapoangalia nyuma, "Mimi" anaona tu nyayo zake.

Upepo mwororo unavuma na kutoa alama za machweo. Kiumbe cha kwanza kukutana nacho ni paka mweusi, ambaye amekaa upenuni mwa nyumba. Anamtazama "Mimi" na kutoa mlio pekee unaomkaribisha katika mji huu. Anajinyonganyonga mkia wake kama kwamba alimtegemea na kumtarajia lakini mara anapomwelekea anaingia kwa nyumba kupitia kwa dirisha na dirisha inafungika na kama milango ya nyumba zingine, mlango umefungwa. "Mimi" anajaribu kuchungulia kupitia nyufa za mlango, anasikia mtu akikohoa aina ya ukohoaji aliyokuwa amesikia kule msituni lakini anapogeuka haoni mtu. Anaogopa lakini anajipa ujasiri.

Mlango ulio mbele yake unafunguka polepole hadi unafika mwisho lakini haoni anayeufungua. Anapoingia ndani mlango unajifunga wenyewe. Nyumba yote imejaa vitabu vilivyoenea vumbi na vile vya chini vimeanza kuliwa na mchwa. Msimulizi anavutiwa na mlio wa paka kutoka pembe moja ya nyumba. Anaelekea huko na kusikia ukohoaji unaomwonyesha nyendo zake zinatazamwa. Paka mlinzi wa kifo, amekaa juu ya kiwiliwili cha binadamu aliyekuwa amepakwa mafuta ili asioze. Katika mkono mmoja binadamu huyu amepakatishwa Biblia Takatifu na mwingine Koran Tukufu. Mdomo wake umefungwa kwa kitambaa cheupe ambacho kina maandishi "*kimya ni hekima.*" (uk 4).

Paka analia tena huku akitazama mlangoni. Polepole mlango unafunguka. "Mimi" anasikia kama nyayo za mtu anayeingia lakini anapoongea anajibiwa na mchwa. Anastukia anapigwa kofi na kusukumwa kwa nguvu. Anaanguka, mlango

unajifunga,dirisha lilelile linajifunga na anasikia mtu akikohoa. Giza la jioni limeanza kuingia na msimulizi anaendelea kuifuata barabara hiyo kuu. Anasikia vicheko kutoka baadhi ya nyumba. Mbele yake anaona jogoo aliyekuwa akielekea alikokuwa anakwenda . Anajaribu kumkaribia lakini hawezi, anastukia yai viza linapasuka kifuani na vicheko kutoka baadhi ya nyumba.

"Mimi" anarudi katika barabara kuu na kwa mara ya kwanza anaona viumbe hai mbele yake, watoto watatu wanaelekea alikokuwa anakwenda. Kadri anavyokaza mwendo awakaribie ndivyo wanazidi kutembea kwa haraka. Wanaingia ndani ya nyumba moja iliyokuwa mbele. Msimulizi anajipa ujasiri na kugonga mlango huo. Mlango unafunguka polepole na mbele yake anasimama mama amevaa nguo nyeupe, ushungi mweupe na kitambaa cheupe kinachofunika mdomo wake. Anajaribu kusema naye lakini mama anatumia ishara ya mkono na kidole kumwonyesha nyumba iliyo upande mwingine wa barabara. Mlango wa nyumba hii ni wazi na msimulizi anaweza kuona mwanga hafifu ndani.

Anapopiga hodi, anajibiwa kwa mara ya kwanza na sauti ya binadamu. Anakaribishwa kwa kinywaji cha mvinyo na Padri wa mji huu. Msimulizi anapotaka kujua sababu ya mji huu kutokuwa na watu, Padri anamwarifu kuwa watu ni wengi na amekuwa akipishana nao barabarani. Padri anamfafanulia mambo yote aliyopitia. Anaelezwa kuwa yule mama aliyemwonyesha nyumba hii ana mimba ya mkombozi wa pili lakini hakuna anayejua aliyempa mimba. Pia, anaelezwa wale watoto watatu ni kizazi kipya ambacho hakina hatia, ni yatima. Padri pia alikuwa akimtegemea msimulizi na anamwambia kuwa kama haingekuwa ajali iliyotokea katika bonde la

taaluma hangekuwa amefika mapema kwani ametumia karne moja badala ya karne nne kufika.

Msimulizi anapotaka kujua kwa nini yule mama hasemi anaarifiwa kuwa watu wa mji huu hawasemi. Anayezungumza katika mji huu ni Padri na mzee mmoja karibu na mto na wote wawili ni wendawazimu. Wanakimbiwa kwa sababu hawajui kuzungumza kwani lugha wanayoijua watu wa mji huu ni kimya na wanaielewa vizuri. Padri anamwarifu kuwa ule msitu ulikuwa maktaba ya taifa na vitabu vilitupwa huko. Kuna mizungu pale na waandishi wanalilia kusomwa ili wasife. Yule maiti alikuwa amekataa kutupa vitabu vyake na alikuwa ameuawa na wanamji, naye paka ni mlinzi wa kifo.

Kazi ya Padri ilikuwa kumgoja msimulizi na kulinda mshumaa kwa sababu siku ya ungamo kuu ilikuwa imekaribia. Watu katika mji huu hawali, wanaishi na kula matumaini ambayo huzaliana. siku hadi siku. Hayo matumaini wanayatoa katika kisima cha ndoto ambacho hakikauki. Jogoo ndiye mlinzi wa kisima na anahakikisha matumaini ya watu wa mji huu hayaoti mbawa na kuruka na anawika wakati ndoto zianzapo kuwa tanzia. Msimulizi anapotaka kujua ama hao watu wamekufa au wazima Padri anamjibu '*kama kufa ni kutokuwako basi wazima*'( uk 10). Watu katika mji huu wanapendelea kucheka kwa sababu ndio njia pekee ya kukishinda kifo na kukohoa ndio njia ya kujihakikishia uhai na kuwako.

Wote wawili wanasikia vicheko na wanatoka nje kwa sababu jambo hili hutokea mara moja kwa mwezi. Nje wanasikia fisi wakicheka na nyani wakilialia, vilisikika

Kenyatta University
Kiswahili Resource Centre

vicheko vya kila aina. Upande wa mashariki panaonekana mwezi mpevu mwekundu. Hii ni siku ya matumaini ya mwezi unaofuata.

Kesho yake asubuhi anaelekezwa kwa yule mzee anayeishi karibu na mto. "Mimi" anampata amekaa ukingoni mwa mto akiyatazama maji kwa makini. Mto huu umejaa damu tupu inayotiririka kwa nguvu na ongezeko la damu linaadhirisa kufika kwa msimulizi. Mzee alikuwa akitafuta miswada yake majini iliyotupwa na watu na alipoikosa alikasirika. Ghafla alianza kucheka peke yake alipotoa mikono yake majini kwa sababu ya ongezeko la damu. "Mimi" anapokohoa mzee anamtazama ,anatabasamu na anamwambia kwamba alikuwa anamtarajia.

Mzee anaandika mswada mwingine lakini kwa wakati huu anauandika kichwani mwake na ameuhifadhi vizuri kimaandishi. Anamwambia "Mimi" kwamba siku ya ungamo kuu imekaribia kwa sababu amefika na kwa hivyo atakamilisha kuuandika. Anaendelea kumwambia kuwa yeye na Padri ni vichaa ingawa kichaa cha Padri kimezidi kwa sababu anakunywa mvinyo usiku na mchana. Anasema yeye huimba tu nyimbo anazozikumbuka kwa sababu walivichoma vitabu vyote vya nyimbo na walisema hakuna nyimbo nzuri kuliko sauti za ndege na kusikiliza ndio njia pekee ya kuzungumza na upweke wa binadamu na nafsi yake. "Mimi" anaporudi kwa Padri jioni, anamkuta akinywa mvinyo. Padri anamwambia anafikiri kichaa cha mzee kimeshinda chake kwani yeye anaweza kuimba usiku mzima na nyimbo ni za zamani mno. Anaendelea kumwambia kuwa wao hukutana siku ya Jumapili mzee anapokuja kutumikia misa na kuchukua shehena ya chakula.

Padri anamwarifu "Mimi" kuwa alitakiwa kuja hapa ili siku ya ungamo kuu asikosee njia. Anaambiwa njia aliyokuja nayo haitamfikisha popote, atakwenda na kurudi hapo hapo na hiyo ndiyo itakuwa siku ya ungamo kuu.. Usiku huo wanakunywa na anasimuliwa habari za jengo lililozungushiwa ukuta wa mawe na mikuki iwakayo. Kesho yake "Mimi" anaondoka lakini hafiki mbali kabla ya kupotea njia.

### 3.1.2 HADITHI YA BABU

"Babu" ni babu yake "Mimi" na ana kipaji cha kuhifadhi utamaduni wa Kiafrika. Babu anamwambia "Mimi" kuwa ataona ishara itakayomwongoza kwenda huko kwani njia inajulikana kwa wote na inakwenda moja kwa moja bila kupinda. "Mimi" anaambiwa hana haja ya kutafuta wataalamu kwani atakuta amefika. Babu anamwambia atakapofika atamkuta amekaa peke yake akiwatazama wale wengine. Anaendelea kumwambia atawatambua hao wengine maana ni ndugu zake na wengi kati yao walikuwa askari wa mwanga na wale hataweza kutambua atajulishwa kwao na yeye atachukua nafasi yake. Anaonywa asistuke kwa sababu ya majina yao makubwa na afanye wafanyavyo.

Babu anajulikana sana kijijini na wazee wengi wanafika mara nyingi kuongea naye.Wanafika kwa sababu ya kutafuta mawaidha, kusikiliza hekima yake na masimulizi ya historia ya wakati uliopita. Mara nyingi Mimi anakaa karibu naye kusikiliza maongezi yake na wazee. Babu anamwambia "Mimi" asikilize vizuri kwa sababu anataka awe shahidi wa kweli. Anamwambia, ishara itakapotokea aifuate hadi kwenye kitovu cha duara. Anawaambia wazee wamtengenezee "Mimi" uta na mishale ili aweze kumsaka paa aliyepotea karne nyingi zilizopita. Anawaambia

wasimpe mkononi, kwanza wasubiri ishara. Kwa sasa paa anajificha mahali palipo wazi na ni mwana wa Mungu na mkombozi. Mkombozi atamwonyesha "Mimi" nyayo tu za paa kwa sababu hata yeye hajawahi kumshika. Anamwambia "Mimi" ajitakase ili aweze kuingia kwenye ngoma.

"Mimi" anangoja miaka kumi , miaka ishirini bila kuona ishara na haukuwa muda mfupi. Kila wakati mazungumzo ya Babu yalikuwa ya aina hii na wakati wazee walisema hawaelewi aliwajibu, *"Kama mimi ningeelewa ningekaa kimya. Tunazungumza kwa sababu hatuelewi"* (uk 16).

Padri ambaye ni paroko anachukia mazungumzo ya Babu sana kwa sababu yanapingana na yake. Anafika nyumbani kwa Babu siku moja na kumkuta katikati ya mazungumzo na wazee. Anapoketi anawauliza kama kuna mkristo kati yao na anaambiwa hakuna. Padri anawaita wote mapagani kwa sababu wanacheza ngoma ya twiga nje ya duara na twiga hawezi kuhimili ngoma yenye vurumai, vurugu na ghasia katika gharika la hisia na fikra. Padri anayafuata mazungumzo ya Babu na anaanza kujiona mwanafunzi. Anaondoka jioni kabisa baada ya kusahau lililomleta na kusikiliza mazungumzo ya Babu pamoja na wazee.

"Mimi" anataka kujua juu ya kuzaliwa kwake kwani wazazi wake hawajawahi kumweleza kikamilifu. Babu anamwambia kuwa alifika wakati ajali lazima ingetokea katika bonde la hisia.

### 3.1.3 SAFARI YA "MIMI"

"Mimi" haelewi ni wakati gani. Anajikuta anatembea peke yake kwenye bustani. Maua na matunda kwenye bustani hii yalitoa mwanga na hakuna yaliyoweza kuchumika, yaliteleza kiajabuajabu. Mara anajikuta kwenye jangwa. Hana hakika ama yumo jangwani au anaelea juu ya mawingu yenye rangi isiyojulikana. Kwa mbali anaona watu wakionyesha bunduki hali wakiwa uchi. Anasikia shoka linashuka shingoni mwake na kelele za "*ushindi!*"

Ghafla anaona kizee chenye mkongojo kikimjia kwa fimbo. Mawingu na ukungu vinayeyuka na chenyewe kinatoweka. Anaona watu kama wanane hivi karibu naye ambao wamekaa katika duara na wamefungwa vitambaa vyeupe kwenye nyuso zao. Baadhi ya watu hawa wanatazama nje ya duara, na baadhi wanatazama katikati ya duara ambapo anaona mwanga umechomoka toka chini hadi juu. Hawa watu ni askari wa mwanga. Katikati ya mwanga huu "Mimi" anaona kitu kama kiwiliwili cha binadamu. Anatembea kuelekea mduara huu.

Hawa askari wa mwanga wametandaza viganja vyao kama vitabu huku wakivitazama kwa makini. Katikati ya viganja hivi kuna kitu king'aacho kama almasi. Sauti inayotoka katikati ya duara inamkaribisha "Mimi" kwenye duara. Sauti inamwambia wamekuwa wakimsubiri na imesikia sifa zake. Wanapokuwa wakiongea sauti inawajulisha kwamba wote wamo mawazoni mwake tu na watapata uhuru wakati atakapowashauri lakini anawakumbusha yeye sio msahaulifu. "Mimi" anaagizwa na sauti atapike roho yake. Anainama, anajiona kama mtu mwenye usingizi na anapofumbua macho anaona roho yake lakini ni chafu sana ikilinganishwa na roho za askari wa mwanga. Anaarifiwa kuwa roho huchukua maelfu ya miaka kuwa safi.

Wale askari wa mwanga ni Plato, Socrates, Aristotle, Hegel, Darwin, Marx, Freud na Nietzsche. Wamefungwa vitambaa machoni kwa sababu walikuwa karibu kukata tamaa. "Mimi" anaelezwa kuwa hiki ni kikundi kidogo tu cha wale waliowekea njia miba, ngazi za kupandia na madaraja yasiyoaminika na waligombana hasa na wataalamu wa Kiafrika. Hawakuweza kukaa katikati ya duara mwanga ulipotokea; kitovu kilipasuka, pakabakia shimo ambamo kizazi kilichofuata kilitumbukia. "Mimi" amefika katika kikundi hiki kwa makosa na anaagizwa azungumze na roho yake. Mimi anashangaa anapoambiwa tayari wametumia miaka kumi katika mazungumzo yake na Sauti na lazima ajifunze kuikubali roho yake. Anapoongea na roho yake, roho inamwambia kuwa ni chafu kwa sababu ya dhambi zake "Mimi" alizoungama kwa padre mlevi.

Sauti inaendelea kumwambia kwamba ilituma dhamiri, mtoto wao amkanye ili abadili vitendo vyake lakini hakusikia. Anaendelea kuambiwa yeye, sauti na dhamiri ni kitu kimoja. Kwa kuagizwa na sauti ya kiwiliwili, anapumzika pembeni na anaarifiwa kuwa mazungumzo na roho yake yamechukua miaka kumi na mitano na sio mwanzo mbaya. Anaagizwa ameze roho yake.

Sauti inawageukia askari wa mwanga na kuwaambia wakati wa kuosha roho zao kwenye maji ya uzima umefika na wanaruhusiwa kufungua nyuso zao. Wanaelekea kwenye mto bondeni lakini wanazipoteza roho zao kwenye ajali ya mkondo mkali wa maji. Sauti inawafukuza kwani hawamo tena mawazoni mwake. Wanakimbia kila mmoja upande wake wakipiga kelele wakisema wako huru.

### 3.1.4 MATATIZO YA ULIMWENGU

Hadithi hii inahusu nafsi "Mimi," msaka paa , silka na dhamiri, askari wa mwanga. Nafsi hizi zinakaribiana na zile ngazi za Freud kuhusu nafsi ya mwanadamu.Wote ni wataalamu wa uchumi ambao wametumwa na serikali zao kuchunguza kuporomoka kwa sekta ya viwanda katika ulimwengu wa tatu. Kazi hii ingewasadia kufikiri na kutatua matatizo ya uilimwengu.

Bondeni kwa mbali wanaweza kuona dalili za makazi na majani mabichi yanayotoa dalili za kuwako kwa maji na uhai. Wanakagua karakana zote za uvumbuzi na kutoa mawaidha kwa serikali. Nia ya serikali ni kuleta amani ya kudumu duniani . Dunia inaendelea kusakamwa na migogoro ya kiuchumi na nchi nyingi za ulimwengu wa tatu zinapata janga la njaa na mamilioni ya watu wanakufa .

Hawakumbuki jinsi walivyotoka hapa, wanakumbuka tu serikali ilikuwa imewapa ndege. Wanatembea kuelekea kisimani kuzima kiu. Wanachota maji kwa viganja vyao lakini kabla ya kuyafikisha kinywani, wanasikia sauti inayowaamuru kuacha. Wanaona kizee kifupi na kinaangalia kila kitendo wanachofanya kwa uangalifu. Kizee kinawaarifu kuwa maji hayo yanatoka kwenye viwanda na karakana, yana sumu kali na ndoto zote za maendeleo ya binadamu huishia humo.

Kizee kinawaambia kwamba walikuwa wakiwasubiri lakini wanashangaa kwa sababu wamechukua muda wa miaka kumi kufika. Wanaagizwa kufuate kizee hadi kwenye kilima na kuonyeshwa eneo kubwa kidogo. Wanaendelea kuelezwa kuwa mashujaa wote wamezikwa kwenye kilima hiki. Wanaonyeshwa kaburi la Yesu, Muhammed, Marx, na Socrates. Kaburi la Marx limekwakunguliwa na limeanza kufifia. Mbwa nao hukojolea makaburi haya kila siku. Wezi, majambazi, maskini,

vipofu, walawiti na vichaa wanafika hapa mara moja kwa mwaka kuyapalilia. Wanaendelea kufuata kizee na ghafla harufu mbaya ya vinyesi inawaingia puani. Kizee kinawaarifu kuwa hapa ni mahali palipozikwa wafalme wa Uingereza, Ureno, watawala wa Ufaransa na maraisi wa Marikani lakini vichaa kutoka ng'ambo nyingine huenda haja hapa.

Vichaa hawa wanasema wanaondoa hasira iliyokuwa imegandamizwa kwao kwa miaka mingi na nguvu za kiuchumi. Baadhi ya vichaa hawa ni wanasiasa na wanamapinduzi ambao ni wanasayansi wa ukombozi wa pili. Wanaendelea na safari na wanapouliza njia kizee kinawaambia kuwa kilikuwa kimeambiwa na dhamiri kije kiwapokee hivyo hawajapotea. Kizee kinaendelea kusema "*kuniamini mimi ni kuamini nafsi zenu*" (uk 35). Anawaarifu kuwa kitendawili cha maisha kilianza tangu wakati wa mfalme Oedipus na tangu siku hiyo uasherati umeingia duniani. Kizee kinaendelea kutembea kikizungumza peke yake. Kinawauliza au wao ni wazima ama wamekufa. Wanashangaa kuulizwa swali hilo na kadri wanavyozidi kufikiri ndivyo wanavyozidi kutokuwa na hakika. Kizee kinawaambia, "*hapa hapajawahi kukanyagwa na aliye hai*" (uk 36)

Mwandishi anaendelea kutuarifu kuwa kizee kilianza kufa tangu kizaliwe na wote wanamwita kifo. Naye binadamu ni kiumbe kilicho katika daraja la juu kabisa kuliko viumbe vyote na chenye uwezo mkubwa wa kufikiri na manju wa ngoma ya uhai ni kizee chenyewe. Kizee kinatuonyesha majengo mazuri lakini yote yamezungukwa na madimbwi ya maji machafu na majengo haya yanalindwa na askari wenye bunduki. Majengo haya yalikuwa kiwanda cha baiskeli bila breki. Wote wanataka kukichunguza lakini hawakubaliwi ndani. Baiskeli bila breki ni ajali na

katika bonde hili kuna imani kuwa ajali ni mwanzo tu wa kitu au wazo jipya. Wanatembelea viwanda saba na kati ya hivyo ni vitatu wanavyoruhusiwa kuingia. wanakatazwa kukikaribia kiwanda cha kutengenezea mabomu ya nyuklia.

Kwa mujibu wa nadharia ya uhalisiamazingaombwe, Kizee kinawaaga na kutoweka ghafla lakini wamefunzwa jambo moja, nalo ni kufikiri. Maisha yanakwenda haraka kwani wanajiona wazee wenye mvi. Wanaandika ripoti na kuikabidhi kwa serikali. Mwaka mmoja baada ya hii safari, ajali za mitambo za nyuklia zikaanza.

### 3.1.5 MWANAMKE NA PAA WA AJABU

Hii ni hadithi ya mwanamke mrembo aliye uchi ambaye anaoga karibu na mahali mto huchipuka. Jambo hili linampa "Mimi" mvuto na motisha wa kukamilisha misioni ya kutafuta maana ya uhai, kifo, na ukweli na hatimaye kukutana na mkombozi wa pili.

'Mimi" anajikuta katika msitu akitangatanga mbali anaona mwanamke akikoga na anamtazama. Anapomaliza anachukua mtungi wake lakini unamshinda kubeba, anaketi. Mimi anakata shauri kumsogelea. Ni mwanamke mzuri na anaeleka kuwa mja mzito na mimba ya mkombozi wa pili. Karibu na chemchemi ya maji ,"Mimi" anaona mishumaa miwili ikiwaka mmoja wa mwanamke na mwingine wake. Mwanamke huyu anamwarifu kuwa amekuwa akimsubiri. Mwanamke anapomwona anamkumbatia na kumwarifu kuwa mkombozi wa pili atazaliwa wakati wa machweo siku moja baada ya Ngoma Kuu lakini ataona ishara.

"Mimi" anaona nyayo zinazoelekea kuwa za mnyama na anaelezwa kuwa ni za paa aliyempurukusha msituni. Pia, anaona upinde na mishale miwili juu ya jiwe. Anaelezwa vyote hivyo viliandaliwa kwa ajili yake. Mwanamke anamwambia avichukue na afuate nyayo za paa, amshike mkonono ili amjue. Anapoondoka anaambiwa upinde na mishale ni ishara zake na asivitumie ovyo.

Anakimbia polepole na hatimaye anachoka na nyayo za paa zinapotea. Anatembea bila kuwa na hakika na anakokwenda. Anafika nchi tambarare iliyokuwa na maji mengi na kwa mbali anaona ng'ombe na kondoo, anakutana na wazee wawili ambao wamemsubiri kwa miaka elfu mbili. Mzee wa kwanza ni Nabii na wa pili Mtume. Mtume anampapasa toka nyweleni hadi kidevuni na anasema ni yeye "*Alama zote anazo! Upinde na mishale*"( uk 45). Wazee wote wanarukaruka kwa furaha wakipiga kelele hadi mbavu zinawauma. Pembeni kidogo anaona jiwe pana na bapa na juu yake anaona mchezo wa bao. Mchezo huu unasaidia kufikiri. Kufikiri ndiyo njia mojawapo ya kuitetea kweli. Kufikiri kunaihamisha milima na kuisukuma pembeni ili mwanga upite. "Mimi" anataka kuwafahamu na Nabii anasema, tangu nyoka kuingia ukumbini ujuzi umefichama na kweli imezungukwa na ukungu. Walimuua yeye badala ya kumuuua *Sphinx*.

Paa wa ajabu ana umbo na mwili wa mwanamke au ukweli wenye utelezi na analindwa na mfalme mwenye nguvu. Ili "Mimi" aweze kumpata, anapatiwa majukumu matatu ya kufanya lakini magumu ambayo ni, kuondoa mlima, kulima sehemu ya nchi iliyokauka sana na kuleta kiko cha mfalme alichoacha nchi ya Sabira iliyo mbali. Kwa usaidizi wa manabii na wafuasi wanaweza kumpata huyu Paa lakini kwa sababu ya utelezi wake hawawezi kumshika.

Wazee hawa waliacha kila kitu na kuandamana na "Mimi" na wanaongoza. Wanafika kwenye mlima mrefu ambao ulikuwa vigumu kuupita na nyayo za paa zinapotea. Karibu wapoteze matumaini lakini Mtume anajitokeza na kuhamisha mlima na wanaendelea na safari, nyayo za paa zinaonekana tena. Wanapofika jangwani wanaona kiu na nyasi inakuwa ndefu na inakuwa vigumu kufuata paa. Mbali kidogo wanaona mzee na kumsogelea na karibu naye palikuwa na kibuyu. Anatabasamu na kusema yote yametokea jinsi yalivyotabiriwa. "Mimi" anapomtazama anaona miguu yake hailingani. Mguu mmoja ulikuwa mfupi na mwingine mrefu sana na mwisho wake haukuonekana. Anaarifiwa kuwa mguu huu unaenda kwenye fikra na unapozama haurudi bila wazo. Wanaambiwa kuwa paa amepita juu ya mguu huo. Wanachukua kile kibuyu na kunywa maji kwa zamu. Mfuasi anaukunja mguu na wote wanafuata kinjia kinachoachwa na huu mguu. Wanapotoka nyikani wanaanza kuona nyayo za paa. Wanapoingia bonde linalokuwa na dalili za moto nyayo za paa zinaanza kufifia. Wanapofika mtoni nyayo za paa zinapotea kabisa.Wanashindwa kuvuka mkondo huu na wanakaa chini kufikiri. Wanamwona mzee mmoja amelala chini ya kivuli cha mti na anaposika nyayo zao anafumbua macho na kuwaarifu kuwa alikuwa ameona paa. Yeye ni Mtenzi mkausha maji. Anawaambia kuwa baada ya mto huu kuna uhai tu na mahitaji ya utashi.

Wanamwambia Mtenzi kuwa wamtafuta paa naye anawaambia amekuwa akiwasubiri kwa miaka mingi. Pia, anawaarifu kuwa paa amepita hapo na wakivuka upande ule mwingine wataona nyayo zake na hazitapotea tena kwa sababu katika ng'ambo hii uongo umejitenga. Cha kushangaza ni kuwa Mtenzi anainama na kunywa maji yote yaliyokuwa mtoni. Anawaambia kuwa haya ni maji ya uzima ambayo hulainisha shamba la mawazo na wanaweza kuvuka. Katika ng'ambo ya pili wanaona nyayo za paa kwa uwazi zaidi. Sasa ni watano, "Mimi" mwenye upinde na mishale, Nabii

mcheza bao, Mtume mhamisha milima, Mfuasi mwenye mguu mrefu na Mtenzi mkausha maji.

Kwa mbali wanaona binadamu lakini anatembea kinyumenyume. Anawaambia kamwe wasitegee kweli mgongo. Anapofika mbali kidogo anawaambia kuwa wamepata habari zao. Anaendelea kupiga kelele na kusema "*Nagona*!"(uk 51) Wanaanza sasa kuona mlima na kwa mbali wanaona jengo lililozungukwa na ndimi na mikuki ya moto. Wanapolikaribia linafunguka lenyewe na msichana anakuja mbio kuwapokea. Moja kwa moja anamjia "Mimi", anainua mkono wake na kusema*"Shujaa msaka paa!"( uk 52)* Tunakaribisha na tunaaarifiwa kuwa mfalme anatusubiri. Wanapoingia ndani muziki wa ajabu kama sauti za ndege unapigwa. Wanamfuata msichana hadi penye duara ambayo imezungukwa na mikuki ya moto. Anamweleza mfalme kwamba ameleta mashujaa wasaka paa. Msichana anawaambia wasujudie mfalme kwa kusema "*Atuna Kiputa!*"(uk 53). Mfalme anafumbua macho na kuwatazama. Wanaambiwa wainuke na kwamba amekuwa akiwasubiri kwa miaka milioni moja. Anaendelea kuwaambia wakisakacho kiko hapo na anahofu kuwa watamshika paa ambaye amewashinda wengi. Wanapelekwa kwenye bonde la mauti na yule msichana. Wanatoka nje na ni kama wamekaa mle ndani miaka hamsini. Msichana anawaongoza bondeni na wanaanza kuona mifupa imetawanywa ovyo ovyo na pandikizi la mtu lililo uchi linakata mtu kwa shoka. Wanaarifiwa kuwa mtu huyu alikuwa msaka paa na ni mwafalsafa mashuhuri na kuwa waliomsaka paa na kukosa kumshika waliuawa na wote walishtuka.

Ni jioni wanapoanza safari ya kurudi kwenye ngome. Lango linafunguka na wanapata askari wawili. Wanapewa malazi na baadaye, msichana anarudi na kuwaagiza

wamfuate na wanaongozwa hadi maliwatoni ili waoge. Msichana anakuja asubuhi kuwaamsha na anawaongoza hadi kwa mfalme lakini wakati huu hakuna muziki, ni viti vilivyoongezeka na wanaketi.

Mfalme anawapa vikwazo vinne. Kikwazo cha kwanza ni kulima shamba lake ndogo siku io hiyo. Shamba lilikuwa ndogo kiasi cha robo eka na mioyo yao inafurahi. Arthi ilikuwa ngumu karibu wakate tamaa, Mtenzi mkausha maji anainama na anatapika maji aliyokunywa mtoni. Anaendelea kutapika na mwishowe udongo ukawa tope. Inapofika adhuhuri wanakuwa wamemaliza na wakati msichana anakuja kuwaita kwa chakula cha mchana anashangaa. Kesho yake mfalme anawaita mashujaa na kuwapa kikwazo cha pili cha kuhamisha mlima kabla ya siku itakayofuata. Msichana anawaongoza hadi kwenye mlima. Siku hiyo Mtume anajaribu na kushindwa. Usiku wa manane Mtume anawaamsha na wanajaribu mara ya mwisho. Wanaandaa shingo zao kwa shoka kali la jitu.Mtenzi anasukuma mlima mara hii kwa bega na mlima unaanza kuondoka polepole. Kesho yake mfalme anaamshwa na mionzi ya jua inayopenyeza dirishani. Mfalme haamini macho yake na anawapa kikwazo cha tatu.. Anataka kiko chake alichoacha nchi ya Sabira, mwendo unaochukua miaka saba kufika siku io hiyo. Mfuasi anatumia mguu wake mrefu kuleta kiko. Mfalme anapokipata anaanza kuwa na wasiwasi kwa sababu huenda wakafanikiwa. Anawapa kikwazo cha nne, anataka mmoja wao acheze bao na paa na kama watashinda watamchukua paa na kuingia katika duara ya ukweli. Nabii anacheza naye na anashinda.Wanafurahi sana, “Mimi” anasogea na kumfunua paa toka kichwani hadi miguuni. Anapomfunua muziki unaanza. Adhuhuri wanaanza safari na wanaitwa wenye maarifa. Wanahisi kuwa wazee kwani wamekuwa hapa kwa miaka mia nne na hamsini. Wanaliacha jengo na kuelekea kwenye duara. Mtenzi

anafika na kutuaga na paa anamwonya ajihadhari asikumbwe na mafuriko ya damu. Mfuasi pia anafika tunapofika nyikani na anatuaga. Paa anamwambia ahakikishe kibuyu chake kina maji kwa sababu wasakaji wengi watapita njia hii.

Paa anaendelea kuongoza hadi wanapofika machungani. Nabii na Mtume wanafika na mtume anasema kuwa ameanza kuwa na matumaini lakini paa anamwambia kuwa huu ni uzushi kwani "*kweli imo katika kimya*"( uk 63). Wanaendelea na safari na sasa ni wawili. "Mimi" mwindaji na paa wa ajabu. Paa anaongoza na :Mimi" anaanza kutamanitamani na kujiona mtu mzima tayari kushika madaraka na majukumu. Wanaendelea kutembea paa akiongoza na "Mimi" nyuma akimsanifu. Mwishowe wanafika pale "Mimi" alikuwa amekuta msichana akikoga. Yule mwanamke yuko palepale na wanakumbatiana na "Mimi" kwa muda bila kusema neno. Huu ni undani katika undani.

Kesho yake asubuhi "Mimi" na yule msichana wanaanza kujenga vibanda vya mviringo aina ya msonge. Wanakanywa na yule mwanamke kutoruhusu neno lolote kutoka nje ya duara. Wanajenga vibanda viwili ili wangoje siku ya Ngoma Kuu. Paa anaagiza "Mimi" azime mshumaa na mwili wa paa unaanza kutoa mwanga na kumulika kibanda kizima. Uzuri wake unaongezeka, anamwita "Mimi" aende kwake lakini anapojaribu kumshika anashusha mikono yake. Anamwambia ni lazima kwanza wapige myeleka na "Mimi" akifanikiwa ataruhusiwa kucheza ngoma katikati ya duara. Anajaribu lakini hashikiki, mwili wake una utelezi. Paa anamshika kwa nguvu, anamwinua na kumtupa chini kama gunia na anaiweka miguu yake kwenye kifua chake. Anavua ushanga na kumvalisha shingoni. Anachukua nguo zake na kumpungia mkono. Mwanamke mwenye mimba anatoka kibadani na anapoona

nikigaragara anasema *"Oo!Hapana! Anguko la pili! Ndiyo maana kishindo kilikuwa kikubwa! O Hapana!"* ( UK 68). Anaona kitambaa alichoachiwa kupanguzia damu na anakikunjua. Katikati mwa kitambaa hiki pamenakishiwa maandishi ya uzi wa dhahabu neno "*Nagona*" (uk 69). Anasoma neno hili kwa shida. Anasema kushindwa kwake kumeandaa njia ya majilio ya pili kwa sababu kushindwa kuna ushindi. Anaporudi kibandani huyu mwanamke anamfunika na kuondoka na mshumaa lakini mbuni anauzima kwa mbawa zake. Baada ya dakika chache "Mimi" anapachikwa kwapani na jitu. Linaelekea bondeni likipiga kelele za "*ushindi*" (uk 69).

### 3.1. 6 UVUMBUZI

Kila mahali ni pakavu na vumbi jeupe kama chokaa limefunika ardhi. Wapiga ngoma wamekaa katika hali ya duara na wanaimba "*utenzi wa kiyama*" (uk 70). Kitu fulani kinajiviringisha karibu nao na ghafla mtu anayepiga kelele anaibuka kwenye vumbi. Anasema "Potelea mbali na *Cogito!* Hakuna *causa ultima* katika duara! Tunachohitaji ni *disciplina voluntatis*!" ( uk 70) Anashtuka anapowaona wacheza ngoma kwa sababu hakuwa anawategemea na anawaarifu kwamba mcheza ngoma ni yeyote yule anayeweza kufikiri. Anasema hata yeye ni mcheza ngoma na alikuwa katika mazoezi ya mazingaombwe atakayoyaonyesha siku ya Ngoma Kuu.

Anapokuwa akiendelea kusema mtu mwingine anaibuka vumbini na kupiga kelele "*Uvumbuzi mkubwa! Uvumbuzi mkubwa ambao umepata kufanywa ni wa roho!"* (uk 71). Anastuka anapowaona watu wengine karibu naye. Anawauliza wao ni nani kwa sababu maneno aliyoyasema hayapaswi kusikika na kiumbe chochote isipokuwa dhamiri. Anawauliza wanavyofikiri wao wenye roho na yule mtu wa kwanza kuibuka vumbini anasema ni uzushi. Anasema "*Huwezi kutenganisha roho na mwili*" . (uk 71). Mtu wa pili pia alizoea kufikiri hivyo lakini tangu apoteze roho yake

alipoamrishwa kuisafisha katika mto wa uhai wa milele ameacha kujali swali hilo. Roho ilimponyoka na kusafirishwa na mkondo wa maji hadi bahari kuu ambamo ndoto huishia. Kwa sasa anajiona huru kwa sababu ya kuipoteza roho yake. Hao watu wawili walioibuka vumbini wanakimbizana huku mtu wa pili akisema hataki kusahaulika kabla ya Ngoma Kuu. Wapiga ngoma sasa wanajifunza wimbo wa pili "*Utenzi Baada ya Kiyama*" ( uk72).

### 3.1.7 UGONJWA WA BABU

Babu anazidi kuzeeka na dalili ya ishara haikuonekana na mwishowe "Mimi" anaanza kutazama kila kitu kwa uangalifu na hatimaye anapata ugonjwa wa ushaulifi hadi anaitwa kichaa. Anapoanza kuzungumza na dhamiri ya nafsi yake anaona pengine hii ndiyo ishara. Anataka kupaona mahali hapo na kwa hivyo anakaa akisubiri tukio la ishara.

Ni usiku wa manane mama anapomwita "Mimi"kutoka kibandani chake. Mama anamuagiza amfuate na wanatembea kuelekea kwenye kibanda cha babu. Babu amelala chali akitazama juu darini. Baba amekaa pembezoni mwa kitanda na anamtazama mgonjwa. Babu anageuza kichwa chake na kumwambia kuwa nyota yake anaiona lakini kwa mbali, anapumzika lakini kuhema kwake kunawadhibitishia uhai.

Ndege wa asubuhi wanapoanza kuimba babu anataka kujua vile Padri alimfanyia. Atuarifu kuwa ni mmoja kati ya wachekeshaji. Anafurahi ameondoka bila kummwagia maji kwani fikra za babu hazingekuwa na maana kwetu. Mama anapoenda shambani na baba madukani "Mimi" anaachiwa jukumu la kumwangalia

babu. Babu anamwambia kuwa askari wa mwanga watafika. Anageuza uso, anamtazama na kusema anakufa. Anashtuka sana anapotoa meno na kuonyesha dalili za maumivu makali. Anapomuuliza ama anaumwa anamwambia kwamba hakuna maumivu katika kufa, kuna masikitiko na huzuni.

Babu anamwangalia na anaona uoga na wasiwasi aliokuwa nao, anamwambia anayeogopa ni aliye na tamaa ya kuishi maisha baada ya kifo. Anaendelea kumwambia maisha ni kitu cha ajabu na kuwa nyuma hakuna nyayo na mbele hakuna nyayo,nyayo ziko katikati tu. Anamuuliza angetaka kuwa nani katika uhai wake. Anamjibu kuwa angekata kuwa mwalimu. Babu anamwambia kamwe asijaribu kufunza jambo ambalo hana hakika nalo, na asidai kuwa na haki mikononi mwake. Ananena neno "*Nagona*" tena kwa sauti kubwa. Anapomuuliza huyu ni nani anamwambia kuwa sasa yuko tayari kuingia kwenye duara na aendelee kusubiri ishara. Baada ya muda, babu anapiga mwayo mmoja mrefu na kusema mambo mawili "*maisha hayatakwisha bali watu waishio*" na "*wakati titi la nyati,hukamuliwa kwa shaka*" (UK 78). Anamwambia haya ni mashairi na kumsihi ayasome. Siku hii hakupata raha kwa sababu neno kifo lilijificha kati ya nyufa za ubongo wake na alikumbuka kila wakati alipojaribu kulisahau. Anaendelea kumwambia kwa muda wote wa uhai wake "*Nagona*" alimpiga chenga. Anamwambia kuwa nyota yake ni nzuri na huenda akabahatika kumshika mikononi mwake. Anaendelea kusema Nagona ni mwanga na yuko kila mahali na alipo uwongo umejitenga, ni yeye peke yake aliye pale. Hakuna anayeweza kuepuka mvuto wake, ni wa kila mtu. Anamwambia atamwona wakati ishara itakapotokea katika bonde la taaluma. Hapa ndipo kitendawili kimeanzia na askari wa mwanga wamelala hapa. Maneno yake ya mwisho kwake yalikuwa daima afuate duara na kila wakati atazame katikati. Kitu

fulani kilimkwama kooni na kwa shida anasema "*Nag...Nag...Nag...*" hakusema neno tena na macho yake yakafumba. Ndugu zake walipofika walimzika katika kaburi la kijiji kilimani.

### 3.1.8 MJADALA WA UNGAMO

Huu ni mjadala kuhusu matukio ya kila wakati ya kutakafuta wanawake na ufisadi ambao unachukua umbo la ungamo linalosemwa na "Mimi" kwa Padri. "Mimi" anaungama dhambi zake kwa Padri na anamwambia kuwa, amezini na wanawake tofauti mara nyingi, ameshiriki katika mauaji ya watu wanne kwa sababu ya wanawake na cheo cha Urais, ameiba pesa za umma na kufungua viwanda na hatimaye kutawala uchumi wa dunia. Anasema alishiriki mauaji ya marais hasa kutoka ulimwengu wa tatu, alishiriki mauaji ya mamilioni ya Wayahudi na watumwa weusi. Pia alishiriki katika mauaji ya mamilioni ya Wahindi Wekundu, Mapigini, wenyeji wa Afrika na Marikani ya Kusini. Anasema aliua kwa sababu aliamini waliteuliwa kuutawala ulimwengu. Mwisho anaungama dhambi ambayo ni kubwa zaidi ya kumuua Papa.

Padri hamwamini "Mimi" na anasema mauaji haya yote yamo katika ndoto zake za kiwendawazimu . "Mimi" anamkumbusha Padri kuwa wako wengi katika mmoja, ni wengi wenye dhambi. "Mimi" anaendelea kusema kuwa haamini katika Mungu, anasema uwongo, anatamanitamani na anajionaona. Kama Padri angekuwa na uwezo angemwamuru atapike roho yake akaisafishe katika mto wenye maji ya uzima lakini anamwamuru asali sala ya imani mara kumi, na rozari kwa muda wa siku tatu. Wanapoagana "Mimi" anaenda kujiandaa kwa siku ya Ngoma kuu.

### 3.1.9 NGOMA KUU

Sura mbili za mwisho zinahusu hadithi ya matayarisho na kufanyika kwa Ngoma Kuu na matokeo yake. Ingawa kwa uchungu, Waafrika hatimaye wanacheza ngoma kwa mtindo wao, huku wakishida na kuwavutia wengine katika utambuzi wao na kwa hivyo kuonyesha matumaini katika mashindano ya mwisho ya Ngoma Kuu.

"Mimi" anapoamka anakuta watu wengi wameanza maandalizi. Anamtembelea jirani yake Mwafrika na anamkuta akilemba kofia na unyoya wa mbuni. Kofia ni ya kila kiongozi wa kikundi. Jirani anamwarifu "Mimi" kuwa viongozi wengi watakuwa wazungu kwani watu wengi ulimwenguni wamechukua majina yao. Mapagani watapangwa mbali sana na kitovu cha duara. Vichaa wataongozwa na mwanafalsafa fulani na kiongozi wa watawa wasio na majina ni mnafiki mkubwa."Mimi" anawekwa katika kikundi cha vichaa kwa sababu hawezi kukumbuka jina lake. Anafurahi kwa sababu huo ndio uhuru autakao na anapatiwa njuga afunge miguuni, Anaambiwa kuwa njuga hufanya mwili wote usisimke wakati wa ngoma, zinawezesha binadamu kuvuka daraja linalounganisha uhai na ufu na pia zinasaidia katika kuwasiliana na wahenga.

Viongozi wanavaa ngozi ya simba ndume kiunoni na wengine wanavaa ngozi ya nyani, mbuzi na usinga wa mkia wa nyumbu ndiyo alama ya umanju. Shanga zinaunda vazi la kiunoni ambalo ni alama ya mapenzi na hupendeza mcheza ngoma anapochezesha mabega yake. Pia, shanga ni alama ya kufungamana na mtu fulani.

"Mimi" anaelekea nyumbani kujitayarisha. Anavaa majani makavu ya migomba , mifupa ya samaki, majalala na njuga moja. Siku inayofuata ni siku ya Ngoma Kuu ambayo ni ya kukoga karne. Wasichana wote walikoga katika ziwa takatifu na

wavulana waliimba nyimbo za vita na ushindi mpya kwa kizazi kijacho. Wanawake nao waliimba nyimbo za mazishi na wanaume walitoa tu mlio kama wa nyuki bila kusema neno. "Mimi" anakuwa katika kundi hili la wanaume. Kufikia saa kumi wote wamekwishatakasika kimwili. Wako tayari kutoa sadaka na kula nyama ya karne.

Baada ya kula wanajiandaa kwa sababu ya Ngoma Kuu itakayofanyika usiku huo. Ngoma zinaanza kusikika hapa na pale. Kila mmoja anajiunga na kiongozi wa kikundi chake kwa mazoezi madogo na maelekezo ya mwisho kuhusu mbinu za uchezaji. Kikundi cha vichaa kinafanya vurumai ili watazamaji wacheke. Kiongozi wetu anatwambia vurumai ndiyo njia ya ushindi na ufundi umo katika vurumai.

Usiku wa Ngoma Kuu unakuwa usiku wa mbalamwezi. Ngoma ya kuwaita watu inalia saa mbili hivi za usiku. Damu imechemka na wengi wanajikuta uwanjani bila kufahamu. Wanatekwa na ngoma na ni kama wanaitika mwito fulani usiozuilika.

Ngoma za aina nne zilikuwa zimeteuliwa kucheza katikati ya duara kwa muda usiozidi nusu saa kwa kila ngoma. Hizi zilikuwa ngoma mashuhuri wakati fulani katika mkondo wa historia. Ngoma ya kikundi cha "Mimi" ni ya nne. Ngoma ya kwanza inachezwa kisayansi na imepangwa vizuri. Wafuasi wanaimba wimbo uitwao '*De Anima*', wanaendelea na'*Politica*','*Metaphysica*' na mwisho wanamalizia na '*De Poetica*' (uk 104*),* wimbo unaowaacha wasanii wengi wameduwaa. Kikundi cha pili kinaongozwa na mwanasaikolojia mashuhuri. Kikundi hiki kinaimba nyimbo ziitwazo '*Totem*', '*Oedipus Comlex*' na *Neurosis*' (uk 104). Ngoma hii inapokelewa kwa mchanganyiko wa ndio na hapana. Ngoma ya tatu inaingia kwa kelele za "*Chinja! Chinja!*" ( uk 105). Ngoma hii inaongozwa na mwanamapinduzi na mtetezi wa

wanyonge. Wafuasi wanaingia katika duara wakiimba wimbo wa kimapinduzi. Kiongozi wao ananyoosha usinga wake juu na kutongoa nyimbo kuhusu maproletariati, nao wafuasi wake wanaitikia kwa maneno yanayohusu ubepari na usoshalisti. Wanamaliza na nyimbo zinazohusu mikinzano ya kitabaka na majilio ya usawa. Inabidi waondolewe kwa sababu muda wao umekwisha. Wanakataa kutoka kitovuni na wanadai kwamba wakati wao wa kushika nafasi ya kucheza Ngoma umewadia. Walitolewa nje kwa nguvu hali wakiimba "*Alutta Continua*" (uk 106). Sasa inakuwa zamu ya kikundi cha "Mimi" kuingia katika duara. Wanaingia uwanjani bila mpango na watu wote wanaangua vicheko. Wanaimba,

*Tumekuja kucheza zeze*

*Zeze la vurumai*

*Tunaweka kituo cha karne*

*Chekeni mbavu ziwaume*

*Yachekeni maisha mpate kuyaishi*

*Aliyewanyima uhuru kafa* ( uk106).

Wanaendelea kucheza kwa vurumai na baada ya muda mfupi kila mtu alikuwa anacheza kwa mtindo huu. Huo ukawa mwanzo wa vikundi vyote vya ngoma kuanza kupiga ngoma zao bila kufuata mpangilio. Uwanja unacharuka na inakuwa vurumai tupu.

Ghafla wanakuta wanasukumwa na nguvu fulani kutoka kwenye kitovu cha duara. Sehemu ya katikati ya duara inabaki tupu na mwanga mkali umejaa ile sehemu. Mwanga unapofifia wanaona kizee kimesimama katikati. Kizee kinainua mkongonjo wake na kuwaambia waendelee kucheza na uwanja unawaka moto kwa vurumai.

Wamechoka sana lakini kizee kinapogusa "Mimi" kwa fimbo anapata nguvu za ajabu na anazunguka pale katikati kama pia. Anapotazama juu anaona mwanga mkali ukishuka machoni mwake. Pia anasikia kitu fulani kama umeme kikipita machoni mwake na wakati huo huo mlio mkubwa wa radi unasikika. Anasikia sauti za umati wa watu wakipiga kelele '*Huraa Atuna Kiputa*' ( uk 108). Halafu kimya na mwisho wa vurumai. Uzito unapungua mabegani mwake na kizee kinapiga kelele "*Nagona! Nagona!"( uk 109).* Mwishowe kizee kinatumbukia kwenye duara na kupotelea huko.

Ngoma kuu inachezwa usiku kucha, wanatawanyika asubuhi, mamilioni ya watu wamekufa na wengi wameumia. Yule mwanamke mja mzito anajifungua kitoto cha kike kutokana na mrindimo wa ngoma na kelele za vurumai. Mtoto huyu anaitwa Nagona. Tangu siku hiyo "Mimi" anakuwa mfuasi wa kitoto kinachozaliwa.

Ilikuiwa ni lazima Kezilahabi angeandika riwaya ya *Nagona* kwa sababu ya mtazamo na imani yake. Riwaya hii inachokoza mawazo ya mtu. Kwa sasa Kezilahabi ana msimamo wake kwamba binadamu hafi lakini anaendelea kuishi. Kezilahabi amelichagua kila neno katika riwaya ya *Nagona.* Kila mstari na sentensi umekaguliwa kwa umakini na umantiki, ili kuwe na muunganiko wa msuko na matukio. Kila neno limewekwa ili lilingane na hoja au tukio fulani na kila sehemu ina uhusiano na sehemu nyingine.

Kezilahabi amechanganya mhusika "Mimi" na maisha yake kwa sababu amekuwa akitatanika sana kuhusu imani mbalimbali za uhai na kifo. Amekuwa akizitazama dhana hizi na kuona zinavyoathiri maisha ya watu na jinsi zinavyopingana zenyewe.

Watu wanalazimika kuwa nazo na hawana uwezo wa kuziepuka. Hili ndilo tatizo kubwa Kezilahabi analotatua.

Kezilahabi amejaribu kuandika kwa lugha rahisi ili aeleweke lakini dhana mle ndani ndizo zinatatiza. Imani ya uhai na kifo ni tata na inaaathiri maisha ya watu wote na dhana hizi zinaingiliana na haziepukiki. Hili ni tatizo kubwa na Kezilahabi anaona kuna umuhimu wa kuzingatia kosmolojia mpya. Kosmolojia inayozingatia tatizo la utu na nafsi. Anataka wasomaji wake wastahimili ukweli kuwa tunakufa lakini kwa kweli hatufi. Ametafuta jibu kwa sababu hatuna suluhisho lingine. Kwa jumla, anazungumzia dhana zinazohusu muundo wa nafsi ya mwanadamu. Dhana ya uhai na kifo katika riwaya hii si ya Waafrika peke yao lakini ni ya watu wote ulimwenguni. Kwa hivyo kusudi sio Mwafrika peke yake na jinsi Waafrika wanavyofikiri kuhusu uhai na kifo lakini ni kuonyesha ndivyo walivyo Waitaliano, Wahispania, Waingereza, Wajerumani, wote wanaamini kuna kuishi baada ya kufa. Dhana hizi zimeenea kote duniani.

Kezilahabi ameona kuwa wataalamu wa kisasa wanaotetea Uafrika wameshatenganishwa na Uafrika wao halisi kwa muda mrefu na sasa anataka warejelee Uafrika halisi. Kezilahabi anaona himaya ya mtanziko wa Waafrika kama umewekwa mbele zaidi kuliko amri za kisheria za Senghor, Kaunda, Nyerere na wengine. Kutokana na maelezo haya, kuweko kwa mwanadamu kumekuwa fumbo kwa muda mrefu. Kusudi la riwaya hii ni kuonyesha kukua kwa mtazamo mmoja wa mwanadamu kuhusu dhana ya uhai na kifo. Ili Kezilahabi aweze kutimiza dhamira hii, ametumia ishara mabalimbali kimafumbo. Anwani ya riwaya hii ni fumbo kubwa.

## 3.2 MAANA YA ANWANI

'Nagona' mwenye fumbo anafahamika katika viwango viwili. Katika kiwango cha kwanza, ni jina la paa anayepotea kila mara na ambaye anabadilika na kuwa mwanamke mrembo. Katika kiwango cha pili 'Nagona' anajidhihirisha kama ishara ya utambuzi na ukweli. Utambuzi na ukweli kulingana na fikra za Kezilahabi ni za kufikirika. Hata hivyo ukweli unabaki kuwa vipandevipande, Kwa hivyo cha muhimu ni kutochoka kuutafuta huu ukweli. Kezilahabi anahusisha huku kufikiri na jinsi anaavyojiona yeye kama mwandishi, na yale tunatarajia kupata katika sehemu yake ya tatu inayokamilisha mfululizo wa sehemu zake tatu. Kwa maneno yake mwenyewe Kezilahabi anasema,

> *(...) tunaianzia katika* Nagona *na kuiendeleza katika* Mzingile*(...) 'Nagona' ndiyo ni dhana yenyewe, na kuna watu ambao walihusika Katika kutafuta huo ukweli. Na mwishoni mwa* Mzingile *tunaona huu mzunguko tena . Unaanza mahali pamoja lakini unaishia pale pale tena huko mwishoni kuutafuta huo ukweli. Na hapo ndipo tunapofikia hatua Kwamba ukweli ni kitu ambacho hatuwezi kukishika mikononi mwetu. Kwa hivyo tutaendelea tu kukitafuta katika uandishi wetu wa kifasihi. Na hapo nilipo siwezi kutoa jibu kamili kwa sababu bado naendelea na wazo la Kuutafuta huo ukweli. Na katika kitabu kitakachofuata kutakuwa na Mwendelezo zaidi* (mahojiano na Kezilahabi katika Diegner 2003).

Kutokana na maelezo haya, Nagona ni wazo lenyewe. Pia ni mwanga na huashiria matumaini, nuru ya akili na kufanya upya.

## 3.3 FUMBO LA UHAI NA KIFO

Mwandishi katika riwaya ya *Nagona* ametumia ishara mbalimali kimafumbo kuwasilisha maudhui ya uhai na kifo ambayo ni ya ulimwengu wote. Ametumia fasihi simulizi ambayo kulingana na Sengo (1977) huweza kulinganishwa na mwavuli unaokinga amali za maisha ya watu. Jung alikuwa amegundua kuwa ishara nyingi ni za ulimwengu wote. Ishara hizi hazina umbo lililo wazi na kwa hivyo zinajidhihirisha kupitia dhana tofauti za ulimwengu unaotuzunguka. Maudhui ya uhai na kifo yamesawiriwa kimafumbo kupiti ishara mbalimbali kama vile,

### 3.3.1 ISHARA YA MAJI

Kulingana na nadharia ya Kikale, mithiolojia nyingi kutoka Afrika zina visasili vya uumbaji zinavyosema, dunia ilikuwa ziwa kubwa na ilikuwa imefunikwa na maji na hapo ndipo uhai ulitoka. Kila chanzo cha maji huashiria mwanzo wa maisha na hivyo uhai. Uhai hutokana na maji ya asili. Kila mwanadamu ametoka kwa maji na kwa hivyo visasili hivi ni sitiari ya maisha mwanadamu.

Maji ni ishara ya uumbaji, kufa, kuzaliwa na kuzaliwa tena. Katika riwaya ya *Nagona* maji yanaashiria kuzaliwa kwa nafsi ya mhusika "Mimi". Kwa Mkabala wa nadharia ya Kikale Kezilahabi anasema,

> *Ulifika wakati ambapo ajali ilikuwa lazima itokee. Ajali hii ilitokea katika bonde la hisia. Wacheza ngoma wawili wakiwa nje kabisa ya duara walicheza ngoma yao ya pumbao katika hali ya uchi wa myama. Katika udadisi wao wa kutaka kutalii mipaka ya bonde hili waliteleza na kuanguka mahali penye majani mororo palipowaongezea fahamu. Walipopata urazini walifanya mchezo wao wa kuteleza na kuanguka tena na tena, mwishowe*

> *ikawa ni kawaida, ukawa si mchezo tena bali ukweli. Katika ukweli huu palitokea gharika katika mto wa bonde uliopeleka maji ya mvua baharini, ambamo wewe uliibuka siku moja ukilia njaa…*(uk19).

Pia, maji ni ishara ya mzunguko, uhai na mshikamano. Kwa kuhusisha maji ya kazi bunifu na uowevu unaopatikana katika miili ya wanadamu, kulingana na nadharia ya uhalisiamazingaombwe Kezilahabi anasema, "*Nilipofika karibu na mto nilishangaa. Mto ulikuwa umejaa damu tupu ambayo ilikuwa ikitiririka kwa nguvu…*" (uk11). Maji ni ishara ya uhai wote, kusafisha na ni nguvu kali ya maisha, nguvu za kuishi na kufikiri na ni fumbo kubwa la uumbaji.

Riwaya ya *Nagona* inasawiri dhana ya uhai na mhusika "Mimi" anazaliwa. Mhusika anasikia mrindimo wa mto na anahisi kuelekea usawa wa mto huu na kuelekea unakotoka . Safari ya kuelekea usawa wa mto ni sitiari ya safari ya maisha . Kwa mkabala wa nadharia ya uhalisiamazingaombwe mhusika "Mimi" anasema,

> *Niliskia tu mrindimo wake maana si kuusogelea kwa kuogopa nyoka. Nilijikuta natembea kuelekea usawa wa mto huo. Nilihisi kuwa nilikuwa nikielekea unakotoka. Kama huo ulikuwa mwanzo wa safari yangu sina hakika. Lakini….*( uk1).

Kulingana na maelezo haya ni dhahiri kwamba mto ni ishara kamili ya maisha. Maisha yamejaa vurugu na matatizo mengi na ndio sababu mrindimo unasikika . "Mimi" anauogopa mto kwa sababu maisha ya hapa duniani yamejaa unafiki, mauaji, ubinafsi uchawi na mambo mengine mabaya .Mhusika anaenda sambamba na

mto unakotoka kuonyesha kuwa mto una uhai hata utokako na hivyo uhai hauna chanzo mahsusi.

Ukweli unapatikana kutokana na ajali iliyotokea wakati wacheza ngoma wawili walicheza ngoma yao katika hali ya uchi wa mnyama. Ajali hii inawaongezea wacheza ngoma fahamu. Mchezo wa kuzaliwa na kuzaliwa tena mwishowe unakuwa si mchezo wa kawaida bali ni ukweli. Ukweli kwamba binadamu hafi bali anazaliwa tena katika umbo lingine. Kwa mkabala wa nadharia ya Kikale, Mtenzi anaendelea kusema,"*haya ni maji ya uzima, hulainisha shamba la mawazo*" (uk 50). Maji ni nguvu kali inayosaidia kufikiri. Dhana ya uhai na kifo imetumiwa na wanafasihi kufikiri zaidi wanapoandika kazi za fasihi.

Mito hutumika kama mipaka, kuvuka mto ni kwenda upande wa pili na ni kupata wazo ambalo haliwezi kubadilishwa. Fasihi kutoka Afrika huonyesha mito kama vyanzo vikuu vya uchumi hivyo ni chanzo cha kudumisha uhai. Mito husawiri ukosefu wa mpito wa wakati na pia hatua za mzunguko wa maisha. Ishara ya maji ni ya ulimwengu wote na maji yana dalili za usafi na uwezo wa kuzaa na kuzaa tena. Kwa mkabala wa nadharia ya Kikale, Kezilahabi kupitia mhusika Mtenzi anasema,

> *Mimi naitwa Mtenzi. Mimi ndiye mkausha maji. Mfuasi wa mwisho. Baada ya mto huu kuna uhai tu na mahitaji ya utashi. Watakao kuvuka Mto huu hupita hapa* (uk 50).

Kutokana na maelezo haya, maji ni chanzo cha uhai na shauku kubwa ya kutaka kufanya jambo fulani. Mhusika na wenzake wanamtafuta Paa. Amepita hapa na amevuka ng,ambo ya pili ambapo uwongo umejitenga na hakuna matatizo na vurugu

za maisha. Ni sharti mhusika na wenzake wavuke upande wa pili ili waweze kumshika paa wanayefuata. Ng'ambo ya uhai.

Pia, maji ni ishara ya busara ama hekima. Wazo hapa ni kuwa, maji huchukua umbo lake na huenda katika mkondo usiokuwa na vizuizi vingi. Ishara ya maji huonyesha hekima ya hali ya juu ambayo kila mwanadamu angependa kuiga. Wagiriki wa kale walifahamu kuwa maji yana nguvu wakati wa mabadiliko. Kutoka uwoevu hadi hali ngumu, hadi kuwa mvuke, maji ni kifano cha ugeuzaji wa umbo, tabia na mzunguko wa mawazo ya falsafa. Ni kama vile Wamisri wa kale walitegemea sana mto Nile. Mto huu una uhusiano na kuweko kwao.

Pia maji ni ishara ya mwendo, kufanya upya, baraka, ujuzi usiohitaji kufikiri, kuakisi, nafsi iliyofichika, kurutubisha, utakaso na mabadiliko. Hekima ya maji haina kikomo na yanaashiria maisha ya milele.

Kulingana na C. Gustav Jung maji ni ishara kuu ya kutokuwa na fahamu . Maji yanaashiria kuzaliwa na kuzaliwa tena , mtiririko wa mpito wa wakati milele, mabadiliko ya hatua za muhula mzima wa maisha na kupata umbo la binadamu la uungu.

Maji yana nguvu za kufanya upya na yana nguvu za kuharibu kama tunavyoona Tsunami katika mataifa ya Asia na Hurricane zinazoathiri maeneo ya Amerika. Visasili vya mafuriko ni sitiari yenye nguvu kuhusu uwili wa maji wa kuumba na kuharibu. Kwa mkabala wa nadharia ya Kikale Kezilahabi anasema,

*Wakati sasa umefika wa kwenda kuosha roho zenu katika maji ya uzima wa milele. Nendeni bondeni lakini jihadharini na mafuriko. Mnaruhusiwa Sasa kufungua nyuso zenu mzitazame roho zenu... Haikuchukua muda Wakawa wamerudi mbio...* (uk30).

Hata ingawa mto ulikuwa umewasafishia roho zao kwa karne nyingi, wamezipoteza katika mto uo huo kupitia kwa ajali. Hapa maji yanaashiria kuwa na uhai na kifo.

**3.3.2 ISHARA YA MSITU**

Misitu kama ilivyo mito, milima na mbingu ina utendakazi wa ndani zaidi katika tamaduni nyingi Kwa mkabala wa nadharia ya uhalisiamazingaombwe, misitu ni mahali ambapo mipaka kati ya uhalisia na uwezo wa kubuni, historia na visasili hupata ukungu, huku ikiashiria dhana zinazoeleweka na kuleta kumbukumbu za pamoja ulimwenguni kote.

Msitu huashiria safari ya akilini na nafsi. Mwanadamu akiwa kwenye msitu huwa katika hali ya kufikiria. Misitu ya kufikirika katika hadithi za kubuni za watoto imekuwa ikiwakilisha ulimwengu mwovu uliojaa wanyama na giza. Wanadamu wakiwa msituni huwa na maisha ya upweke.

Misitu ya mazingaombwe huashiria yote mwanadamu huogopa na yote mwanadamu hupenda na jambo hili ni fumbo .Msitu haujulikani na bado mhusika anadhubutu kuingia mle, anatambua sehemu chache, anapata umahili, uelewa na anafurahi. Msitu wa mazingaombwe hauna kipimo cha wakati na ni mkubwa kuliko mwanadamu. Kukaa karibu na msitu ni kuwa na uhusiano wa kiroho na yaliyo ndani na ya kale kuliko utambuzi wa kufa. Kukaribia msitu wa mazingaombwe ni jambo muhimu

katika kuanza safari ngumu na ndefu ya mishangao ya ulimwengu na nafsi ya mwanadamu. Kwa mkabala wa nadharia ya uhalisiamazingaombwe Kezilahabi anasema,

> *Kama huo ulikuwa mwanzo wa safari yangu sina hakika. Lakini nilijikuta nimechoka . Mbele yangu niliona jiwe jeusi. Nilijikokota kwenda kulikalia. kabla sijakaa nilisikia mtu Akikohoa. Kwa hofu nilisimama wima, nikaangalia huku na huko. Hapakuwa na mtu! Nilitembea kwa harakaharaka kutoka hapo Mahali. Nilianza Kusikia Sauti za watu wasomao vitabu. Walikuwa Wakisoma bila kusikizana kila mmoja alikuwa akisoma lake. Sikuona watu wala shule...Nilijaribu kuongeza mwendo. Nilisikia vicheko karibu katika kila mti. Msitu nzima ulianza kunicheka* (uk 1-2).

Mtazamo wa sasa unaoathiriwa na tamaduni mbalimbali unaonyesha msitu kama mahali patulivu, mahali wanyama hupatikana na wahusika huenda ili kuondokea maisha yenye vurugu na kuungana na mambo ya asili. Misitu ni ishara ya mipaka kati ya uhalisia na utouhalisia. Watu waishiyo katika misitu hawaongei na lugha waijuayo ni kimya na nyimbo ni za ndege tu. Misitu ni mahali ambapo mwanadamu hawezi kutabiri yaliyomo na kwa hivyo ni mahali hatari. Ni mahali ambapo maadili ya jamii hayafuatwi. Ni mahali mazimwi huishi, mahali wachawi hufanya mazingaombwe katika sehemu ndogo zilizotengwa na mahali ambapo watu hulilia roho zisizojulikana.Kwa mkabala wa nadharia ya uhalisiamazingaombwe, Kezilahabi anasema,

> *Milio ya ndege ilisikika hapa na pale. Niliendelea kujikokota kwa magoti Kuelekea nisikokujua. Nilistuka napigwa kiboko matakoni na mgongoni. Mwanzoni nilisikia maumivu, nikajaribu kuongeza mwendo, lakini baada ya muda kichomi kilinizidi. Nilipigwa viboko mfululizo, lakini sikuweza Kujitingisha. Polepole nilijiona naishiwa nguvu na fahamu, na mwili ukafa ganzi* (uk 2).

Maelezo haya yanaonyesha safari ya "Mimi" msituni. Msitu unatawaliwa na kimya pekee na mhusika anasikiliza mwito wa mazingira yake tu. Kimya kinaashiria kifo na kusikiliza ndiyo njia pekee ya kuzungumza na upweke wa binadamu na nafsi yake. Mhusika anapitia mambo magumu na mateso hadi anapoteza fahamu.

Misitu pia ni ishara ya mapenzi na mwangwi wa misitu ulitolewa wakati wa historia ya vita vya pili vya dunia wakati misitu ya uzunguni iliwakinga na kuwapa makazi watu wasiojiweza ulimwenguni kutoka Italia hadi Ukreni. Pia misitu huashiria nguvu za ulimwengu na wakati usiokuwa na mwisho. Miti msituni ina mpito tofauti wa wakati na mwanadamu kwa sababu miti haihisi wakati. Wakati katika misitu hupimwa kwa miongo ikilinganishwa na jinsi mwanadamu hupima wakati kwa kuhesabu siku na miaka. Kipimo cha mara moja ni nyongeza ya wakati mwingi mno.

Msitu humsafirisha mhusika hadi karne zilizopita na huleta mambo ya kihistoria na ya kabla ya historia mbele ili yaweze kukabiliwa wakati wa sasa. Kwa mkabala wa nadharia ya Kikale, Kezilahabi anasema,

*Basi hayo ndiyo yalikuwa maktaba ya taifa. Walikata shauri kutupa vitabu vyao vyote huko. Vimeoza na miti imeota juu yake. Waliopata Kupita humo wanasema kuna mizungu. Waandishi wanalilia kusomwa wasife* (uk8-9).

Msitu ni mahali mtu asiyejiweza hupotelea na kwa ajali anakutana na sehemu ya wachawi au makazi yaliyolaaniwa. Misitu humpa mwanadamu utulivu na amani, Pia misitu ni shara ya uovu, kuhisi kupotea na uoga. Kwa mkabala wa nadharia ya uhalisiamazingaombwe Kezilahabi anasema,

*Ukimya ulitawala mji huu. Ulikuwa mji mdogo wenye barabara Moja kuu iliyokuwa wazi. Hakuna kiumbe hata kimoja kilichoweza kuonekana* ( uk 2).

Baada ya "Mimi" kupita na kuacha msitu anafika katika mji huu ambao haukuwa na binadamu yeyote hivyo hakuna matatizo yanayosababishwa na binadamu kama ya usherati, mauaji, ufisadi na mengine. Mhusika anajikuta peke yake hivyo ana utulivu na amani.

### 3.3.3. ISHARA YA MZEE

Kulingana na Carl G. Jung, huyu ni mhusika wa kutathmini, mwenye ujuzi, wa mawazo, wa utambuzi, hekima na mwenye uwezo wa kuhisi jambo haraka na pia anaelewa uroho wa nafsi. Ana sifa za maadili mema kama ukarimu na kila wakati huwa tayari kusaidia. Mambo haya yote yanafanya sifa zake za "kiroho" kuwa dhahiri. Anajaribu ubora wa maadili ya watu wengine na zawadi za watu hawa hutegemea majaribu haya.

Kulingana na nadharia ya Kikale, huyu mzee hutokea wakati nguli yuko katika hali zisizokuwa na matumaini na za kukata tamaa. Ujuzi anaohitaji nguli na upungufu wake unapatikana kupitia umbo la mzee msaidizi mwenye hekima. Mzee huonyesha nguli jambo la asili la pamoja na lisiloeleweka. Huyu mzee ana mwelekeo wa kike unaopatikana katika kutofahamu kwa pamoja kwa wanadamu wote. Kwa mkabala wa nadharia ya Kikale Kezilahabi anasema,

> *Utakapofika pale ambapo kila mwanadamu lazima afike utajua hukukosea ; kwani njia ya kwenda huko inajulikana kwa wote na inakwenda moja kwa moja bila kupinda. Huna haja ya kusoma kitabu chochote kupata maelezo ya kwenda huko, wala hakuna haja ya kusikiliza mahubiri* (uk 15).

Mzee anamweleza "Mimi" kuwa kifo ni lazima kwa kila mwanadamu. Wanadamu wote lazima wapitie kwa kifo ili waweze kuvuka ng'ambo ile nyingine ya uhai wa milele na kupatana na ndugu zao walioaga zamani. Anaendelea kumwambia njia ya kwenda huko ni wazi na haina vizuizi vyovyote. Mzee anataka "Mimi" awe shahidi wa kweli. Wanadamu kutoka jamii zote ulimwenguni wanapatana huko na wanadamu ni wa jamii moja.

Mzee pia anawashauri wazee wengine katika migogoro yao na wanapenda sana kusikiza hekima na masimulizi yake ya historia ya wakati uliopita. Kwa mkabala wa nadharia ya Kikale Kezilhabi anasema,

> *Babu yangu alijulikana sana kijijini. Wazee wengi walifika mara nyingi jioni kuongea naye. Baadhi walifika kutafuta mawaidha kuhusu migogoro yao, wengine walifika tu kusikiliza hekima yake na masimulizi ya historia ya wakati Uliopita*...(.uk15).

Kulingana na riwaya hii mzee huyu tayari amevuka ng'ambo ya pili na anayafahamu zaidi mambo ya sasa na ya kale, hivyo ana ujuzi na uelewa wa mambo zaidi na ndiposa wazee wengine wanafika kuomba usaidizi wake.

Mzee mwenye hekima ni mwanafalsafa wa maana sana anayejulikana kwa sababu ya hekima na ushauri wake. Anahudumu kama mwalimu kwa anayeingizwa jandoni ili kupata hekima. Ni mhusika wa kuigwa na mara nyingi hutumika kama mfano wa mzazi. Kwa mkabala wa nadharia ya Kikale anafundisha kwa matendo ustadi, umahiri na ujuzi wakati wote wa safari na uchunguzi na utafutaji. Kezilahabi anasema,

> *Wazee walikuwa wakitingisha vichwa vyao wakati babu akizungumza. Naye Padri alianza kujiona mwanafunzi. Aliondoka jioni kabisa baada ya kusikiliza mazungumzo ya wazee. Akasahau jambo lililokuwa limemleta* ( uk 18).

Padri alikuwa akichukia mazungumzo ya babu lakini baada ya kumsikiliza babu akasahau lililokuwa limemleta. Maneno aliyokuwa amesikia kuhusu babu yalikuwa yanapingana na yake lakini anaposikiliza yeye mwenyewe hatimaye anakuwa mwanafunzi wa babu.

### 3.3.4 ISHARA YA DUARA

Kwa mkabala wa nadharia ya Kikale, duara ni ishara ya kitu kizima na nafsi. Huwakilisha elementi nne ambazo ni dunia, maji, moto na hewa. C. G Jung anasema duara humaanisha uungu na kwamba Mungu kwanza alijihidhirisha kupitia uumbaji wa elementi hizi nne. Duara ni mstari usiokatika, hauna mwanzo wala mwisho na hauna mwelekeo na kwa sababu ya mambo haya duara ni kitu kizima, fumbo la uhai,

nguvu za vizazi, fikra, uwezo wa kufikri, jua, ukamilifu na ukweli wa milele. Pia huashiria mbingu, uhusiano kati ya umoja na wingi, pumzi, nafsi na roho.

Duara ni ishara ya dhana ya upamoja mmoja wa ulimwengu mzima. Duara huashiria kutokuwa na mwisho kwa mambo yasiyojulikana, yasiyopimika, yasiyoeleweka, na kutoweza kufafanuliwa kwa vipengele vya milele. Mambo haya hukanganya urazini wa akili za mwanadamu. Duara ni ukumbusho kuwa hatuwezi kufahamu kiini cha nafsi ya mwanadamu.

Vizazi vya kale vilikuwa na sura ya duara la wakati, hasa wakati wa kutambua majira na pia mapinduzi ya dunia. Binadamu anaweza kuhisi mabadiliko ya wakati na majira jinsi wahenga walivyohisi. Duara huashiria muhula mzima wa maisha.

Mtazamo wa Kiafrika ni wa ndani zaidi na kwa hivyo duara hujumuisha nguvu za nafsi, jua, mwezi, sayari, yai na huwa na maana ya kiroho. Kwa jumla vielelezo hivi vya duara ni sehemu ya fumbo la kutuonyesha picha iliyovuka uwezo wa mwanadamu wa kuuelewa ulimwengu wake. Kwa mkabala wa nadharia ya Kikale Kezilahabi anasema,

> *Mwanga wa jua ulipoanza kuonekana, nilihisi nasukumwa kutoka katikati ya duara. Kizee kilipiga kwa fimbo yake sehemu ya katikati ya duara halafu Kikazunguka kama pia. Kitovu cha duara pia kilianza kuzunguka. Palitokea Shimo kubwa kwenye kitovu ambamo kizee kilitumbukia na kupotea* ( uk109).

Haya maelezo yanaonyesha kwamba asili au chanzo cha wanadamu wote ni kitovu cha duara Uhai wa wanadamu wote hutoka kwenye duara.

Duara ni ishara ya kinga. Duara humkinga mwanadamu kutoka kwa hatari za ulimwengu na kutoka athari za nje ya duara. Pia, duara inaweza kuweka yale yaliyo ndani kutoachiliwa.

Duara katika jamii ya Wachina hudhihihirisha umbo la mbingu na dunia na kwa hivyo huashiria umoja wa mbingu na dunia. C.G. Jung alitazama duara kama uchanganuzi wa kikale wa roho na uchanganuzi huu ukiwekwa pamoja na kikale cha mwili duara hueleza uhusiano wa roho na mwili.

Athari ya duara ni kama ya nyota kwa sababu ni ya ulimwengu wote na ufalme wa mbinguni. Ni utambuzi wa kujitazama; ni kuangalia muhula mzima wa wakati, maisha na ulimwengu. Pia huwa na maana ya kiini, mwanzo wa kila kitu, ukamilifu, tumbo la uzazi, kuweka katikati, mapinduzi, pasipo na mwisho na uwezo wa kutembea. Kwa mkabala wa nadharia ya Kikale Kezilahabi anasema,

> *Kabla ya ngoma zote kucheza kwa pamoja, ngoma za aina nne zilikuwa zimeteuliwa kucheza katikati ya duara kwa muda usiozidi nusu saa kwa Kila ngoma. Wengine walitakiwa kutazama tu kwanza. Ngoma hizi zilikuwa ngoma mashuhuri wakati fulani katika mkondo wa historia...(uk103).*

Ngoma zilizochezwa zimetoka sehemu zote ulimwenguni. Ngoma ya kwanza inaongozwa na mwanafalsafa aliyetamka maneno yake kwa kithembe na inachezwa kisayansi. Kikundi cha pili kinaongozwa na mwanasaikolojia aliyekuwa na mawazo ya ajabu. Ngoma ya tatu inaongozwa na mwanamapinduzi anayejiita mtetezi wa wanyonge. Ngoma ya nne ni ya vichaa tupu na imejaa vurumai. Wakati wa

malimboto kiongozi wa kikundi hiki anakanyagwa hadi kufa lakini hakuna mtu anayemjali. Baada ya muda mfupi watu wote wanajikuta wanacheza kwa vurumai. Huo ukawa mwanzo wa vikundi vyote vya ngoma kuanza kupiga ngoma zao na kucheza bila kufuata mpangilio. Msimulizi anasema,

> *Tulijikuta tunasukumwa na nguvu fulani kutoka kwenye kitovu cha duara. Sehemu ya katikati ya duara ikabaki tupu. Mwanga mkali ulijaa ile sehemu ya katikati. Mwanga ulipofifia na kutoweka, tuliona Kizee chenye matege na mkongojo kimesimama katikati* (uk 107).

Maelezo haya yaashiria kwamba kiini cha wanadamu wote ni duara. Wote ni wacheza ngoma. Duara hapa ina ishara ya uhai.

### 3.3.5 ISHARA YA MWANGA

Kulingana na nadharia ya Kikale, mwanga huashiria matumaini, nuru na kufanya upya. Wakati msimulizi anachoka kwa sababu ya kucheza ngoma sana kizee kinaugusa mwili wake na kusema,

> *"Cheza!" ghafla nilipata nguvu za ajabu. Nilijua sasa la kufanya. Nilizunguka Pale katikati kama pia...Nilicheza nikajisahau. Nilianza sasa kuona kizunguzungu. Nilipokaribia kuanguka kizee kilinigusa tena kwa fimbo. Nilipata tena nguvu za ajabu...."Tazama juu!"... Nilicheza nikitazama juu, halafu macho yangu yakafunguka. Niliona mwanga mkali ukishuka machoni Mwangu kutoka juu. Nikajihisi kama kwamba mwili mzima ulikuwa umewekewa damu mpya. Mwanga ulikuwa mkali...*(uk 107-108).

### 3.4 HITIMISHO

Sura hii imejadili matumizi ya ishara kimafumbo katika riwaya ya *Nagona*. Riwaya hii ndiyo sehemu ya kwanza katika mfululizo wa riwaya tatu za Kezilahabi. Uchanganuzi umeonyesha Kezilahabi ametumia ishara mbalimbali kuhuisha na kufikisha ujumbe kuwa mwanadamu hafi lakini anaendelea kuishi katika umbo lingine. Aidha, ishara hizi zimetumika kuwasilisha ujumbe wa mtunzi kwa wasomaji wake.

Sehemu hii imebainisha kwamba kuna aina mbalimbali za ishara zinazojitokeza katika riwaya ya *Nagona* hususan, ishara ya maji, ishara ya msitu, ishara ya duara na ishara ya mwanga. Katika uchanganuzi wetu, tumebainisha dhahiri jinsi matumizi ya ishara na mazingira ya mwandishi yalivyochangia pakubwa katika kuwasilisha maudhui ya uhai na kifo.

Katika kuzihakiki ishara hizi, utafiti umedhihirisha kwamba Kezilahabi anatumia ishara kimafumbo kuendeleza maudhui ya uhai na kifo katika riwaya ya *Nagona*. Hata hivyo kulingana na uhakiki wetu tumegundua kwamba ishara hizi hazijaendeleza msuko wa hadithi kwa sababu zimewasilishwa vipandevipande na hakuna mfululizo wa matukio. Hali kadhalika, tumeonyesha kwamba ishara hizi zimeendeleza maudhui ya mwandishi. Baadhi ya maudhui ambayo yameweza kudhihirika katika riwaya ya *Nagona* ni pamoja na mauaji, usherati, migogoro ya kiuchumi, kutoamini Mungu, fumbo la uhai na kifo miongoni mwa mengine.

Kwa jumla Kezilahabi ametumia ishara katika riwaya ya *Nagona* kwa njia faavu zaidi. Ishara hizi zina nguvu kubwa kwa msomaji na zimeendeleza maudhui ya mtunzi kufikia ukamilifu wake.

Katika sura itakayofuata tutajadili riwaya ya *Mzingile* ikiwa ndiyo sehemu ya pili ya mfululizo huu wa riwaya tatu za Kezilahabi. Tutajadili kwa kina dhana za uhai na kifo na jinsi zimesawiriwa kimafumbo kupitia ishara mbalimbali.

# SURA YA NNE

## MAUDHUI YA UHAI NA KIFO KATIKA RIWAYA YA *MZINGILE*

### 4.0 UTANGULIZI

Katika sura iliyotangulia tumehakiki riwaya ya *Nagona* na hadithi zilizomo kwenye 'hadithi kuu' zikiwa ni pamoja na hadithi ya "Mimi", hadithi ya babu, safari ya "Mimi", matatizo ya ulimwengu, mwanamke na paa wa ajabu, uvumbuzi, ugonjwa wa babu, mjadala wa ungamo na Ngoma Kuu. Aidha, tumeangazia maana ya anwani na fumbo la uhai na kifo. Tumejadili ishara mbalimbali za uhai na kifo zikiwemo ishara ya maji, ishara ya msitu, ishara ya mzee, ishara ya duara na ishara ya mwanga.

Sura hii ya nne imeonyesha jinsi dhana ya uhai na kifo imesawiriwa katika riwaya ya *Mzingile*. Maudhui ya uhai na kifo katika riwaya ya *Mzingile* yamesawiriwa kupitia mhusika Kakulu ambaye ni wahusika wengi ndani ya mmoja. Kakulu amechorwa kama mtoto, mzee, kiongozi, mungu na anapatikana kila mahali hivyo, anaashiria uchangamano, utengano wa kiutu na vilevile kusambaratika kwa utambulisho wa wahusika. Mwandishi ametumia wahusika wengi ili hoja zake ziwe na uzito katika kukuza maudhui ya uhai na kifo. Kusudi la riwaya hii ni kutoa mwanga wa mawazo gizani hivyo, wahusika katika riwaya ya *Mzingile* wanaleta mwanga kwa giza lililokuwa katika riwaya ya *Nagona* kwa hivyo umuhimu wa matukio ya wahusika katika riwaya hii ni kuleta mwanga. Wakati wahusika katika riwaya ya *Nagona* wanaleta giza, wahusika katika riwaya ya *Mzingile* wanaleta mwanga.

Ukosefu wa utambulisho wa wahusika ni sifa moja ya uhalisiamazingaombwe. Mhusika wa aina hii amejitokeza kwa mara ya kwanza katika riwaya ya *Mzingile*. Mwandishi amechanganya wahusika hawa na maisha yake kwa sababu amekuwa

akitatanika sana kuhusu dhana ya uhai na kifo. Dhana za uhai na kifo zinaaathiri maisha ya watu wote ulimwenguni na wanalizimika kuwa nazo na hawawezi kuziepuka.

Utafiti huu umebainisha kuwa mazingira ya mwandishi yamechangia sana katika kuwasilisha maudhui yake. Kama riwaya ya *Nagona*, riwaya ya *Mzingile* ina sitiari ya safari ambayo inakaribiana sana na tukio la kweli katika maisha halisi. Masimulizi katika riwaya ya *Mzingile* yametokana na fasihi simulizi ya Ukerewe ambapo Kezilahabi amezaliwa. *Mzingile* ni sehemu ya pili ya riwaya tatu za mfululizo za Kezilahabi. Kufikia sasa ni sehemu ya kwanza *Nagona* na ya pili *Mzingile* zimechapishwa. Lengo la utafiti huu ni kuchunguza fumbo la uhai na kifo katika riwaya za *Nagona* na *Mzingile*.

Riwaya ya *Mzingile* (1991) inaendeleza motifu ya utafutaji au uchunguzi wa maana ya maisha kupitia ishara ya mwanamke mwemye utelezi, ishara ambayo imeazimwa kutoka kwa Friedrich Nietzsche. Kuna kisasili cha Kakulu ambacho kinaonyesha vipawa vyake vya kipekee ambavyo vinawafanya wanakijiji wampende. Umbo na uhodari wake unaowashinda wote ni sifa inayohusishwa na fasihi simulizi ya tendi za kishujaa. Riwaya ya *Mzingile* ina tendi kadhaa kama vile utendi wa kutoka na kuanza safari kwa Kakulu hadi katika upweke wa milima. Hii ni motifu inayopatikana kote ulimwenguni katika tendi za fashi simulizi kutoka kwa *Fumo liyongo* hadi kwa Anglo-Saxon *Beowulf, tendi ya Gilgamesh* kutoka Sumeria na ya *Ramayana* na *Mahabharata* kutoka India. Kakulu ni mfano halisi wa motifu ya ukombozi inayohusishwa na nguli wa tendi. Taswira za mawazo yenye nguvu ya kufichua kichefuchefu na kuchukiza katika riwaya ya *Mzingile* zinakumbusha riwaya ya Armah

*Why Are We So Blest?* Riwaya ya *Mzingile* imetoa taswira ya ulimwengu uliojaa unafiki, mapinduzi, machafuko, maumivu na uchungu.

Riwaya ya *Mzingile* inaeleza matukio baada ya *Ngoma Kuu*. Msichana anayezaliwa siku hiyo anakuwa mkombozi wa pili aliyekuwa anangojewa sana lakini juhudi zake za kuukomboa ulimwengu zilizohuishwa zinaambulia patupu na anauawa. Mtangulizi wake ambaye ndiye "*Mimi*" anatakiwa kumtafuta baba yake msichana huyu ili ahudhurie mazishi. "Mimi" anapata kujua kuwa babake msichana bado ni kile *kizee chenye fimbo*. Wakati huu ni mzee asiyekuwa na nguvu anayengojea kufa. Mzee anakataa kutoka kwenye kibanda chake kilimani na kwa hivyo "Mimi" anarudi peke yake katika ulimwengu wa watu halisi na anatambua kuwa wakati alipokuwa ameenda ulimwengu ulitawaliwa na serikali ilioleta maafa ya nyuklia.

Riwaya ya *Mzingile* ni mchanganyiko wa mambo mbalimbali yanayoelezwa kupitia hadithi ya safari inayopinda ya mhusika *Mimi*. Ametumwa kumpelekea ujumbe *mzee* ambaye ni baba yake mkombozi wa pili aliyekufa ili aweze kuhudhuria mazishi. Safari hii ya *Mimi* inasawiri utafutaji na uchunguzi wa maana ya maisha. *Mimi* anampata *mzee* juu ya kilima katika kibanda chake na anazungumza naye lakini, *Mimi* anarudi kabla ya kumsadiki *mzee* amfuate. Safari ya kurudi inakuwa safari ya kutafuta majibu ya maswali ambayo kwa kawaida hayaulizwi.

Anaporudi kwao, "*Mimi*" anatambua kuwa karne kadhaa zimepita na kuna kukata tamaa duniani kwa sababu ya ajali ya nyuklia. Kwa mshangao, "*Mimi*" anapata *mzee* katika mabaki ya nyumba yake na mazungumzo yao yanaendelea. Anamtunza huyu mzee lakini anachoshwa naye na hawezi kumwacha peke yake. Baada ya muda mfupi mvua inaanza kunyesha na mazingira yanaanza kurudi polepole. Wakati huu

*mwanamke* wa ajabu anatokea, anamchukua "*Mimi*" na kumwongoza hadi mahali kama paradiso. *Mzee* anabaki peke yake na baada ya muda anatoweka.

"*Mimi*" na mwanamke wanabaki wakiwa wawili pekee na wanaanzisha ulimwengu mpya. Wanaelewa makosa yaliyofanywa hapo awali na ili kuepuka makosa hayo tena, wanaanza kujenga dunia mpya. Sehemu nyingi katika riwaya hii zinahusu mambo ya hapo zamani. Kezilahabi amefafanua mambo yaliyomo katika ulimwengu wa awali na ni sura chache tu pale mwisho zinazoonyesha mabadiliko, maendeleo na mawazo yanayoleta ulimwengu mpya. Sio rahisi kujua wakati ulimwengu mpya unaanza kwa sababu elementi za dunia ya awali na za dunia mpya zinaonekana kuchanganyika wakati wa mabadiliko

Kezilahabi anatuasa kwamba maisha ni kama mkufu, unachukua kipande hiki na kukiunganisha na kingine, kile kisichokufaa kitupe kitamfaa mwingine. Kezilahabi hatoi wazo tu la safari inayopinda lakini utungo huu una maudhui mengi yakiwemo maudhui ya uhai na kifo uhai na kifo.

## 4.1 UHAKIKI WA RIWAYA YA *MZINGILE*

### 4.1.1 KAKULU

Ukweli wa Kakulu unazingirwa na ukungu na kisasili. Kuwako kwake ni kama mzaha na kuzaliwa kwake pia ni kwa ajabu. Anaongea bado akiwa tumboni mwa mamake na anaingilia kati mazungumzo ya wanawake na hata kuwajibu. Anaitwa mtoto wa mchawi hata kabla ya kuzaliwa. Mkunga anapoitwa kuja kumhudumia mamake anastaajabu kuona kichwa cha mtoto kina ndevu nyingi ndefu zenye kuchanganyika na mvi. Mkunga anamwambia mama kuwa amezaa shetani naye

mama anaanza kukimbia huku amepanua miguu na anamzalia nje kwenye shina la mti. Wakati Kakulu anapondondoka chini anakata kitovu kwa meno yake, anajipangusapangusa yale maji ya utelezi na kuwakaripia wazee wanaokuwa karibu. Anawaambia, "*Ondokeni hapa! Mnachunguliachungulia nini! Hampaswi kuona mwanzo wangu na njia nilioijia*!"( uk 2).

Wanakijiji wanampa jina la Kakulu kakubwa kazee kwa sababu amezaliwa akiwa na ndevu. Habari zinavuma kwa sababu hajanyonya ziwa la mamake lakini siku hiyo hiyo anapozaliwa anamwomba mamake ubuyu ulioivia mtini. Mama anapomwambia kuwa hawezi kupanda ule mti anaitisha kigoda chake na anaarifiwa kuwa kiko cha marehemu babake. Kakulu anasema huu ni uzushi na anamwambia mamake kuwa kabla ya mti uliotengeneza kigoda hicho kuwako yeye alikuweko. Mamake anashangaa na Kakulu anawaambia wanawake waliokuwa pale kuwa ulimwengu huu haukusikia la mkuu. Anawafukuza kwani anasema wanatafuta umbea. Wanasambaa wakicheka na pia Kakulu anacheka na cha kushangaza ni kuwa meno yamemjaa mdomoni. Mamake anapoona hivi, anaingia kwa nyumba na kutoroka kupitia mlango wa nyuma. Anapogeuka nyuma anakaona kamepanda mbuyu kakila ubuyu na kanampigia kelele arudi lakini hakurudi na hakuonekana tena. Kakulu anatunza migomba inayoachwa na mama yake, analima na anaishi kwa kujitegemea. Anatembelea jirani zake na kuwaamsha asubuhi.

Katika mikutano Kakulu anawashangaza wengi kwa sababu ya ujuzi wake kuhusu historia iliyopita , mila na desturi. Mara nyingi anauliza maswali yanayowashida kujibu. Kwa sababu ya mazao yake mazuri panatokea uvumi kuwa ana mkono wa

bahati. Anapopanda mbegu inazaa sana na watu wengi wanamwomba awapandie mazao ya kila aina . Anawashauri jinsi ya kulima na wengi wanapata mavuno mazuri.

Kakulu ni mfupi na ni wa futi tatu na nusu hivi ingawa kimawazo amepevuka. Ni kipenzi cha wengi lakini kwa sababu ya mizaha yake haheshimiwi kijijini. Mapadri, masista, wavaa buibui na masheikh wanakaogopa kwa sababu kanazoea kufunua makanzu yao na kuingia miguuni mwao na ni wao tu wanaojua kanachowafanyia. Wenye mabinti wanamtania kwa sababu hajaoa na Kakulu anakuwa na wachumba wengi kijijini. Kwa sababu ya sifa zake za kupiga myeleka anamtia mimba binti mmoja bado akiwa ndani. Pia, ni mcheza hodari wa mariba, zeze na chombo cha nanga. Ana mazoea ya kuzunguka vilabuni akiwapigia walevi vyombo hivi na alipewa pombe ya bure na kuzawadiwa pesa. Wakati anapiga muziki anaimba kwa Kiswahili, Kirusi, Kiarabu, Kiingereza, Kifaransa na lugha zingine ambazo hazieleweki. Watu wanafikiria ni utani hadi anapofika mzungu siku moja na Kakulu anazungumza naye lugha ya kwao. Wanakijiji wanamwamini na uvumi unaenea kuwa yeye pia ni mwanasanaa. Anajenga nyumba yake ndogo kilimani, anachonga vinyago, anasuka mikeka na anawasuka nywele wanawake. Watu wanaanza kuiga ufundi wake na polepole anapata heshima. Kama si kukosa mke angeteulliwa kushika nyadhifa mbalimbali.

Anapokuwa mzee heshima inamjia katika utukufu wake na anajulikana kama mganga. Watu wanaenda kwake kuomba ushauri. Anawafukuza nzi kwa usinga wa pundamilia na anakaza macho yake kwa kitu kinachoelekea kuwa mbali. Anaponya kila magonjwa na wanakijiji wanamtengenezea fimbo ndefu ya kutembelea. Panapotokea ukame, wanakijiji wanamwendea ili awasaidie kuleta mvua. Anawaambia waanze

Kenyatta University
Kiswahili Resource Centre

kuandaa mashamba kwani mvua ingeanza baada ya wiki moja. Kakulu akawa mleta mvua na mali kwa sababu mwaka huu mavuno ni mengi. Anajulikana kama mtoaji wa vyote.

Mzee Kakulu anawateua wazee watano kutoka kila kijiji na anaenda nao msituni. Anakaa nao kwa muda wa mwezi mmoja akiwafunza historia, mila na desturi, dawa, unajimu na mengine mengi. Anapoona wazee wamekomaa anawaongoza hadi chini ya mlima mkubwa na wanapanda hadi kileleni. Kwa mara ya kwanza, wazee wanaona nyumba yake ndogo. Wakiwa juu ya mlima anawaonyesha kwa fimbo yake nchi iliyo chini na kuwaambia kuwa nchi hiyo yote ni yao na wasikubali ichukuliwe na wageni. Anawaambia sasa waondoke na wafundishe watu aliyowafundisha. Kakulu anabaki akiwasha moto unaomlika dunia nzima. Anakaa pale milele na wazee wanashuka chini kutekeleza yaliyoagizwa na Kakulu.

Baada ya siku tatu mlima unaanza kutoa ndimi za moto mkubwa unaomulika vijiji vyote vitano vilivyo chini yake. Watu wanaanza kutoa maombi yao kwa Kakulu. Siku moja mlima unachachamaa na unatoa moto mwingi. Mwingine unafurika toka juu hadi chini kama tope zito la moto na watu wengi wanaungua na kufa. Watu wanamwomba Kakulu usiku na mchana atulize hasira yake kwa waliomcheka na kumdharau. Pia, wanafanya jitihada za kumweleza Kakulu kama mtu mnene na mrefu mwenye ndevu nyingi na kipara kidogo karibu na paji la uso.

Wazee wanaanza kutoa sadaka chini ya mibuyu na pia kuchuma ubuyu na kumpelekea Kakulu chini ya mlima. Mvua inaanza kunyesha kwa wingi na moto unazima na arthi inapoa. Baada ya miaka kadhaa arthi hii inakuwa na rutuba sana na

mazao yanakawa mazuri na mengi. Wanaamini kuwa wao ndio wana wateule wa Kakulu. Ustaarabu unapoingia wanajenga majumba makubwa na ya kupendeza na kumtolea Kakulu sadaka na maombi humu ndani. Hatimaye, Kakulu anakuwa kisasili na anakuwa mwanzilishi wa taifa, pia anakuwa kweli na kweli hii inaenea ulimwengu mzima. Msimulizi anasema ingawa alikuwa nusu macho, nusu usingizini bado anakikumbuka kisa chote cha siku hii.

### 4.1.2 SAFARI YA MSIMULIZI

Kichaa anapiga kelele na kusema ulimwengu unahitaji mwanga. Naye msimulizi anataka kujua asili ya mwanga na anatazama sayari, nyota na mwezi zinavyozunguka. Kutokana na jinsi sayari ziko mbioni kulizunguka jua na dunia inavyojiviringisha yenyewe kwenye mhimili wake, msimulizi anafikiria binadamu ana mhimili wake mwenyewe pia. Katika mhimili wake mwanadamu yuko mbioni kulizunguka jua lake lisiloonekana. Msimulizi ana hisia kuwa mhimili huu uko karibu kuporomoka kutokana na ukame wa muda mrefu. Ukame huu ni wa wema, imani, upendo na wa fikra. Kuna wingi wa uchoyo, kiburi, uonevu, ubinafsi, ubarakala na maasi. Hali ya wasiwasi inatawala mahali uhakika wa uhai ulikuweko. Watu wanahitaji mtu wa kuwaambia kwamba hawatakwisha, Kuwahakikishia kwamba wataishi milele na kwamba amani ya kudumu itapatikana.

Anayepatikana ni mwanamke na wengi wanaamini kuwa vilio vyao vimesikika lakini haishi na wao kwa muda mrefu kwa sababu ya akili ya mwanadamu ya kuwa na shauku. Msimulizi anasikia sauti inayomwamuru aamke kwani wamemuua na ni yeye tumaini la mwisho la heshima na utu wa binadamu. Sauti inaendelea kusema kwamba

kama hawezi kufika atoe ruhusa wamzike. Msimulizi yu nusu macho na nusu usingizini na anaamka.

Anapoamka anafikiria juu ya safari ndefu inayomkabili. Hii si mara yake ya kwanza kwenda kutoa taarifa ya kilio kwa jamaa ya marehemu lakini wakati huu kilio ni cha aina yake na vivyo hivyo ndugu na jamaa wa marehemu ni wa aina yake. Katika kifo chake mlikuwa na sitiari ya matamanio na matumaini yao. Upande wa pili jamaa zake walifunikwa na wingu nzito la fumbo. Sauti inasikika tena safari hii kwa uwazi zaidi kidogo.

Mzee mara nyingi huwa amelala lakini wakati huu anamwambia msimulizi asukume mlango kwa nguvu zake zote maana haujapata kufunguliwa na nyumba yenyewe haina dirisha. Dhamiri ya msimulizi inatoa jibu kuwa maisha ya mwanadamu ni kama mkufu. Binadamu huchukua kipande hiki na kile na kukiunganisha. Anaarifiwa kuwa siku ya kufa atavishwa shingoni mkufu wake na anaonywa asitegemee kuokota mkufu uliokamilishwa. Ni lazima asafiri ili atafute vipande hivyo vingine.

Safari ya msimulizi inaanza asubuhi mapema kabla ya fikra kuchoka. Hajui aelekee upande gani kwa sababu hakuna anayejua mzee anapoishi lakini anafuata silika zake. Anatembea kuelekea sehemu zenye milima na mabonde na anazungumza tu na dhamiri yake. Sio rahisi kupanda na kuivuka milima inayojulikana tu katika historia na imeficha kinachopatikana upande wa pili. Mabonde yana maporomoko makali yanayojulikana kwa uwezo wake wa kudumaza fikra zisijikwamue lakini msimulizi anasukumwa mbele na utashi. Anavuka milima, mito, na mawe hadi mahali tambarare. Anapoachana na milima anafika mahali panapokuwa na njia tatu. Moja

inaelekea kushoto ambako anaona vichaka vidovidogo vikavu na nyayo za mtu ambaye alipita kitambo maana hakuweza kumwona. Mkono wa kulia anaona njia inayoelekea kutopitiwa na watu wa karne hii na ina majani yaliyoota hadi katikati. Njia ya tatu imezibwa kwa miiba lakini inaonekana kuwa wazi na haipindapindi kama zile zingine mbili. Anasimama kwa muda akifikiri njia ya kupita na anapotazama zile nyayo za njia ya kwanza anaona mwanamke ambaye amekuwa akimtazama kwa muda huu wote. Anapomwona anatembea mbele polepole na anatoweka machoni. Kimbunga kinatokea upande wa njia inayokuwa na miiba na kinavuma kwa kasi kuelekea anakosimama. Anajaribu kuyaficha macho yake lakini vumbi linamwingia machoni. Kivumbi kinapotulia anapekecha macho yake na kutazama mbele. Anamwona ndege mweupe akirukaruka nyuma ya miiba hiyo na moyo wa ujasiri, udadisi na utundu unamsukuma mbele. Anataka kujua nini kilicho nyuma ya miiba hiyo na anakata shauri kuifuata hii njia. Anapomkaribia anaruka mbele zaidi na kumwomgoza njia, naye anasukumwa mbele na wazo la kumkaribia na kuangalia uzuri wake kwa makini. Mwishowe, anafika bondeni panapokuwa na mto na ndege anajitumbukiza majini, anajibaraguza mbawa na kutoka harakaharaka. Ndege anafanya hivi mara kadhaa na anapomkaribia anaruka upande mwingine wa mti akawa anapekuapekua minyoo matopeni.

Msimulizi anapata wazo la kuoga. Anaoga polepole kwani hajui umbali wa anakoeleka na hajui atafika lini. Anajitumbukiza majini halafu anatoka na kujisugua kwa mchanga mwororo. Anapomaliza anapata nguvu mpya na anapotoka majini anafurahia mwanga wa jua ambao hapo awali ulikuwa unamkaanga. Analala chini ya mti akiwa uchi wa mnyama na usingizi unamchukua. Anaamka kama saa kumi macho yake yakiwa mazito. Katika jitihada za kutaka kuona anaona mwanamke karibu naye

akimtazama na anasitiri sehemu za mwili wake. Mwanamke amevaa khanga tatu, moja amefunga kuanzia kifuani na nyingine kiunoni na zote zinafanana na kichwa chake kinatanda khanga yenye rangi tofauti. Msimulizi anapomtazama machoni anatabasamu. Bila kusema neno mwanamke anaelekea mtoni na kuvuka upande wa pili. Anachukua kibuyu kikubwa cha maji na kukiweka kichwani. Anamgeukia na kumwonyesha njia kwa mkono wake wa kulia bila kusema neno.Wote wanafuata njia moja.

Upande wa pili umejaa mchanga na ni jangwa. Msimulizi anamfuata mwanamke kwa shauku kubwa akiwa na matumaini ya kumkaribia na kuzungumza naye. Mwendo wa mwanamke haukuwa wa pole na kwa sababu msimulizi hana ufundi wa kutembea mchangani, umbali kati yake na mwanamke unazidi kuongezeka.

Mbele kilima chenye mchanga kinaanzaa kuonekana na mwanamke ameanza kukipanda na msimulizi anaanza kukipanda baada ya muda mfupi. Mwanamke anapofika juu ya kilima anageuka na kumtazama halafu anaanza kushuka chini na kupotelea upande mwingine wa kilima. Msimulizi anajaribu kukimbia ili apunguze umbali kati yao lakini anapofika kileleni mwanamke haonekani tena. Anafuata nyayo zake.

Jua linapotua msimulizi anakuwa ameshuka chini bondeni. Giza linapoingia nyayo za mwanamke hazionekani tena. Anatafuta mahali pa kulala na akiwa usingizini anaota mtu akimsemesha. Mtu huyu amefunikwa na hali ya mawinguwingu au labda ukungu na kwa hivyo msimulizi hatambui. Huyu mtu anamtazama bila kusema neno kwa muda. Msimulizi anajaribu kuinua kichwa chake lakini ni kizito, anajaribu kupiga

kelele lakini kinyua chake kinakataa kufunguka na ulimi ni mkavu. Yule mtu anamnyooshea mikono miwili lakini msimulizi anapojaribu kusimama anashindwa. Anamwambia kuwa baada ya mto hakuna kitu kingine isipokuwa kina cha fikra safi katika upweke. Anaangalia jinsi anavyohangaika bila nguvu za kuinuka.

Asubuhi anapoamka anakumbuka ndoto hiyo pekee na kisa cha yeye kuwa hapa. Anapoangalia alipolaza kichwa chake usiku anaona khanga iliyokuwa imekunjwa vizuri kama mto mdogo. Msimulizi anakumbuka hiyo ndiyo khanga mwanamke alikuwa ametanda kichwani. Pia karibu naye anaona kibuyu kikubwa ambacho kina maji. Anakunywa maji haya kwa hamu kubwa na pia anasafisha uso wake na kusukutua mdomo. Anapotazama huku na huku anaona mwili wa mwanamke anayelala chali akiwa uchi. Anamrukia na kukumbatia huku akimpapasa na kumweleza jinsi anavyompenda na amemtafuta kwa karne nyingi.

Anaporuka ili amshika anaangukia mchanga uliokuwa kama tuta na hashiki chochote isipokuwa mchanga. Anajipangusapangusa na kusukuta kinywa chake kwa maji. Anapokuwa tayari kuondoka anaweka khanga begani na kuangalia nyayo zilizomfikisha pale lakini zilikuwa zimefifia kwa sababu ya kufunikwa na mchanga uliosukumwa na upepo usiku. Anapotazama zinakoelekea anaona yule mwanamke kwa mbali amekaa mchangani akimtazama. Anasimama na kwa mkono wake wa kushoto anamwashiria amfuate. Anapopiga hatua mbili tatu hivi, anageuka na kuanza safari. Anaongoza na msimulizi anamfuata huku amebeba kibuyu cha maji. Mchanga unaendelea kuyarudisha nyuma mategemeo yake lakini matamanio yalimsukuma mbele pamoja na utashi uliokuwa katika kitovu cha nafsi yake.

Inapofika saa sita hivi za mchana wanaanza kuingia kwenye arthi yenye changarawe. Msimulizi anakaa chini kupumzika na yule mwanamke anasimama, anatazama nyuma na anapoona amekaa pia yeye anakaa. Msimulizi anapopata nguvu mpya wanaanza safari. Msimulizi anatambua kuwa wanafuata njia nyembamba inayopindapinda. Anapomwita mwanamke anasimama na kwa mkono wake wa kushoto anamwonyesha mlima mkubwa uliokuwa mbele yao. Anaanza kukimbia kwa mwendo wa pole na anapotelea nyuma ya jiwe kubwa. Msimulizi anapofika nyuma ya jiwe hili haoni mtu isipokuwa mjusi mwekundu anayetingisha kichwa chake kisha anaingia kwenye ufa. Anazunguka jiwe hili lakini hamwoni mjusi. Anapumzika na anapopata nguvu anaanza safari kuelekea kwenye mlima mkubwa. Upepo mkali unavuma ghafla na kupeperusha khanga juu juu hadi ikapotea machoni mwake na kutua mbali msituni.

Mlima unakuwa mgumu kupanda na sehemu ya chini ni msitu ulioshonana na anajipenyeza pasipokuwa na mwanya. Baada ya msitu huu anafika sehemu inayokuwa na miamba mikubwa na upandaji wake unakuwa mgumu na anachukua karne nyingi kuvuka sehemu hii. Anapomaliza hii sehemu anakaribia kileleni na anaweza kuona kitu kama nyumba. Nyumba ilikuwa imejengwa juu ya mwamba mkubwa na mwamba huu ulikuwa juu ya mawe makubwa na inakuwa vigumu kuufikia. Ni kichaa pekee angeweza kujenga mahali pale na sio mtu wa akili timamu. Ni vigumu kujua anayelala au kukaa huko hupanda na kushuka vipi. Nyumba haionyesha kuwa na dirisha na mlango haufunguliwi. Asubuhi anaanza jitihada za kujaribu kufika kwenye kilele. Anaenda kwa magoti kuifikia ile nyumba, yanakwaruzika na damu kidogo inatoka. Anapumzika mlangoni akijua kuwa yeyote yule angeufungua ule mlango angelazimika kumwamsha.

Hakuna anayeufungua na siku moja asubuhi anaanza kugonga mlango wa nyumba hiyo. Anagonga kwa siku mbili hadi vidole vinaanza kuuma lakini hakupata jibu na jina la mwenye nyumba hakulijua. Anakumbuka neno "*mzee.*" na anaanza kugonga hali akiita mzee lakini hakuna jibu linalotoka ndani. Anapochoka, analala usingizi na anapoamka anapata bado kuna giza. Usingizi unaisha na hali ya giza inakuwa ya kutisha na bado anaendelea kugonga bila kukata tamaa. Mwishowe mlango unaanza kulegea na ulegevu wake unamtia moyo. Anaandaa nguvu zake zote na kama kondoo dume anakimbia na kuugonga mlango kwa bega na anaanguka ndani kwa kishindo.

Sauti kutoka humo ndani inataka kujua ni nani huyu ambaye ameingia. Msimulizi anasikia mlio wa kitanda kama wa mtu anyanyukae na kujinyoosha. Sauti inasema kila kitu kimevurugika kwa sababu ndoto zake zimeharibiwa. Anaagizwa kuingia ndani na anaambiwa kuwa hakutarajiwa wakati huo. Taa inayotoa mwanga hafifu inawaka na kati yake na yeye pana pazia la gunia kuukuu linalofanya nyumba igawanyike mara mbili. Nyuma ya gunia hili anaona kiwiliwili cha mtu anayejaribu kujifunga blanketi kiunoni. Sauti inamwarifu kuwa imesahau mambo mengi na bado wanaendelea kumfuata. Haitaki kuhusishwa na mambo na ghasia zilizotokea.
Anainuka polepole kutoka kitandani na kulisukuma gunia kwa mkono mmoja. Anapomkaribia anaweka taa juu ya meza na kuchukua fimbo iliyokuwa juu ya meza hiyo. Kwa miguu inayotetemeka na mgongo ulioinama, anatembea hatua chache kuelekea kwa msimulizi. Anapomkaribia, anatazama kila pahali kwa makini, anachezesha masikio yake kama ng'ombe na kumwongoza aketi kwenye kochi moja kuukuu ambalo limetatuka. Anamwarifu kuwa sio kosa lake kuvunja mlango kwani ilibidi iwe hivyo. Anaendelea kumwarifu kuwa kwa karne nyingi watu wamesita kuingia humu kwa nguvu. Anaketi katika kochi la pili na kupandisha utambi wa taa.

Anaagizwa arudishe mlango ili wapate joto. Anaanza kwa kumuuliza ama ametumwa kwenda kumhoji na anaendelea kusema kuwa amekwishawaambia amesahau mambo mengi na hafahamu sababu za kuendelea kumghasi. Msimulizi anamwambia kuwa ametumwa kwenda kumwarifu kuhusu kifo cha mwanawe ambaye amekufa lakini mzee anasema hakumbuki kuwa na mtoto na anakubali tu. Anataka kujua sababu ya kuuawa kwake na anaarifiwa kuwa alidai kuwa na uwezo wa kila aina na kuna uwezekano wa kuishi milele. Watu walimwita mwongo na alivuka mpaka alipojiita mwanaye na kupoteza uaminifu aliokuwa nao miongoni mwa watu. Aliuawa alipoamsha fikra za wanawake kuhusu usawa. Anaendelea kumwambia kuwa watu wanaomba kumzika kama hawezi kuhudhuria mazishi naye mzee anamwambia kuwa ni wajibu wa kila anayekufa kuzikwa. Msimulizi anapotaka kujua ni jambo lipi lingine atawaambia watu anaambiwa kuwa mzee anatumia muda wake mwingi katika kuota ndoto halisi kuliko uhalisia wa maisha. Anaambiwa awakumbushe kuwa kila kitu kimo kitabuni.

Msimulizi anapoamka kuondoka anaitwa na kuambiwa kuwa hatafika mbali gizani kwani yeye ni mtoto wa mwanga. Anapoketi anaambiwa awaambie kuwa mzee anaelea katika amani ya vurumai kwa sababu hataki kuhusishwa na muundo uliokuwepo. Anaendelea kusema kuwa kitovu cha duara kimevunjwavunjwa na sasa ni shimo kubwa na hakuna awezaye kusimama hapo. Pia, anasema alipokuwa kijana alipiga myeleka hodari na alishikilia kitovu cha duara kwa karne na karne hadi siku moja kichaa alipowaambia washindani wake siri ya kivuli chake. Kivuli kilipopigwa kwa fimbo, nguvu zilimwishia na akaanza kuwa mzee kadri wakati ulivyopita. Anakubuka sifa za ujana wake na watu walimpa sifa ya *omnipotentia,* wengine

*omniscentia* na sifa zake zote zilianza na *omni*. Jina lake bado limezungukwa na uajabuajabu. Wasichana walimpenda lakini alikuwa na uchu wa mabikira.

Kwa sababu alikuwa na tuhuma ya kusalitiwa alijenga nyumba hii ili kujikinga na ghadhabu ya wale wangetaka kujilipizia kisasi wakati hana nguvu. Aliijenga kwa utulivu, makini, akili na maarifa. Anaendelea kusema sasa wote wanaendelea kumtania lakini kila siku wanasali na kutaka mategemeo yao yatimizwe. Anasema wanafanya mzaha lakini maisha yenyewe ni mzaha. Anamwambia msimulizi kwamba kama anaogopa kufa akae kimya arejeapo na akumbuke kuwa ujasiri wa mja hukamilishwa na kifo. Kimya kinafuata na msimulizi anaanza tena mazungumzo na kuuliza mzee ama haoni upweke kwa kuishi peke yake lakini anamwarifu kuwa muda wake mwingi huutumia usingizini kwa kuota ndoto. Anasema kisanaa alitaka nyumba yake iwe mfano mwema wa ujenzi, na kiusalama alitaka iwe ngome ngumu itakayoweza kuhimili mashambulizi ya kila aina kwa karne nyingi.

Msimulizi anamwarifu kuwa nyumba kama hii ikionekana itafikiriwa ya kichaa na itavunja heshima ya wananchi. Mzee anaarifiwa kuwa siku hizi kuna nyumba za kisasa zinazojengwa kwa mwezi au miezi miwili na wajenzi hutumia mashine. Anaarifiwa kuwa hii ni mitambo ya kisayansi inayofanya kazi usiku na mchana Wametengeneza mabomu yanayoweza kuharibu miundo ya mzee kwa dakika. Mzee anastaajabu kwa sababu hapo zamani ilikuwa mwiko kuvunja miundo yake ili kujaribu kujua undani wake. Anahofia kivuli chake kama kinafika huko na kupigwa kila siku kwani nguvu zake zinaisha kila siku, anazeeka haraka na amekuwa msahaulifu. Anahofia kuwa ule uajabuajabu uliozunguka jina lake umekwisha na isiwe moto aliofukia chini arthini wameufukua. Anamwambia msimulizi wasiwe

wamefukua alichokuwa amefukia kukinga uhai wake. Anamwambia aende awaambie kuwa wasahau ujana wake na wasichanganye kuwako kwao na kwake na waishi kwa utashi ulioamshwa na nguvu za *Lumen natural* zitakazowaongoza vizuri kuliko ndoto zake. Anauliza wanasiasa siku hizi huimba nyimbo gani na msimulizi anamwambia kuwa karne iliyopita kumezuka ujamaa na usoshalisti unaoleta usawa wa binadamu. Mzee anashtuka anaposikia sifa yake ya mgawaji wa vyote pia imepotea na watu wanatunga maneno kama matabaka ambayo hayamo katika kamusi lake. Anamwambia kuwa wao wote ni wanyonyaji.

Anapoulizwa ama atahudhuria mazishi anajibu kwa sauti ya kuogofya kuwa amekwisha sema na hataki kujihusisha na muundo wa ulimwengu. Anainuka na kumwonyesha mlango wa kutokea na kumwambia atoke nje ya fikra zake. Anachezesha masikio yake kisha anatabasamu, anaweka fimbo chini na kufumba macho yake bila kuzima taa.

### 4.1.3 KICHAA

Alitaka kuwa kichaa daima lakini akili zilimkataza. Alitamani sana kuogelea katika bahari ya nusu urazini, kati ya kuwa na kutokuwako, kati ya ndoto na hali halisi na kati ya uhuru na ufungwa. Daima alitaka kuwa asili ya kicheko cha furaha, uchungu, huruma, ukatili, hofu na ujasiri. Daima alitafuta kazi ya kubweka usiku mmoja mrefu wenye karne nyingi wakati wenye akili timamu wanalala usingizi. Alitamani kutazamwa na watu kwa wasiwasi wasiwezi kutabiri vitendo vyake. Alitaka uhuru wake, uhuru wa kuwa katika kutokuwako.

Anaendelea kuishi akihisi kuwa alichotamani kinatamaniwa na wengi lakini hawana ujasiri wa kutamka hadharani. Walimcheka hasa jirani yake alipotamka kuwa anataka

kuwa kichaa. Kwa sauti ya kutisha anasema anaweza kumla mtu mzima mzima na wote wanakaa kimya.

Siku chache baadaye anajiona akishuka ngazi kuelekea mahali alipofiri palikuwa na chemchemi. Mbele yake palikuwa na mwanamke aliyekuwa na debe tupu. Watu wanaongezeka kadri wanavyoshuka ngazi na taa za umeme zinamulika njia.Wanapofika chini wanakuta uwanja mkubwa uliojaa watu wa kila jinsia. Wanavua nguo na kuanza kuoga kwa maji yanayotoka juu kama mvua na kupiga kelele "*Wokovu!*" (uk31). Ghafla wakajiona bila vidole na wote wanakuwa mifupa inayosimama na watembea lakini wanaogopana. Anakimbia na anapofika kwenye ngazi, anaona kitabu kikindondoka chini, anakiokota na kukimbia nacho. Anaona watu wanaotoa michirizi ya machozi wamemzunguka. Kuna shimo karibu naye na watu wanashikilia mchanga viganjani wakimtazama kwa mshangao mkubwa. Anajaribu kukimbia lakini hawezi.

Baada ya siku hiyo anafanyiwa makafara na kuletewa waganga wa kila aina. Wengi wanaamini kuwa tangu siku hiyo akili zake sio sawa. Wanasema alipoteza kitabu na kama adhabu amekuwa kichaa. Tangu siku hiyo anaitwa kichaa na hana manung'uniko. Huu ni utashi wake tangu awali. Anawasikia watu wakimcheka lakini yeye anaona ni vizuri kuwa kichaa wa kuogopwa. Wakati mwingine anawavulia nguo na kuwakenulia meno hali macho yake yakiwa mekundu. Wengine huogopa, baadhi wanacheka na wengi humwonea huruma. Msimulizi hataki kuonewa huruma kwa sababu hivyo ndivyo alivyo, naye ni kiumbe kikamilifu kama wao.

Yeye hukumbuka kisa chake mara kwa mara siku ya Ijumaa Kuu. Anakumbuka siku moja alipopita karibu na kanisa akitoka msituni kujisaidia. Aliona dirisha limefunguliwa na akajitumbukiza ndani. Akaona msalaba mmoja karibu na altare na akatamani kufa kifo jasiri kama cha huyu jamaa. Huyu jamaa alijenga msingi wa historia mpya na akajiuliza kama yeye angeweza kuinjega historia. Akasimama mbele ya mti mkubwa na kunyoosha mikono yake kama mtu aliyesulubiwa na ikaanza kuuma. Ghafla akasikia mlango unafunguliwa na masista ambao walibeba maua mikononi wakaingiai. Alijificha lakini kwa sababu ya wasiwasi na joto ubongo wake ukaanza kufurukuta. Masista walipokaribia altare akapiga chafya. Masista wakaogopa na maua yakawandondoka. Kwa sauti alipiga kelele "*Eli, Eli, Lama Sabachtani*?"(uk 33). Masista walikimbia kuelekea mlangoni na walipotoweka akachukua maua na kuyaweka chini ya msalaba. Akatoweka kupitia lile dirisha.

Siku hiyo mchana alisikia mtangazaji wa habari akitangaza kuwa Yesu ametokea watu wanne kanisani na anaulilia ulimwengu. Taarifa ikaendelea kusema kuwa kulikuwa na nyayo zilizoachwa na kuwa Yesu huyo ni mweusi. Kanisa hilo lilibomolewa na sasa kanisa kubwa zaidi la makumbusho limejengwa. Maelfu ya wagonjwa hufika hapa kuubusu msalaba na wengine wamepona. Padri wa kanisa hili amemshauri mara nyingi akaubusu ili apone kichaa chake. Sasa anaanza kuamini kuwa historia hujengwa na vichaa wazushao imani na itikadi.

Anaposikia watu wakija karibu na kibanda chake anawatisha kwa kusema, vunjeni makanisa na misikiti yote na kuanza misingi mipya. Misingi mibovu itavunjwa na kichaa, kipofu, mwotaji na mwanamke na wao ndio watakaowavusha walimwengu katika mabonde, mito na milima na mbele ya utashi hakuna lisilowezekana.

Anawaeleza kuhusu kisa cha jirani yake mwotaji na aliyedai kuwa nabii. Mkewe alifariki mwaka jana. Huyu jirani ni baadhi ya wachache wawezao kuzama katika urazini na kuweka misingi mipya ambayo haikutarajiwa. Wako katika ulimwengu wao huru na wanaishi katika ng'ambo ya pili.

Siku moja msimulizi anaamka asubuhi, wakati ndoto zianzapo polepole kurudia uhalisia. Anapiga kelele na kusema wamemuua na hakuna tena matumaini. Anaendelea kusema kama hawezi kufika siku hiyo atoe ruhusa azikwe. Jirani yake akiwa katika hali ya nusu ndoto anayasikia maneno haya. Anaamka na kuanza safari bila ya kumuaga baba yake mgonjwa. Anasukumwa na nguvu fulani maana mwendo wake sio wa kawaida. Hatua zake ni ndefundefu, hajikwai, na anaelekea kuwa na nia na utashi. Msimulizi anamfuata na anamsikia akigunaguna na ni kama anazungumza na dhamiri yake. Anapofika bondeni kwenye mto anavuka kwa uangalifu. Anamtazama hadi anatoweka na tangu siku hiyo hajaonekana kijijini.

Anaona mtu mwingine akitembea karibu na kibanda chake na anasoma kitabu. Anamshtua na kumwambia kuwa yeye ndiye mwotaji aliyepotea na atammeza mzimamzima. Huyu mtu anatoroka na kundondosha kitabu chini. Anapokiangalia anaona ni kitabu cha *Das Kapital*. Baada ya kusoma kitabu hiki kwa wiki moja hali yake inakuwa nafuu kidogo kwa sababu hili buku lina mambo mengine mazuri.

Baada ya maafa ya bomu kupasuka, waliosalia wanajua kuwa vifo vyao vinabisha hodi mlangoni. Wanakaa wakihesabu siku na kuna vituko vingi wakati huu. Mzee mmoja aliyekuwa ameumwa sana na njaa anakwenda ziwani kutafuta maji ya kunywa na anapoona samaki wakiogelea kwa raha anatamani kumpata mmoja kama

mboga ya jioni. Anapoingia majini anajaribu kumshika kwa mkono lakini mamba aliyekuwa pia anamnyemelea anamshika kwa meno.

Kuna kisa cha Padri mzungu ambaye anasali lakini ukame hauishi. Anapoona waumini wameanza kutoa makafara mbuyuni, anaanza kunywa pombe kali ya kwao. Katika ulevi wake anavunjavunja masanamu kanisani huku akiuliza huyu ni Mungu gani. Anapoanza kuchanganya gongo na mvinyo masista wanamkimbia na anaanza kuhubiri juu ya dini mpya ambayo nitokeo la Biblia na Kurani. Anakuwa wa kwanza kupinga wazo la mwanamke kuwa mkombozi wa pili. Anamkana na anapouawa anashangilia. Babake alipochelewa kuhudhuria mazishi yeye ni mmoja wa wale waliomla wakati njaa ilipokidhiri. Jinsi Padri alivyokufa ni mambo ambayo hayasemeki hadharani.

Sheikh anapoona mambo yanazidi kuwa mabaya anaoa visichana vitano vidogo anavyoviita mahurulaini. Anadai pepo huanzia hapahapa ulimwenguni na waumini wake wanafuatia. Uislamu unabaki jina tu na binadamu wanapoanza kulana wenyewe kwa wenyewe msikiti unaota nyasi hata paani. Nguvu za kujitafutia zinapomwishia Sheikh, mahurulaini wanamkimbia na anapokosa nguvu za kujinyanyua mwenyewe fisi walimla. Majirani wanasikia tu mifupa ikilia katika meno ya fisi huku wanacheka.

Pia, kuna kisa cha mwanasayansi ambaye aliyejiita mwafalsafa wakati mwingine na ni mtu wa hasira. Watu wanapomwendea kutafuta ushauri wa kupata chakula anawajibu kwa lugha ya mkato na kuwaambia, kwani ni lazima binadamu ale. Watu

wanaondoka bila kujua wafanye nini. Alizoea kusema kwa hasira kwamba wanasiasa wote ni wajinga.

Pia, kuna habari za huyu jangili kijana anayewashinda wazazi wake. Anaiba ng'ombe, mali ya watu na anaua watu wengi. Ng'ombe wanapokwisha anaanza kuiba watoto na kuwauza mbali. Anapowindwa na watu kwa mikuki na mishale anatoroka na watoto kadhaa. Mwalimu mkuu wa shule anaendelea kufundisha watoto lakini jangili anapoanza kuwawinda watoto, shule inakufa. Mwalimu hafi moyo na anaendelea kufundisha darasa tupu, wanafunzi ni wale wa wakati ujao. Anadai kuwaona kabisa mbele yake na anaamimini binadamu wa sasa hafunziki. Anapiga kelele na kumpiga mwanafunzi wake wa kufikirika akimwambia asifanye tena makosa ya wakati uliopita. Wanafunzi wake wa mawazoni wanajibu maswali kwa lugha isiyoeleweka na jambo hili linamfanya ajiue. Kisa cha mlevi ni cha kuchekesha mno. Anakaa akijua kesho au kesho kutwa atakufa njaa.

### 4.1.4 MZEE KIPOFU

Anakoroma pale kochini na ni kama ameanza kuota kwani anatabasamu kana kwamba hayuko usingizini. Msimulizi anapomtazama anaona ute ukimtoka mdomoni na anapomgusa kidogo begani anastuka na kupanguza midomo yake. Kipofu anamwambia kuwa ameona kila kitu ndani ya kila kitu na hakuna uwongo tena. Anamlaumu kwa kumharibia ndoto zake na hana hakika au ndoto hiyo itarudi tena kwa kuwa hajawahi kuota ndoto kama hiyo aliyowaona wote katika dhambi zao. Anaendelea kusema labda alichanganya uzuri na ubaya. Anamtazama tena lakini safari hii anainua fimbo yake juu na kumuamuru aondoke. Anasema msimulizi anataka kumwibia vitu vyake vya siri wakati amelala lakini msimulizi haondoki.

Anaposimama anazima taa na kujikokota nayo nyuma ya gunia. Anaita ndoto na baada ya sekunde chache anaanza kukoroma.

Msimulizi anapotoka nje anaona ukungu umeanza kuota juu ya kibuyu alichokuja nacho na mwamba ambao kibanda kimenjengwa juu yake umekuwa mweusi. Ni kama amekaa muda mrefu kibandani. Hakumbuki njia aliyoipitia akija, kushuka ni kugumu kuliko kupanda na mawe mengi yameanza kuoza. Kuna maporomoko hapa na pale na anaanza kuwa na wasiwasi na msingi mzima ulioonekana kuwa mlima imara hapo awali. Mlima huu ni kama kitabu ambacho kimepoteza kurasa muhimu, kimetupwa jalalani na inamchukua karne nyingi kuushuka.

Anapofika chini anapumzika na usingizi unamchukua. Anaota akiwa kanisani ambalo limejaa wanafunzi na wote wanaimba kwa masikitiko "*Dies irae, dies illa*- (uk 40). Msimulizi analia na wanapotoka kanisani wanafunzi wanampa pole kwa kushindwa mtihani. Wanamsaidia kufunga mizigo yake na anapokuwa akiondoka Padri mmoja anamfukuza kama mbwa huku akimwambia kuwa hakuteuliwa kwa sababu alikuwa mwizi wa ujuzi. Anapoanza safari fisi wanamfuata lakini hana nguvu za kukimbia na wanapojaribu kumla anaamka ghafla.

Anakumbuka tu alikuwa kwa mzee fulani kwenye mlima. Anatembea kuelekea kwenye mto bondeni, anajitumbukiza majini na kujinyoosha. Anaelekea ukingoni, anaanza kujisugua kwa mchanga na anaanza kutamanitamani. Anapotazama upande mwingine wa mto anaona mwanamke amekaa kivulini akimtazama huku akitabasamu. Hana aibu na anapotoka majini anajianika ili mionzi ya jua imkaushe.

Mwanamke anacheka kicheko cha juu ambacho yeye mwenyewe anazima. Baadaye anavaa nguo zake kwa utaratibu na mwanamke anasimama na kuongoza njia.

Upande ule mwingine wa mto una arthi yenye mchanga. Wanasafiri mchana na usiku bila kupunguza umbali kati yao. Wanapofika jangwani mchanga unaanza kurudisha nyuma hatua za msimulizi. Anajaribu kumfikia yule mwanamke ili aweze kusema naye lakini hawezi. Msimulizi anatamani tu kumgusa na anaamini wanaelekea mahali pamoja na anamwamini. Anaendelea kumfuata na miaka inapita mbila kupunguza umbali kati yao. Wanatembea usiku na mchana, mchana wakichekeana na usiku wakihisi tu umbali uliokuwepo kati yao. Safari inaendelea hivi mpaka wanafika mahali panapokuwa na njia panda na msimulizi anapakumbuka. Mwanamke anashika njia ya kwenda kwa mzee na kuacha kibuyu pale kwenye njia panda. Anamwonyesha msimulizi njia ya kufuata na anamuaga. Anatembea kwa haraka na anamwona pale yule mwanamke wa kwanza alikuwa ameketi na msimulizi hana uhakika ama ni yuleyule.

Anapotazama alipoweka kibuyu anaona miiba imesukumwa pembeni kidogo na anajua hajapotea njia ya kurudi nyumbani. Anakunywa maji wimawima na kumpungia mkono yule mwanamke. Kiasi cha maili moja kutoka njia panda anaona mtu amekaa kivulini peke yake karibu sana na njia. Huyu mtu ni mwanaume na anatega sikio moja anapomkaribia. Anapomtazama vizuri anatambua ni kipofu ambaye ameshikilia fimbo yake mkononi. Msimulizi anaposimama yule mwanaume anamwambia kuwa anajua amesimama na anamtazama na kwamba yeye ni mboni kati ya giza na mwanga. Anaendelea kumwambia kuwa hakuwa akimtarajia na amefika mapema sana. Msimulizi anapotaka kujua anachofanya hapa peke yake,

kipofu anamwambia aulize jinsi alivyofika hapa peke yake. Kipofu naye anataka kujua aendapo na anapomjibu anamwambia hajui aendapo. Kipofu anafikiri msimulizi anahitaji usaidizi naye msimulizi anafikiri kipofu ndiye anahitaji usaidizi lakini kipofu anamwambia yeye ndiye anahitaji msaada wake kwani baada ya njia panda hakuna njia nyingine isipokuwa hiyo na bila msaada wa jinsi ya kuvuka mipaka ya mwanga anaweza kupotea njia. Kipofu anamwambia kuwa hata yeye alifikiria anajua nyumbani hadi siku aliyohamia katika mazingira haya.

Msimulizi anapomwambia kuwa yuko njiani kurudi nyumbani mzee kipofu anamwambia kuwa anaelekea kwa mfadhili na sio kwake kama anavyofikiri. Kipofu anasimama na kuongoza kwa fimbo na mwendo wake ni wa haraka. Anamwambia aharakishe kwani ni bora akistuliwa. Anapotaka kujua atakayestua anaambiwa tu amfuate. Anaambiwa kama angekuwa akienda nyumbani kwake maisha yasingekwenda haraka. Wote wawili wanaamini kila mmoja wao anafuata njia aliyoijua. Kipofu anaenda kwa mwendo wa kazi na haonyeshi dalili za kuchoka. Msimulizi anapomuuliza ama anaishi sehemu hii anamwambia kuwa ameishi hapa karne na karne. Kipofu anamwarifu msimulizi kuwa hapo awali walikuwa majirani. Anamwambia kuwa alifukuzwa na mlevi mmoja. Sasa msimulizi ameanza kuhisi kuwa huyu mzee si kipofu anapomwambia kuwa atamweleza hadithi iliyopelekea kufukuzwa kwake wakifika karibu na mti. Msimulizi anamwambia mzee kuwa anaona na mzee anafurahi kwani msimulizi ameanza kumwamini. Msimulizi anaendelea kumwambia kuwa anahisi anajifanya.

Mzee anakasirika sana na kumwambia asirudie kusema hivyo tena kwani hii ni njia mojawapo ya kumtukana. Anamuuliza au azipasue gololi za macho yake kwa fimbo

na anaendelea kumwambia kama angekuwa akiona hangekuwa hapa. Msimulizi hasemi neno na wanaendelea na safari yao. Mzee kipofu anakuwa wa kwanza kuanza kuzungumza. Anamuuliza ama anajua kwa nini ubikira hupendwa sana na kwa sababu msimulizi hakutegemea swali kama hili, anasema hajui. Mzee anamwambia kuwa ni kwa sababu palipozibwa ndipo penye njia ya kweli. Naye anamuuliza na palipozimbuliwa ni wapi na anamjibu kuwa aulize aliyepazibua. Baada ya hatua chache mzee anauliza swali lingine wakati huu gumu zaidi. Anamuuliza msimulizi, kama binadamu angezibwa matundu yote angekuwaje. Anamjibu labda hangeweza kuishi. Kipofu anasema angeishi na angekuwa bora zaidi. Msimulizi anamuuliza alipata wazo hilo wapi na anamjibu kuwa alisoma kitabu zamani wakati maji ya gololi yake yahakuwa yamepasuliwa.

Mwishowe wanafikia ule mti na kipofu anapatambua mara moja na anaketi karibu na shina lake. Wanapumzika na mara nyoka anaanguka kutoka juu ya mti kwa kishindo. Anapowaona anakimbia haraka na kutokomea majanini. Kipofu anashangaa na kumwambia msimulizi kuwa yule nyoka anamwogopa. Anamwambia ashukuru aliyempa kibuyu cha maji. Anamwambia msimulizi kuwa alizaliwa nusu kipofu kutokana na magonjwa ya zinaa aliyokuwa nayo mama yake. Mama yake kipofu alikuwa Malaya aliyetafuta riziki kwa kuuza mwili wake kwa mabaharia walioeneza uchafu mwingi katika miji iliyokuwa kwenye upwa wa nchi aliyokuwa anaishi. Anaendelea kumwambia kuwa siku aliyozaliwa uchafu ulimwingia kwenye mboni za macho. Akawa nusu kipofu na mamake akamtupa ndani ya pipa la taka na akaendelea kutetea uhai wake. Anaendelea kusema aliokotwa na wazoa taka waliomkabidhi kwa baba mmoja mzee aliyemkuza kwa maziwa ya mbuzi. Alikuzwa katika nusu giza iliyogumbika macho asiuone ulimwengu. Alikuwa katika hali ya nusu ukweli na

akasoma kwa shida na alipokuwa akijitayarisha kufanya mtihani wa kuhitimu shule taa ikazima

Babake kipofu alikuwa mpiga marimba na hakuwa na mtoto mwingine. Mboni za kipofu zilipoziba alimwita na kumwambia hana kitu kingine cha kumridhisha isipokuwa marimba. Alimwambia marimba ndiyo itamhakikishia uhai wake baba atakapokuwa amekufa. Kuanzia siku hiyo alimfunza jinsi ya kupiga marimba naye akajifunza kwa bidii. Babake alizoea kupiga mariba kilabuni na wakati mwingine alipokuja na mashabiki wake, walipiga marimba usiku wote huku wakikunywa pombe. Usiku mmoja alirudi kwa nyumba peke yake na walikuwa bado hawajala chakula cha jioni. Alimwita kipofu chumbani mwake baada ya kula na kumpa marimba mkononi. Alimwambia apige wimbo mmoja na asipige kimyakimya. Aimbe juu ya chochote, kifo au upofu, chochote kitakachofanya sauti yake ipasue upepo wa giza la usiku lililogumbika macho yake. Anamwambia ukweli sasa umo katika giza na alitaka aone kwa mboni za macho yake. Kipofu aliweza kupiga marimba kidogo lakini hakupata maneno. Babake alikasirika na kunmuuliza ama akifa atakula mavi yake. Akamnyang'anya marimba na kurudi naye kwenye pombe.

Usiku huo kipofu hakulala, alifikiria sana juu ya ulimwengu. Kuna kitu ambacho kiliusumbua moyo wake lakini hakuwa na la kusema. Polepole mawazo yakaanza kuungikana na mwishowe maneno yakaibuka hapa na pale na siku moja akamwendea babake chumbani na kuomba apewe marimba. Alipopewa marimba akakaa chini na kuaza kupiga huku akiimba na akahisi babake alikua anasikiliza kwa makini. Baba alishtuka na kumwambia aimbe tena kwa sauti ya juu kidogo. Wimbo ulikuwa huu,

*Ninaimba juu ya giza lililogumbika ulimwengu.*

*Tumetembea katika msitu wa kurasa potovu*

*Na kutafuna kila neno na kila aina ya wino.*

*Tumemeza yapaswayo kunywewa*

*Na kucheua yatakiwayo kumezwa.*

*Vipofu na vichaa wataurudisha ulimwengu*

*Katika nyayo zilizofichana gizani*

*Ondoeni mwanga katika bonde la taaluma*

*Kupunguza ajali na maluweluwe.*

*Muhimu ni kuona gizani*

*Bila kupapasa kuta hafifu za karatasi.*

*Wanaojidai kuona wametufikisha*

*Ukingoni mwa bahari yenye papa na nyangumi,*

*Na wanatushauri tuogelee katika mihadhara*

*Ambayo vichukua sauti vyake ni mitutu ya bunduki*

*Na viti vyake ni vichwa vya nyuklia.*

*Kesho hapatakuwa na msemaji,*

*Msikilizaji wala mshangiliaji*

*Bali mcheko wa utupu katika jangwa*

*Ukishindana na mlio wa vizazi*

*Ambavyo havikupata kuzaliwa (uk 49-50).*

Anapomaliza kuimba, baba anachukua marimba na kumwambia akalale. Anakwenda kulala bila kujua kama babake alifurahia au bado alikuwa na mfudo moyoni mwake. Siku inayofuata majirani wanapita wakisifia sauti waliyoisikia usiku. Baba anaporudi jioni siku hiyo anamkabidhi kipofu marimba mpya. Anasema sasa anaweza kufa

kwani ameacha mtu nyuma wa kuughania ulimwengu tanzia ya binadamu. Kunapokucha kipofu anaagizwa achukue marimba yake na anaongozwa hadi katikati ya mji, njia panda. Njia moja inaenda kanisani, ya pili ikulu, ya tatu sokoni na ya nne msikitini. Anamwambia akae hapo na aimbe ule wimbo wake wa marimba. Msimulizi anapoanza kuimba babake anaweka kopo tupu mbele yake na kuondoka. Msimulizi anatambua kuwa atakuwa maskini ombaomba maishani. Anapoimba anahisi kikundi cha watu kimekwishamzunguka. Anasikia mlio wa sarafu kooni na wasamaria wema wanamletea chakula saa sita. Anaimba hadi jioni anapokuja kuchukuliwa.

Msimulizi anaongoza njia siku ya tatu na anapokosea njia anamwelekeza. Wiki chache baadaye babake anaaga dunia. Anatunga nyimbo zingine mpya na anaishi kwa misaada kuanzia Jumatatu hadi Jumapili. Moyo wake unaanza kuwa karibu zaidi na ushairi. Anaanza kuhisi kama mtu aliyevuka msitari fulani na sasa yuko upande ule mwingine. Siku moja lori mbovu lililoendeshwa na dereva mlevi likampitia na hiyo ikawa nukta ya mwisho ya nyimbo zake za kitanzia. Huyu dereva alimwezesha kuvuka msitari unaoogopwa na wengi. Aliendelea kusema binadamu ni waoga sana, wanajenga majengo marefu na kuruka angani lakini wanasubiri kichaa fulani kama magonjwa yanayoletwa na vijidudu mbalimbali viwasindikize kaburini.

Msimulizi anashangaa anapotambua kuwa anaongea na mtu aliyekufa lakini kipofu anamwambia kuwa amekuja kumshukuru kwa ujasiri wake wakati wa mazishi ya kipofu hata kama bado alikuwa mtoto mdogo. Anamwambia kuwa bado kuna safari ndefu mbele yake ya karne na karne. Anaendelea kumwambia kuwa hana hakika ama ataruhusiwa kwenda nje ya duara maana hatakiwi kucheza ngoma ya pumbao. Anaagizwa asimame na kusindikizwa hadi mahali ambapo angepata malazi.

Anamwarifu kuwa mwenye nyumba ni mpole sana na atamtunza vizuri. Kipofu anatembea kwa mwendo aliouita wa kazi.

Baada ya muda mfupi wanaanza kushuka bondeni na mteremko unaanza kuwa mkali na unabadilika kuwa maporomoko. Wakati mwingine wanashikilia matawi madogo madogo ili wasiporomoke. Wanapofika chini ya bonde kipofu anaongoza hadi mahali panapoonekana kuwa na pango. Anamwonyesha njia itakayomfikisha kwa mfadhili na anamsindikiza kidogo ili kumwondolea wasiwasi. Msimulizi anaambiwa ashikilie ncha ya fimbo kwa sababu hawezi kuona gizani. Kipofu anajua kona zote na mahali vikwazo vilikuwepo. Wanafika mahali penye unyevunyevu na hali ya ubaridi inaanza kusikika. Mlio wa vyura unasikika na arthi inaanza kubonyea na wakawa wanatembea topeni.

Wanapofika mtoni wanapumzika kabla ya kuvuka na kipofu anamwambia kuwa ataweza kumfikia atakapovuka mto lakini hatatambua atakavyomfikia. Kipofu anamwambia kuwa yeye huja hapa mara nyingi lakini mfadhili hunung'unika kuwa wamefanya mahali pake kuwa pao. Msimulizi anahofia hata yeye atafukuzwa lakini kipofu anamwambia kuwa hawezi kufukuza wenye shida ya haki. Msimulizi anapotaka kujua ama anaishi humu peke yake anaambiwa kuwa amuulize yeye mwenyewe.

Msimulizi anataka kurudi nyumbani haraka kwa sababu watu bado wanasubiri jibu na huenda wamemzika msichana tayari. Kipofu anaarifiwa kuwa huyu ni mmoja kati ya wale wanaodai kuwa na kweli mikononi mwao. Msimulizi anaona sasa kifo chake kimeanza kuingiliana na maisha yake. Anakumbuka zamani alivyokuwa akitunga

nyimbo nzuri kuhusu watu kama hao na sasa wasikiapo ushairi wanatoa kwikwi za maumivu makali. Msimulizi hataki kuwa chanzo cha mateso. Wanaanza kusikia maporomoko ya maji na kipofu anamwarifu kuwa mkondo wake una nguvu sana na pahali pa kuvukia ni pamoja tu na mtu anapopakosa huenda na maji. Anamwambia msimulizi kuwa mto huo umeishia ziwani na mfadhili amejenga nyumba yake katikati ya ziwa hili na inaelea tu majini. Kutokana na maelezo haya msimulizi anakosa haja ya kuvuka mto lakini kipofu anamwambia hiyo ndiyo njia pekee ya kumfikia. Wanatembea usawa wa mto na mwishowe kipofu anasimama mahali fulani karibu na mbuyu.

Kipofu amefika mwisho wa safari yake na lazima msimulizi avuke peke yake lakini anamwonya kuhusu jambo moja; lazima awe na ujasiri. Anamwambia kuwa atamsubiri hapo. Anajitosa majini na kuendelea kutembea kwa ari. Kila hatua anayopiga inaelekea mahali fulani kwenye kitu anachotaka kujua lakini hana uhakika. Kadri anavyozidi kwenda mbele ndivyo kina cha maji kinavyoendelea kuwa kirefu na maji yanamfika kifuani na anasimama. Kipofu anamsihi aendelee kutembea kwani hajakosa njia. Anaendelea na maji yanapofika shingoni, miguu inaanza kutetemeka na anahisi kuteleza. Ghafla miguu inainuliwa na mkondo mkali wa maji, anaviringishwa kama pia na hapati muda wa kupiga kelele.

Anajipata amelala karibu na nyumba ndogo inayokuwa na mwanga ndani na mlango ni wazi. Anapokaribia mlango, mwenye nyumba anasikia nyayo zake na anafikiria ni kipofu na kumwambia kuwa amechoshwa na upofu wake. Bila kujali msimulizi anaingia ndani na kumkuta mzee akiota moto akiwa uchi wa mnyama. Msimulizi haamini macho yake kwani ni yule mzee aliyekutana naye kilimani ila sasa amekuwa

mzee zaidi. Msimulizi anajitambulisha kuwa alikuwa hapo siku chache zilizopita lakini anaambiwa kuwa karne nyingi zimepita. Anamwambia mzee kuwa kipofu ndiye amemwelekeza hapa na hajafika kwenye mazishi. Mzee anasema kuwa hataki kusikia tena vifo vya watu vya kujitakia. Mzee anasema kipofu amezoea kuingilia muda wake wa faragha na marimba yake. Anasema analohitaji ni muda wa kukaa peke yake kufanya mambo yake bila kuwa na wasiwasi wa kutazamwa na wachao. Anamkumbusha msimulizi kuwa yeye ndiye alivunja mlango wake na sasa uko wazi. Kama alitaka kuona kila kitu anaambiwa sasa ameona na hajapata faida kutokana na utundu wake. Anakaribishwa na kochi sasa ni kuukuu zaidi na msimulizi anaona aibu kumtazama mzee.

Msimulizi anapotaka kujua kwa nini mzee akahama kutoka kilimani hadi kwenye pango, anasema kuwa zamani alijenga nyumba yake juu kilimani ili aweze kuigwa kutoka mbali lakini sasa amejenga nyumba yake juu ya maji ndani ya pango lenye giza totoro ili isionekane kwa watu watumiao macho kuona. Hataki tena kuigwa na nia yake ni kujificha ili apate muda wa faragha. Msimulizi anataka kujua sababu za kujificha kwenye kibanda cha kishenzi kama hiki. Mzee anakasirika na kusema kuwa ametukanwa na kwamba hahusiki na muundo wa fikra zao tena. Anaendelea kumwambia kuwa kama kuwako kwao kunategemea sana kuwako kwake, basi watafute mwingine wa kujaza nafasi alioiacha na kisha wafuate nyayo zake. Anaendelea kusema hakuna tena awezaye kusimama katikati ya duara. Msimulizi anamkumbusha alivyofurahi hapo zamani alipofuatwa na kupewa sifa za kila aina na anataka kujua kilichomzindua. Mzee anamwambia kuwa zamani walikuwa mawazoni mwake tu lakini sasa amegundua kuwa hata yeye yu mawazoni mwao. Anaendelea kusema yeye ni marejeo ya fikra zao zinazowashinda kuelezwa kikamilifu na moto

wao ni mwigo wa moto anaouona hapa. Anamweleza kuwa alikuwa ameanza kutekwa na mwelekeo wao na alijivuna kwa kiburi kuona taswira zake zinarudufiwa. Kwa sasa ameitupilia mbali ile taa kwa sababu hataki kuwa na mwelekeo wao wa kisasa. Anataka kuwa kama alivyokuwa *in principio,* yaani mwanzoni peke yake. Anataka kufurahia kimyakimya moto wake kwa faragha. Anamwambia arudi alikotoka na asirudi kwake tena kwa sababu kuwako kwake hapo ni kumpotezea uhuru na kunachelewesha mwelekeo wake wa upekee. Anapoona hatingisiki, anainua fimbo yake juu kama anayetaka kumpiga na kuchezesha masikio yake. Anamwelekeza mlangoni kwa fimbo na bila kusema neno msimulizi anatoka nje kwa mwendo wa kunyata. Anatembea kwa uangalifu kwa sababu ya giza lakini ghafla anateleza na kuanguka majini. Anajaribu kuogelea lakini hana nguvu na anapopata fahamu bado yumo gizani. Anahisi kuguswa na kitu fulani, anastuka, lakini wasiwasi wake unapunguzwa na sauti ya mcheko.

Sauti inamwambia ashike fimbo ili waondoke humu kwani macho yake hayatamwondoa humu ambapo atapapasa karatasi milele. Sauti inaendelea kumwambia kuwa taswira za pangoni ni nyingi mno na ni kama amemuudhi mfadhili. Msimulizi hana njaa na ameshiba kutokana na alichokiona. Anaporudi, kipofu anamwambia kuwa mzee huyo ni beberu bazazi kwani hana msimamo. Anamwambia msimulizi kuwa aliitupa ala yake ya muziki motoni huku akisema huo uwe mwisho wa ushairi wake mbovu unaomfanya aote juu ya binadamu. Hamwamini huyu mzee kwani anadai kujua fikra za binadamu zote. Wanatembea kimyakimya na msimulizi anamwambia kipofu kuwa mzee alijivunia nyumba yake ya zamani pekee. Naye kipofu anasema kuwa mzee alifikiri nyumba yake ingedumu milele bila matengenezo. Ilipomporomokea alitoka uchi na fimbo yake na kukimbilia pango hili,

taa yake ikavunjika na ndoto zake zikasahaulika. Ni kipofu na yule mwanamke walioenda kuangalia masalia na walimbebea kochi moja tu. Nyumba haikuporomoka kwa kishindo kwa sababu ilikuwa imejengwa juu ya miamba. Kijumba cha mzee kilitawanyika kama jivu la sigara na kupeperushwa na upepo. Pia msimulizi anaarifiwa kuwa walifika viumbe waliodai kuwa na akili na wakaziba zile nyufa kwa sementi.

Viumbe hawa walipofika kileleni kijumba hakikuwepo na mzee hakuonekana tena. Walikaa chini na kufikiri alikoenda na mmoja wao akawaambia kuwa ukweli umehamia katika kitovu cha mlima huo. Inakuwa vigumu kufikia kitovu kwa sababu tayari walikuwa wameimarisha mlima kwa sementi ngumu. Waliinamisha vichwa vyao na walipoviinua mmoja wao akawaambia washuke na waanze kuubomoa. Kukawa na zogo na mwishowe wakakubaliana wasiubomoe lakini walikosa kufahamu jinsi alivyowapita. Walifikiri Mzee alikuwa amewapita usiku wakati wamelala na kwa sababu alikuwa uchi wa mnyama hawakumwona lakini alikuwa ametumia zile ngazi zao za kujengea kushuka.

Wakati huo wanasikia sauti ikitoka pangoni, ilikuwa ya mwanamke aliyekuwa katika uchungu wa kujifungua. Wanaondoka upesi na kipofu anahisi hii ni mimba ya huyu bazazi ambaye ni hatari. Wanasikia sauti ya mtoto na msimulizi anataka waende wakamwone mtoto lakini kipofu anakataa. Kabla ya kufika mbali wanasikia mlio mwingine wa mtoto. Kipofu anasema sasa ni mapacha na wanaondoke upesi. Anamwambia kuwa dira yao ni kuelekea kule nyota ilitoka la sivyo hawataona njia yao. Wakawa wametoka nje ya pango na macho ya msimulizi yanachukua muda kuzoea mwanga wa nje. Anaachilia ncha ya fimbo ya kipofu ambaye sasa anatembea

kwa mwendo wa kasi zaidi. Wanachukua muda mrefu kupanda kutoka bondeni. Kipofu anaongoza hadi njia anayoikumbuka msimulizi. Inakuwa ni njia ileile aliyoipitia wakati wa kwenda kutoa habari za mazishi. Wanapumzika kidogo halafu wanaagana na msimulizi anaelekea nyumbani. Kipofu anabaki pale labda akisubiri watu wengine ambao wangehitaji msaada wake. Moyo wa msimulizi ni mwepesi sasa kwa sababu ya kuachana na mazingira ya mzee. Amemwekea duara alimozunguka bila kutoka nje.

**4.1.5 MSICHANA AFRIKA**

Wanaposikia habari zake wanatuma polisi kwenda kumshika. Wanamkuta akiwahutubia wanawake huku amesimama kwenye kichuguu na anasikizwa kwa makini. Polisi bila kusema neno wanamshika na kumtia pingu na kumpeleka kwenye gari. Wanawake wanawatupia mawe lakini risasi moja ya hewani inawasambaza wote. Wanampeleka kwenye kitongoji kimoja karibu na mji mkuu wa mkoa na wanamfungia ndani ya kijumba kidogo. Polisi wanamwambia asiwe na wasiwasi kwani kesho yake usiku watamchukua.

Kesho yake jioni, saa moja hivi anachukuliwa na minibasi. Wakati huu Polisi hawamo na anapewa nguo nzuri za kuvaa na mapambo ya mwili. Anaagizwa avae na awafuate. Anapoingia ndani ya kibasi hicho anawakuta wanawake wengine wanne na wote wamevalia vizuri. Kutokana na maumbile yao anabahatisha kuwa wametoka mataifa mbalimbali. Dereva na kodakta ni wanaume weusi. Dereva anamwambia kodakta kuwa siku hiyo itakuwa siku nzuri kwani watu watajionea utukufu wa ulimwengu mzima. Wanaingia kwenye barabara kuu ambayo ina njia mbili; ya kwenda na kurudi na kila njia magari manne yanaweza kupitia. Mataa ni mengi,

yanatoa mwanga wa kutosha na yalipangana vizuri na magari mengi yanaelekea wanakokwenda. Msichana anahisi kana kwamba gari mojawapo la mbele lingepata ajali na mengine yaliyokuwa nyuma yangefuata.

Baada ya muda mfupi wanaingia mjini na mwendo unapunguka. Msichana anatambua kuwa wameanza kupanda kilima kuelekea kwenye kilele. Anapotazama mji kupitia kwenye kioo, anaona vijibarabara vidogo vilivyotoka na kuingia barabara kuu na vingine vilikuwa vyembamba. Anahisi magari ya kisasa yasingeweza kupita, vingine ni vya njia moja tu ya kwenda bila ruhusa ya kurudi, vingine vimezibwa huko mbele na hakuna njia ya kutokea. Vingi havina mwanga wa kutosha, na vingine havina taa kabisa.

Njia wanayofuata imepitia kwenye sehemu ya majengo ya zamani ya Waarabu, makanisa yaliyo na mjengo wa majumba ya Ulaya na karibu na kilele nyumba za kisasa zinaanza kuonekana. Msichana anapatwa na wasiwasi kama kweli angerudi mzima kutoka huko anakopelekwa. Inawachukua dakika ishirini kufika juu ya kilima. Gari linasimama mbele ya jengo kubwa lenye taa nyekundu. Juu ya jengo hili pana maandishi: "*Jengo la Starehe la Olympus.*" Jengo hili limetazamana na jengo lingine ambalo limeandikwa "*Maktaba Kuu ya Taifa.*" Jengo la starehe la Olympus ni la tajiri mmoja wa Kigiriki aliyetokana na ujukuu wa Socrates. Kwa sababu hii, jengo hili limepambwa na picha za wanasayansi mashuhuri, waimbaji na waandishi.

Wanapoteremka, wale wanawake wanne wanaelekea kujua njia na madhumni ya safari yao. Wanazungumza kama kwamba wanajua wenyeji wa sehemu hii ingawa mmoja kati yao anababaika. Mmoja wao anasema siku hii watu ni wengi. Msichana anaongozwa hadi chumba cha maandalizi. Wanakuta mama wa Kigiriki ambaye anawaandaa na kuwaremba vizuri. Msichana kwa mshangao anataka kujua hapa ni

wapi. Yule mama anamwambia kuwa anapaswa kuja hapa kwa sababu pia yeye ni mwanamke. Anapewa jina Agatha na anakumbushwa kuwa mwanamke ana uwezo kuliko kiumbe chote kile. Anaweza kuumba na kuumbua. Agatha anaarifwa kuwa wako hapa ili kuwatia wanaume vichaa. Wanawake wale wengine wanne wamevua nguo zao zote na wanatembea wakichagua nguo za kuanzia.

Ghafla mwanaume anaingia lakini hawashtuki na anafurahi kuona wametimia. Anawaambia Ulaya ataanza kuingia, Amerika atafuata naye Asia atafuatwa na Australia. Afrika anaarifiwa kuwa ataingia akiwa wa mwisho. Huyu mwanaume ni meneja wa mwanga mwekundu wa Olympia. Ndani ya jumba hili mna kelele la zogo kama soko la watumwa. Watu tayari wamekaa na viti vimejaa. Mstari wa mbele wamekaa wanasayansi mashuhuri kutoka nchi mbalimbali na hawakupenda kuona wengine mbele yao kwa sababu ni viongozi na wanapaswa kuona vizuri. Nyuma yao wamekaa viongozi wa dini mbalimbali. Mstari wao ni kama ukuta unaowakinga wanasiasa kwa nyuma. Wao ni viongozi wa roho. Viongozi hawa wanafuatwa na maprofesa wa vyuo vikuu, walimu wa vyuo vidogo na mabaharia wamejipenyeza katika kundi hili. Maprofesa wamepumzisha vichwa vyao baada ya kutoka kwenye maktaba kuu. Katika kundi hili pia kuna wanafunzi wa vyuo vikuu ambao wamekuja kutafuta data za tasnifu zao. Pia kuna wafanyakazi wa kawaida na nyuma yao hakuna viti lakini kuna nafasi iliyo wazi kwa wanaotaka kulipa pesa kidogo. Hapa pana genge la wezi, wavuta bangi na makuli. Wako mbali na jukwaa na hawawezi kuona vizuri lakini wanafurahia vurumai iliyoko hapa nyuma.

Kuna wasichana wadogo wanaowapa vinywaji wanaoagiza. Baharia mmoja anashika chuchu za msichana mmoja na maprofesa wanajiuliza anafunza chuo kipi. Hawa

wasichana hawafiki katika viti vya nyuma. Wale ambao wameagiza vinywaji vikali wameanza kulewa, hasa wale walio katika viti vya mbele lakini wanatunza heshima zao. Polisi wanaingia kulinda sehemu ya nyuma mambo yanapokaribia kuanza.

Nje bado kuna msururu mrefu wa watu wanaotaka kukata tiketi ya kuingia. Hawaamini wanapoambiwa hakuna nafasi usiku huu. Wengi wao wanashangaa kwa sababu walikuwa wamefika mapema na ni watu wachache tu waliokuwa mbele yao. Pia, hawaelewi wanasiasa wanafanya nini humo ndani na huu ni ulimwengu wao. Milango inafungwa na saa mbili kamili mambo yanaanza. Pazia inainuliwa na msichana wa kwanza anaingia akicheza kwa mwendo wa harakaharaka uliodhihirisha uhai wake. Amevalia vizuri toka kichwa hadi miguuni. Muziki wa kuingia unapokwisha, anachukua kipaaza sauti na anaanza kuzungumza kwa tabasamu akiwatazama wateja wake. Anasema yeye ni msichana wa kazi na baada ya muda mfupi watakiri kwamba kazi ipo. Anawaambia kuwa anazo rekodi tano ambazo atapiga na kucheza.

Rekodi ya kwanza anayoipenda na kuithamini ilimwondoa utumwani, utumwa wa kanisa na malaika wake. Anacheza rekodi kidogo kisha anavua blauzi, anabaki na sidiria tupu na wateja wanashangilia. Wanasiasa wanaanza kusogezasogeza miwani na viongozi wa dini wanashikwa na butwaa. Msichana anawaambia kuwa huu ni mwanzo tu. Rekodi ya pili ilimwonyesha njia mpya na inapolia anacheza kwa bidii kuliko ile ya kwanza. Safari hii anavua sketi na anabaki na gagulo na sidiria tu. Waliokuwa katika mstari wa mbele wanaanza kuhema na kiongozi mmoja wa dini anapiga ishara ya msalaba. Msichana anatoa ufundi wake wote na wateja wanataka arudie. Rekodi ya tatu ni rekodi iliyomtoa jikoni na anapoianza anavua gagulo

harakaharaka kama kichaa, anavua sidiria na zote anazitupa pembeni. Anacheza na mara anawategea mgomgo, mara anawatazama. Walioketi katika viti vya mbele wanajitahidi kutoonyesha hisia zao za kweli na maprofesa wanavuta pumzi ndefu kupunguza mbanano wa hisia za ndani.

Rekodi ya nne ni rekodi iliyompa uhuru wake kamili. Inapowekwa kwanza anacheza bila kufanya lolote la ajabu lakini inapofika katikati anazima rekodi na kuwauliza wateja ama wanataka kuona. Wote wanataka kuona, anavua viatu na kwa madaha anavua nguo yake ya mwisho na kuitupia wateja. Holi zima inapata kichaa na ni kama Warumi wanamwona simba akimrarua mtumwa miaka michache kabla ya anguko la himaya yao. Macho ya wateja yanajaribu kuona kila kitu na wengi wa mbele wanafikiri wameona matamanio ya ndoto zao. Wakati huu baadhi ya wanawake waliokuwa wameandamana na waume zao wanasimama kutoka nje; wengine wana hasira na wengine huruma. Msichana anacheza rekodi yake ya mwisho iliyomtia kichaa cha uhuru, rekodi iliyomfunga mwanaume akawa anamfuata na kutii amri zake. Rekodi inapoanza hakuna jambo jipya analofanya lakini inapofika katikati anaanza kucheza akipanua miguu na wateja wanapata kichaa. Kiongozi mmoja wa dini anazimia lakini hakuna anayemjali. Msichana anapolala chini wote walio mbele wanasimama na walio nyuma wanapiga kelele. Anapomaliza anatoa heshima kwa kuinama hali amewategea mgongo. Holi zima inajaa vifijo. Anatembea kama askari wa Sparta kutoka jukwaani na pazia inashushwa. Ni kama karne nne zimepita. Mwanasiasa mmoja anasema pesa zake zimeenda kwa haki.

Msichana anaporudi katika chumba cha matayarisho ana hema na wenzake isipokuwa Agatha wanampongeza na kumbusu. Meneja anaingia na kumpa bunda la shilingi

elfu kumi. Msichana wa pili anaingia, anapomaliza wa tatu anaingia halafu wanne. Wote wanatakiwa kucheza rekodi tano mara nne jukwaani na walicheza mitindo tofauti. Usiku mmoja wanapata shilingi elfu arobaini kila mmoja, mshahara ambao profesa hangeufikia maishani.

Sasa ni zamu ya Agatha kuingia jukwaani. Amevaa vazi jeusi toka blauzi hadi kiatu. Muziki wa kuingia unapolia anaingia kwa utaratibu bila kucheza. Anachukua kipaaza sauti na kusema yeye ni mwanzo na mwisho wao. Anaendelea kuwaaambia kuwa walikuja kupitia kwake na wataondoka kupitia kwake. Kumvunjia heshima ni kama kuvuja heshima ya utu wao. Anawaambia hatacheza densi mbele yao kwa sababu wote wameoza na Afrika haitacheza densi katika mwanga wa usiku. Meneja anakasirika kwa sababu ya kuharibiwa sifa za kimataifa. Anaamuru wanaume kumi wamshike na wamvue nguo kwa nguvu. Wanapomkaribia anavua viatu vyake na kumpiga mmoja wao jichoni anapojaribu kugusa nguo zake. Jicho linapasuka na wengine wanarudi nyuma. Msichana anamfuata meneja akiwa na viatu mkononi na meneja anakimbia akipiga kelele. Anasema ashikwe kwa sababu ana kichaa cha mbwa. Wafanyakazi wengine watano wanajitokeza lakini anawapiga mateke na kuwaangusha kabla ya kusalimu amri baada ya kutupiwa kamba shingoni. Wateja walifurahia vurumai ya wenyeji wao. Hali inapokuwa shwari meneja anatambaa toka chini ya viti na kuenda jukwaani kutoa tangazo.

Anawaambia wateja wamsamehe kwa kuwa alimtoa msituni siku iliyopita na hajamwingiza katika muundo wa uchumi wa ulimwengu na pia hajazoea mwanga wa aina hii. Anaahidi kumfunza ustaarabu na pia kuwarudishia pesa zao. Wateja wanaridhika na kutoka nje na wanarudishiwa pesa zao pale mlangoni. Agatha

anafungwa na kupelekwa katika chumba cha meneja. Baada ya kupigwa viboko wanamfungua. Anaanza tena kupigana nao, wanamuua akipigana na wanamnajisi akiwa amekufa. Wanarudisha maiti kijijini baada ya kumwekea dawa ya kuhifadhi mwili. Wanakijiji wanakaa na maiti wakisubiri baba yake ahudhurie mazishi hadi siku moja Padri mlevi anaposema kuwa anakumbuka jinsi walivyomuua akipigana na tangu siku hiyo, Afrika mpya ikazaliwa.

### 4.1.6 AMANI

Amesafiri mwendo kiasi na moyoni anajiuliza kama kuna uwezekano wa kutoka nje ya duara ya mzee. Mwili wake unaanza kupata nguvu mpya anapoanza kuona miti inayofanana na mahali alipotoka. Anaongeza mwendo lakini kadri anavyotembea ndivyo hali ya ukame inavyozidi kuongezeka. Anaanza kuwa na wasiwasi kwa sababu hali hii inaonyesha hakuna kiumbe hai katika nchi yake.

Kwa mbali anaona kikundi cha watoto kumi hivi wanaofukuzana na ni kama wanawinda. Wanapomwona wanashtuka na kusimama kumsubiri. Anapowakaribia anawatazama kwa muda bila kusema neno. Baadhi wanatazamana halafu wanacheka. Wako vifua wazi na wamevaa matambara yanayoonyesha dalili za shida na umaskini. Wote wana pinde na mishale. Wanamweleza kuwa wanakaa bondeni na kaka yao na mmoja wao anaongoza njia na msimulizi anamfuata. Hawa watoto wengine wanamzunguka pembeni na nyuma. Bondeni anaona vibanda viwili vya majani na kimoja ni kikubwa. Kijana anayeongoza anamuashiria asimame huku wengine wakimzunguka. Kijana mkubwa wa umri wa miaka ishirini hivi anatoka mle kibandani akiwa na mkuki mkononi. Anamuelekea kwa mwendo wa kishujaa na anasimika mkuki wake undongoni na kumtazama kwa macho ya ukali na yeye pia

anamwangalia vivyo hivyo. Kijana anataka kujua ama ni amani au ni vita. Msimulizi anapomwambia kwamba ni amani anachomoa mkuki wake toka udongoni na kumkaribisha ndani. Kijana anawaambia watoto waandae chakula cha mchana. Wanapokaa anamuuliza msimulizi jina lake. Anapomwambia anamtazama kwa mshangao na kumweleza kuwa jina lake si geni sana na habari zake wamezisikia ila hana uhakika ama ni yeye au ni mwingine kwa sababu hakutegemewa wakati kama huu. Kijana anamwambia kuwa kabla baba yake kuaga alikuwa anasimulia habari za msimulizi. Watu walikuwa wametambua kuwa msimulizi ni mwenye fikra nyingi na walianza kuyakumbuka maneno yake maafa yalipotokea. Kijana anamweleza kuwa alitorokea hapa maafa yalipoanza kutokea. Msimulizi anapewa maji ya kuoga na baadaye anakaribishwa kwa chakula cha mchana cha panzi waliokaangwa na mizizi.

Wanapomaliza kula anaelezwa habari kamili kuwa mambo yalianza kama mzaha. Watu walishangilia baada ya ukame na wote wakalima. Chakula kikawa kingi mwaka huo halafu kukatokea wazo na wakaimba kuwa watawasha mwenge mlimani umulike dunia nzima. Watu wote wakapata moyo wa kushirikiana na kukawa na matumaini lakini katika hali hii kukatokea balaa. Viongozi walitaka sifa kwa yote yaliyotokea na viongozi wa chama ndio walikuwa wa kwanza kulewa heshima na wakataka watu wote nchini wawe vikaragosi vyao. Waandishi walitakiwa kuandika juu ya sifa za viongozi hawa. Chama kikawa na kauli ya mwisho juu ya kila kitu. Kikaongoza uchumi na utaalamu wa walimu wa vyuo vikuu ukaacha kudhaminiwa tena. Wafanyakazi wakapewa mishahara duni na wakafanya kazi kwa masaa mengi. Wanafunzi walipoandama walipigwa virungu na walipoendelea wakafukuzwa shule. Wengi wakaogopa na wataalamu wakaacha jahazi liendeshwe na upepo. Katika kuyumbayumba huku chakula kikakosekana na watu wakala chochote

kilichopatikana. Waimbaji wakaimba nyimbo za kejeli lakini walikemewa. Wazee wakaanza kugawana kile kidogo kilichokuwepo na kilipopungua kukatokea ugonjwa wa kuwania vyeo katika chama na serikali. Wakaanza kuuana na ikawa vurugu tupu. Ukame ukaanza tena na kukawa na chama cha kuzikana. Anaendelea kumwambia kuwa pakatokea kipofu na akaimba wimbo wa wakati ujao. Viongozi walikasirishwa na jinsi alivyodai kuona zaidi ya wenye macho. Akagongwa kimaksudi na lori ili akawaimbie sisimizi kwenye giza la milele. Haukupita muda kabla ya bomu la nyuklia kudondoshwa na mataifa makubwa na watu wakafa kama panya na waliobaki walidhoofika. Hawakuwa na nguvu za kuchimba makaburi marefu na fisi wakazifukua maiti na kula. Mvua haikunyesha hadi ikafikia hatua ya binadamu kumla binandamu mwenzake. Anamweleza kuwa hali ilipokuwa hivi, yeye na watoto hawa walisafiri hadi wakafika katika bonde hili walipopata maji. Bonde ni refu sana na hawajui lilichimbwa na nani na wanaishi kwa kula panzi. Msimulizi anaarifiwa kuwa hawa watoto ni yatima na wanamwona huyu kijana kama kaka yao.

Baada ya maelezo haya anamsimulia msimulizi juu ya maisha yake humo bondeni. Anakiri kwamba maafa hayo yote yalimfunza kuwa mtiifu kwa yeye mwenye uwezo wote. Wanapomaliza chakula anawaita watoto na wanasali wote kwa pamoja. Anamweleza uzoefu wake kuhusu matendo ya binadamu ya njaa na kuwa kushiba au kutoshiba ndiko kunatoa umbo la mwanadamu. Kabla ya kulala anamwelekeza jinsi ya kufika nyumbani. Anamwambia aelekee mashariki na asikate tamaa.

Usiku msimulizi halali vizuri kwa sasbabu ya kuumwa na mbu na anapata usingizi wakati jogoo wa kwanza anawika.Anaamshwa mapema ili jua likichomoza awe amefika mbali na anapewa watoto watatu wamsindikize hadi mpakani. Pia, anapewa

kibuyu cha panzi na kile chake kinajazwa maji ya kunywa. Wanaagana na watoto wamnafuata wakiwa na pinde na mishale na wanamfikisha hadi mpakani.

Msimulizi anatembea juu ya arthi inayokuwa nusu jangwa kwa siku tatu huku akipumzika mchana na kulala usiku. Siku ya nne anapotea njia kwa sababu ya mawingu na hana uhakika mashariki ni wapi. Siku hiyo hiyo ya nne anakumbana na mijusi na hakuna mahali pa kukanyaga kwa sababu walikuwa wengi. Wanapomwona wanainua vichwa juu na kuvitingisha chini kwa wakati mmoja kama alama ya salamu au swali. Wote wanageuka na kuelekea anakokwenda naye anawafuata. Anapoanza kushuka bondeni anaona kibanda kilichokuwa na ukuta wa mviringo na mijusi wanatembea kuelekea huko naye anawafuata.

Mlango wa ukuta ulikuwa wazi na mijusi wanaingia na kuwa kama ng'ombe zizini. Anapogeuka anaona kijana amesimama na mkuki mkononi. Anamtazama kwa uangalifu huku akitabasamua na kumweleza kuwa hakuwa akimtarajia wakati huo. Anamkaribisha kwa heshima na wanaketi chini ya mbuyu uliokuwa karibu na nyumba yake. Baada ya muda, msimulizi anaanza kuuliza maswali kuhusu nchi yake lakini anaambiwa kuwa dalili zote zinaonyesha kuwa hajakosea njia. Kijana anaendelea kumwambia kuwa ulimwengu haujui namna ya kupafikia tena pale alipoanzia safari. Anasema, wanapoongeza ujuzi wanafikiri wameongeza maarifa mapya. Baada ya kimya kidogo msimulizi anamwarifu kuwa alikuwa ameenda kutoa taarifa ya mazishi na sasa anarudi nyumbani. Kijana anamwambia ni vizuri kama ameamua kutalii mipaka ya nafsi yake kwani ndanimwe hamna barabara. Anamwambia kuwa anaweza kusafiri mumo mpaka afikie *axis operandi;* mhimili unaofanya mambo yaende na hakuna binadamu ambaye hana nguvu za kuzunguka kwenye mhimili wake mwenyewe.

Kijana anamstua msimulizi anapomuuliza kama amemwona mzee. Msimulizi anataka kujua kama wanajuana na anamweleza kuwa alikuwa amepita hapo na blanketi huku amejiharia na amezeeka sana. Msimulizi anamwambia kuwa walikuwa na mzee na yale yote yaliyotokea kati yao. Mzee alikuwa amemwambia kuwa ataishi milele na awaambie kuwa bado anaweza kutembea kwa miguu yake mwenyewe. Kijana anasema kuwa yule mzee hupita hapo hata mara tatu kwa mwaka na mawazo yake ni kuwa kila mtu anamfahamu. Hana makao maalumu, yuko kila mahali anazurura na hana chochote cha maana kwake, ni maskini sana. Kijana anaendelea kusema kuwa yeyote yule ambaye amepata kuzungumza na dhamiri ya nafsi yake amepata kufika kwake.

Wanatoka nje na kuingia kwenye zizi la mijusi na kijana anawashika. Wanaenda nyuma ya kibanda na anawakata vichwa na kuwapasua tumbo kwa kisu. Anampa kazi ya kuondoa matumbo, kazi iliyokuwa na kinyaa halafu wanaoshwa na wanaandama hadi kibandani. Mijusi wanawekwa juu ya wavu wa chuma na kubanikwa motoni. Mijusi ni samaki wa jangwani. Msimulizi anapomuuliza kijana muda ambao amekaa hapo anaarifiwa kuwa ni kutoka ule wakati wa njaa kuu. Kijana hataki kuhama kwani hajui mahali pengine penye samaki wengi wa jangwani na watamu kama hawa. Kijana anamweleza alivyowapata wale mijusi na jinsi wanavyowasiliana. Anasema hawa samaki wa jangwani hawana dhana ya kukataa na hutuliza ile hali ya ubwana aliyo nayo mwanadamu.

Mijusi wako tayari na wanapangwa vizuri ndani ya chungu, anaweka maji na kukitega chungu juu ya mafiga. Wanaendelea kuzungumza kuhusu mada mbalimbali na samaki

wa jangwani wanapokuwa tayari anatega sufuria ya ugali. Baada ya chakula anamtayarishia kitanda na analala. Hakulala kwa sababu ya mbu na anapata usingizi wakati jogoo wa kwanza anawika. Kifungua kinyua ni mchuzi mzito wa mchuzi wa samaki wa jangwani. Wanafunguliwa na wanakwenda machungani. Wanapomaliza kuosha vyombo anamwonyesha baadhi ya kazi zake.

Wanaongozana hadi bondeni na njia inawapeleka hadi pangoni. Msimulizi anastuka lakini anakaa kimya. Wanapofika kwenye mlango wa pango, unajifungua wenyewe na mara moja taa za umeme zinawaka na kuna chemchemi ya maji katikati. Pango ni safi ingawa limejaa vyombo vya maabara. Msimulizi anagundua kuwa kuna mto chini ya pango hili ambalo kijana hutumia kujipatia umeme.

Pia, hutumia nusu ya muda wake kufanya majaribio na nusu nyingine katika kuwaza. Anaendelea kusema kuwa kwa miaka mingi amekuwa akifanya jaribio moja tu la kugundua kindonge kinachoweza kumshibisha mwanadamu kwa muda wa juma, miezi na hata miaka. Anasema akigundua kindonge hiki ataweka herufi kubwa ya kuanza sura mpya ya kuzaliwa kwa mwanadamu kwani binadamu angekuwa na ubinadamu zaidi. Ulaji ndio umeleta ghasia ulimwenguni na unaleta kutoaminiana kati ya wanadamu. Anasema kama binadamu angetumia muda wake kuwaza na kufanya majaribio mengi angekuwa amekishinda kifo. Angeweza kujiumba na kuumba binadamu wengine kwenye maabara. Anasema binadamu angetumia muda kujifunza jinsi mwili wa sisimizi unavyofanya kazi na angejipunguzia udhia mwingi. Neno maumbile limewapumbaza wengi na kutokana na maumbile waliyo nayo wanaweza kujaribu maumbile mapya kupitia sayansi.

Msimulizi anamwambia amependezwa na majaribio yake lakini msingi wa falsafa yake unawarudisha nyuma walikotoka. Imani ni kuwa binadamu ndiye kitovu cha maumbile yote na kila kitu ni kwa ajili ya matumizi yake. Anamwambia kijana kuwa ana wasiwasi na falsafa inayojaribu kufanya sayansi na teknolojia vitawale kuwako kwa binadamu na mwishowe kuwa kitovu cha fikra. Pia anasema, sayansi na teknolojia havifikiri na anaendelea kusema kuwa binadamu ana uwezo wa kuzunguka kwenye mhimili wake mwenyewe. La sivyo angekuwa hatarini kutoweka kwenye sura ya dunia. Kijana anamwonyesha mtambo utakaomkoboa mwanadamu kwa kunyonya takataka zote zilizotokana na bomu la nyuklia kutoka udongoni ili mazao yasiwe na madhara. Anasema mitambo mia moja itatosha ulimwengu mzima na huu ni wa sehemu hii pekee. Wanarudi nyumbani kwa chakula cha mchana na baadaye wanakuwa na majadiliano makali kuhusu umuhimu wa vurumai katika fikra na ulazima wa kuvunja uhusiano uliopo kati ya mtu na kitu. Majadiliano yanaendelea hadi jioni. Ni wao tu wamesalia na juhudi yao ni moja. Kijana anamwambia atarajie kukuta mabadiliko makubwa.

Baa la njaa na uharibifu mkubwa umeweka nukta kwenye fikra zitazamazo wakati kama mstari mmoja mrefu wenye mwanzo na mwisho. Anasema sura yenye mtazamo mpya lazima ianze lakini itaanza wakati mzee atakapoondoka katika kitovu cha duara. Ni lazima aache kuzuru mashamba ya fikra zao ijapokuwa ana uwezo wa kurutubisha. Kizee ambacho hakijafa huwaweka walio hai utumwani na kuzaliwa kwake kulikuwa kama mzaha na walimwita Kakulu.

Lepe la usingizi linaaanza kumshika msimulizi na anayasikia maelezo haya akiwa nusu usingizi na nusu macho. Hakusikia mbu usiku huo. Anapata ndoto ambapo kizee

kinamkaba koo na taswira hii inajitokeza tena na tena usingizini. Anapoamshwa asubuhi, yuko katika ubishi mkali na kizee. Kesho yake msimulizi anaondoka ili afikishe ujumbe hata kama ni kupiga kelele katika utupu. Anamshukuru kijana kwani mazungumzo yao yalikuwa mazuri. Anaanza safari tena na anawekewa maji kwenye kibuyu chake na ndani ya kibuyu kingine amewekewa mchuzi mwororo wa samaki wa jangwani. Siku hii inaanza vizuri na anakuwa na uhakika wa dira anayofuata. Siku ya saba anafika kwenye nchi ambayo ilikuwa imeanza kupata mvua na wazo linamjia kuwa yuko karibu na kijiji chake.

Anaona jiwe kubwa mbele yake na linamkumbusha utoto wake. Anakumbuka zamani wakitoka shuleni walizoea kupanda juu ya jiwe hili na kutereka toka juu hadi chini kwa mwendo mkali. Nguo zao zilipasuka mara kwa mara toka makalioni. Siku ya Jumamosi walizoea kulikalia wakitoka kanisani kuungama dhambi zao kwa Padri. Hawakuwapenda mapadri waliotoa malipizo marefu ya sala ya imani na rozari kwa sababu hawakujua uzito wa ala hizo kwa dhamiri zao na maisha ya baadaye. Anapoendelea kwenda anaona gofu la jengo lililofanyiwa marekebisho baada ya vita na kuwa shule ya msingi kijijini. Anapotembea kuliekea anaona ni darasa tu limesimama. Anaingia kwenye darasa hili na buibui wametanda katika kila pembe na anasema kimoyomoyo kuwa bado kuna uhai. Baadhi ya sehemu za darasa hili zimeanza kuoza na madawati hayana kitu. Mbele yake kuna ukuta wenye sehemu nyeusi ambayo imeanza kufifia na maandishi hafifu yanaweza kuonekana. Anasogea karibu na anapoyasoma yameandikwa hivi;

> *Kwa watakaosalia. Msifanye makosa tuliyoyafanya*
> *sisi. Tulifunzwa hatukufunzika. Hatukuweza*
> *kuongoza mkondo wa sayansi na uchumi, siasa*

*iliposhika hatamu. Yote myaonayo ni kumbukumbu*

*tu za ujinga wetu. Aibu kwetu ngulu mbili!* (uk 96).

Anatoka nje na karibu na gofu hilo anaona gofu lingine ambalo limesimama imara na halionyeshi dalili za kuanguka hivi karibuni. Anatembea haraka kuelekea jengo hili akiwa na matumaini ya kukutana na kiumbe. Jengo hili ni kanisa na msalaba ulio juu ni imara. Milango iko wazi, anaingia ndani na kuna dalili za uhai kwa sababu viti vimeanza kuliwa na wadudu.

Anatembea hadi sehemu za mbele na macho yake yanavutiwa mara moja na sanamu la Yesu msalabani ambalo halikuwa na kichwa. Anaposogea karibu anaona kuwa kimedondoka chini. Kina nyufa na kimezungukwa na taji la miba na macho yanaangalia juu kama kwamba yanachunguza umbali uliopo kati ya sakafu na shingo. Anapogusa kiwiliwili kilichobaki msalabani sanamu yote na msalaba wake inaporomoka sakafuni na kuvunjika vipandevipande. Mwanguko huu unamtisha. Ukutani picha yenye macho matatu yaliofifia inamtazama lakini haitishi kama hapo zamani. Sanamu ya Bikira Maria imo juu ya altare ndogo na mikono pamoja na kitoto chake imedondoka. Kipande cha mkono uliovunjika kinamfanya aonekane kama kilema ombaomba. Sanamu ya mtoto ilikuwa imeanguka kifundifundi kama iliyosukumwa kimaksudi na kilijaribu kujinyanyua bila mafanikio. Katika altare nyingine pamesimama sanamu ya Mtakatifu Yosefu lakini wakati huu haikuwa na ile fimbo ndefu ya kuchunga au kutembelea. Imevunjika vipadevipande na macho yake yanaangalia kwa huzuni uwanja ambao hauna kondoo tena. Sehemu ya katikati ambayo ni altare kubwa haina kitambaa chochote na maua yamekauka. Anatembea kuelekea tabenakalo ambamo hostie zinatunzwa. Funguo imo tunduni lakini shauri ya

kutu haifungui. Anaenda katika chumba cha sakristia ambamo mapdri walivalia nguo za kutolea sadaka.

Kwa mara ya kwanza anakuta mifupa ya mtu aliyefariki miaka kadhaa ndani ya chumba hiki. Pembeni anaona kitabu cha *Das Kapital* ambacho kimechakaa. Vipande vya nguo vya kusomea misa vimeizunguka mifupa. Karibu na mifupa hii anaokota karatasi ambayo imeandikwa maandishi haya;

*Kwa yeyote yule awaye*

*Nilikuwa wa mwisho kufa*

*Katika tarafa hii*

*Ninayo mawili tu ya kusema*

Nil desperandum! ( uk 98).

Anafungua madawati na yote yana nguo na zana zingine za matambiko. Kabati lina chupa nyingi za mvinyo na anachukua mbili na kutoka nje. Kutazamana na jengo hili anaona msikiti wa Waislamu wachache walioishi kijijini. Ndani kuna hali ya unyevunyevu kwenye kuta na ni kama paa lilivunja wakati mvua zilianza kunyesha. Ndani hamna kitu isipokuwa msala mmoja ambao umeoza. Kwenye ukuta mmoja anaweza kusoma maneno "*Allah Akbar*" ambayo yameandikwa kwa mwandiko mbovu wa Kiarabu. Anaondoka mahali hapa kwa sababu ya hali ya baridi.

Baada ya hatua chache kutoka msikitini anafika makaburini na mipaka kati ya Wakristo, Waislamu na Wapagani inaweza kuonekana na baadhi ya misalaba bado inajitokeza. Anatafuta kaburi la mkewe na analiona. Ndilo pekee limepaliliwa hivi karibuni na hajui aliyelipalilia. Pia analiona kaburi la mama yake lakini anakata tamaa

anapoona makaburi mengi hayana majina na mengine yalikuwa makubwa sana. Hatafuti la babu yake kwa sababu amezikwa sehemu ya kaburi la wapagani na sehemu hizi majani ni marefu sana na miti imeanza kukua.

Anaondoka makaburini kwenda kijijini jua linapotua. Kila mahali ni kimya isipokuwa milio ya wadudu waliao wakati wa kilimo. Njia ambayo hapo zamani ilikuwa barabara pana sasa ni kichochoro kidogo kati ya majani marefu. Anapofika mahali penye mbuyu anahisi mtu au mnyama fulani anamfuata nyuma Anapotazama nyuma haoni kitu na anarudi hadi kwenye mbuyu, anauzunguka lakini haoni kitu. Anakumbuka wazee walifanyia makafara hapa. Anakata shauri kuendelea mbele na njia aliyofuata. Kabla ya kufika mbali anasikia mtu anapiga makofi, kama alama ya kumwambia arudi. Safari hii anaangalia nyuma haraka lakini haoni mtu.

Anatembea hadi anapofika mahali ambapo pana mto na anaona korongo refu. Chini anaona maji machache ya kimvua kilichonyesha siku kadhaa zilizopita. Maji haya yameanza kuzalisha mbu ambao sasa wanamsakama. Hisia zake zinamfanya arudi nyuma anapohisi kuwa ameacha kijiji chake nyuma na kuna mtu ambaye bado anamfuata. Anatafuta kijia kilichochepukia kijijini na sasa giza limekuwa nene. Anapinda kulia na mbali kidogo anaanza kuona nyumba.

Anaingia ndani ya nyumba moja iliyokuwa imeezekwa kwa bati moja. Kwa wasiwasi anapapasa kuta na anagusa kitasa cha mlango, anaifungua na kuingia chumbani. Mara anajigonga na kitanda cha chuma. Anakipapasa kupata sehemu ya mto na shuka iliyokuwa juu imeenea vumbi na takataka nyingi. Akiwa humo gizani anafungua chupa moja ya mvinyo na kunywa kabla ya kulala. Mwanzoni mbu wanamsumbua

lakini baadaye analala usingizi wa pono na ndoto zinaanza kumsumbua. Anaota amemkata mtu shingo kwa kisu na damu yake ikamrukia machoni. Mara kile kichwa kinabadilika na kuwa cha yule mzee aliyemjua hapo zamani. Anastuka na analala tena na kuota akifanya mapenzi na mwanamke pia aliyemjua zamani. Anastuka na anapolala anaota nyati mkali akimfukuza na hana nguvu ya kukimbia wala sauti haimtoki. Anastuka na kuanguka chini ya kitanda na wakati huu haoti tena anapolala.

Nyimbo za ndege zinamwamsha na hii ni ishara ya uhai mahali fulani katika msitu. Kuna mwanga wa kutosha ndani ya nyumba na msimulizi anaona nyumba yenyewe ni gofu lenye kuta mbovu na mashimo kila mahali. Anapopepesa macho, bila kutegemea anaona mwanamke akiwa uchi huku akitabasamu na amekaa kitandani. Anasimama bado akitabasamu na kumwashiria kwa kidole amfuate. Msimulizi sasa anatambua kuwa ule mto aliolalia ni khanga iliyokunjwa na shuka pia ni khanga nyingine. Anazichukua pamoja na chupa za mvinyo na kumfuata. Anakumbuka aliacha vibuyu kanisani.

Mwanga unamulika magofu ya nyumba kijijini na hakuna tena cha kujivunia. Mwanamke anaongoza njia na anahakikisha umbali kati yake na msimulizi haukuongezeka wala kupungua. Anaongoza na wanapita magofu kadhaa lakini msimulizi hayaangalii kwa makini kwa vile anayaelekeza macho yake kwa umbile nzuri la mwanamke huyu. Anapofika kwenye kibanda chenye matofali anasimama na kumwonyesha kwa kidole mlango wa kibanda hicho na kuzunguka nyuma. Msimulizi anazunguka kwa haraka upande mwingine ili akutane naye huko nyuma ya kibanda lakini hamwoni.

Anaporudi mbele ya nyumba anaona kuwa nyumba hii ni imara kidogo na anakumbuka kuwa hiyo ndiyo ilikuwa nyumba yake. Anapotazama nyumba zingine jirani anaona zimeanguka na anaona nyumba ya kichaa. Anapotazama nyumba yake anaona mlango bado umefungwa lakini dirisha la chumba cha babake ni wazi. Anausogelea polepole na anapousukuma ndani unaanguka kwa kishindo. Anamsikia mtu akikohoa ndani na anajiuliza au babake ambaye bado alikuwa hai au ni yule mwanamke. Chumba chake ni kama alivyokiacha lakini anapoelekea katika chumba cha babake anastuka.

Mzee mwenye mvi nyingi amelala juu ya kitanda na amejifunika blanketi kuukuu sana na lilikuwa na mashimo mengi yaliyoonyesha sehemu za mwili wake. Alikuwa amefumba macho yake lakini anatambua kuwa yuko hai kutokana na kupanda na kushuka kwa kifua chake. Anapomtazama anaona anafanana na baba yake na pia anafanana na yeye. Huyu mzee anamwambia kuwa anajua anamtazama na kuwa hakuwa anamtegemea wakati kama huu na anamkaribisha. Msimulizi anasukumwa na kitu fulani kusema "*baba nimerudi*"( uk103). Baba anapotabasamu anafanana na kile kizee na huku amekasirika anasema kuwa msimulizi amezoea kumvunjia milango yake na kumharibia ndoto zake. Sasa anataka kuota tena kwa sababu amegundua kuwa mwisho wa ndoto lazima uharakishwe kwa kuota. Anataka kujua aliyemwonyesha msimulizi kwake . Mzee anaendelea kumwambia kuwa anachanganya kitambulisho chake na cha babake na kama si cha babake basi anarudi nyuma kwa babu na babu hadi kumfikia yeye. Anataka wasuluhishe jambo hili ili kila mmoja wao apate uhuru kamili.

Kadri anavyozidi kumtazama ndivyo anafafanana na kile kizee. Anaanza kusumbuliwa na wazo la kutokuwa na uhuru. Kitu kama chuki kinazuka moyoni mwake na anamwambia mzee kwa sauti kuwa yeye ni mwongo mkubwa na kila mahali aendapo anamkuta na anadai uhuru wake. Anamwambia kuwa amekuwa kama jiwe lililofungwa shingoni mwake. Naye mzee anasema mwongo ni msimulizi na wote wa aina yake. Anasema anataka uhuru wake kwani kila mahali anapohamia msimulizi anamfuata na anamnyima muda wa faragha. Anamwonya akome kumvunjia milango yake akiwa katika ndoto zake tamu. Anamwambia kuwa amemtafuta kanisani, msikitini, makaburini mbuyuni na hata ndani ya magofu. Anataka kujua shida yake ni ipi haswa kama sio umbea. Msimulizi anamwambia kuwa yeye ndiye anayestahili lawama kwa sababu amekuwa akimtii wakati huu wote na hana uvumilivu tena na ni lazima mmoja wao aondoke. Mzee anamwambia kuwa maneno yake ni ya hatari na anahofu kuwa siku moja angeweza kumuua. Anamuuliza ni kwa nini anatangaza vita wakati wa uzee wake badala angetoa majigambo wakati wa ujana wake. Msimulizi naye anamwambia kuwa na yeye ametangaza vita wakati wa vurumai zake. Anamwambia kuwa anatumia uzee kama njia ya kuwaminyaminya watu na msimulizi anataka kujua mzee anafanya nini nyumbani kwake. Mzee naye anadai kuwa hapa ni nyumbani kwake. Anataka kujua nyumba yake inastahili kuwa wapi kama sio hapa. Anamwambia msimulizi kuwa ni ujinga kung'ang'ania gofu ambalo lazima lianguke ili kipya kijengwe. Msimulizi anamwomba mzee aondoke katika kitanda cha baba yake na mzee anamwambia kuwa anakichanganya kitanda chake na cha babake. Anapoambiwa kuwa ataondolewa kwa nguvu anasema kuwa haondoki lakini alazwe vizuri upande wa kushoto ili aweze kuota juu ya utupu.

Msimulizi anapandwa na hasira na anamkaba mzee koo na kusema kwa kigugumizi kuwa atamuua. Mzee anakaa bila hewa na kuanza kufurukuta ingawa mwili wake hauna nguvu. Mwili wake unapoanza kufanana na wa babake, msimulizi anaachia vidole polepole na hewa inaanza kupitia kooni. Anameza mate na kwa sauti hafifu anaanza kuongea na kumwambia akamilishe ili mwisho uwe mwishowe na mwanzo mwanzowe. Anaponyamaza anamfukuza aondoke juu ya tumbo lake. Mzee anaendelea kumwambia msimulizi kuwa katika ujana wake aliumba mali halafu kutoka ndotoni akamteua msimulizi kuwa mshiriki wake. Naye Msimulizi akalewa hadhi na afya njema aliyotunukiwa na fikra zikamwotesha mbawa na sasa anamkaba koo. Msimulizi anaonywa asifikirie tena magofu lakini ajenge kipya bila kutegemea kuwako kwake kwani karne mpya imekuja.

Jua lilikuwa limewaka nje na msimulizi anapata nafasi ya kukiangalia kijiji. Baadhi ya nyumba ni imara ingawa zimezungukwa na majani na kuna vichaka hapa na pale. Baada ya kukizunguka anaamini kuwa hakuna mtu mwingine amesalia isipokuwa kile kizee, mwanamke na yeye. Anachuna ubuyu, wanakula na kuishi na mzee kwa muda. Sio rahisi kuishi naye kwani kila anapolala anahitaji kugeuzwa, kushikiliwa wakati wa kujisaidia, kuoshwa na kutolewa nje kuanikwa juani. Msimulizi anajiuliza sababu ya kufanya haya yote na anatoa wazo kuwa ampeleke aishi kanisani au msikitini wakati anapojenga kibanda kipya. Mzee anakataa na kumwambia kama amechoka kumhudumia aseme kwani huko hakuna mtu wa kumhudumia na yeye hataweza kufika kila siku. Anamwambia kuwa alikuwa akiishi huko lakini alipotea kwa sababu ya ubaridi. Msimulizi sasa hataki mjadala huu uendelee.

Mzee anamwambia jinsi alivyokuwa amekutana na kijana mmoja mbea kama yeye ambaye ametunga hadithi nyingi kumhusu za kuchekesha. Anasema huyu kijana ni mwizi mkubwa wa mawazo kwani yeye huchukua mawazo ya mzee na kuyatumia bila haki ya kunakili. Huyu kijana anajidai kuwa mwanasayansi na mvumbuzi mkubwa atakayeokoa ulimwengu wa binadamu. Mdomo wake hautulii mara hili mara lile na angemfunza adabu ila alikuwa na moyo wa huruma kama msimulizi. Anaendelea kusema kuwa anajiita mwanafalsafa na falsafa yenyewe haijui na maneno yake ni usaliti mtupu na kashfa. Mzee alikasirika lakini hasira zake za ndotoni huishia ndotoni. Sasa wanaheshimiana sana na msimulizi na wanaelewana fika. Msimulizi anaambiwa kuwa wakati utafika ambapo ataonyesha unyonge wake mbele ya ulimwengu.

Anapotaka kujua mahali msimulizi hutoa pombe kila siku anaarifiwa kuwa ni kanisani. Anamwambia kuwa amegeuza kanisa kuwa klabu na kwamba atafurahi wakati mvinyo huo utakwisha. Msimulizi anamsindikiza hadi kitandani na kumlaza upande wa kulia ili aweze kuota juu ya nafsi yake pekee. Anaendelea kuishi hivyo na mzee. Maisha yao yakawa ya kuambizana ukweli, kukaripiana, kuchekeana na kujadili yaliyokuwa mioyoni mwao. Mwishowe uhusiano wao unakuwa wa utani.

Siku moja akiwa nje aliona mawingu meusi yakizengea angani. Siku hiyo mvua ilinyesha usiku mzima hadi asubuhi. Hali hii ilieendelea kwa siku saba na udongo ukatepeta na arthi ikatitia. Magofu na nyumba za bloku zikaanguka na zingine kupata nyufa. Hii mvua ilitonesha uhai na majani ya kila aina, miti na maua yakaota. Mto ukafurika na chemchemi zinaanza kuchirizika maji safi. Wadudu na wanyama wadogo wanaanza kuonekana na usiku kukawa na milio ya kila aina. Moyo wa

msimulizi unajaa matumaini na kuwako kwa mzee sio mzigo tena kama hapo awali. Wakati huu mzee anaanza kupoteza uwezo wake wa kusikia na kuzungumza na macho yake yanaanza kuota ukungu lakini anaweza kuona kiasi.

Usiku mmoja wa mbalamwezi msimulizi anasikia kitu kikigongagonga dirishani. Analifungua na kulifunga bila kuweka kitasa ili aweze kulifungua haraka kwa sababu hakuweza kumwona aliyegonga. Anakazia dirisha macho na wakati huo anaona mkono mrefu mwembamba ukipitishwa dirishani toka nje. Mkono huu unatoa mwanga kama taa ndefu ya umeme. Anautazama kwa mshangao halafu chumba kizima kinajaa mwanga. Vidole vya mkono huu vinamwashiria atoke nje na sauti ya mnong'ono inamwambia asiogope. Anapotoka nje anamsikia mzee akikoroma na hakutaka kumharibia ndoto zake. Anamkuta mwanamke bila nguo amesimama, mwili wake wote unatoa mwanga na uzuri wake unaongezeka maradufu. Anatabasamu msimulizi anaposogea karibu lakini anapomkaribia anamkataza kwa mkono asisogee mbele tena. Anaambiwa hajawa na anaagizwa avue nguo zake zote azitumbukize chumbani mwake kupitia kwa dirisha. Anavua nguo zake na wanaanza kutembea kuelekea bondeni mwili wa mwanamke ukimulika njia.

Anaongozwa hadi bondeni karibu na mto na anafikishwa sehemu iliyokuwa ngeni kwake. Kuna chemchemi iliyotoa milizamu ya maji. Kisima kimezungukwa na mashina ya mti na majani yote katika sehemu hii yamekatwa vizuri kibustani.

Msimulizi anapomuuliza mahali hapa paliandaliwa na nani, anamwonyesha kifua chake kwa kidole. Anachukua sufuria iliyo karibu na kulijaza maji ya chemchemi na kulibeba hadi mahali wazi penye majani mororo chini ya mti. Anamwambia

Kenyatta University
Kiswahili Resource Centre

msimulizi ayaogee ili apate kuwa na akasimama pembeni huku akimsanifu. Msimulizi anatembea polepole kuelekea kwenye sufuria na maji haya yana joto yenye vuguvugu. Anaoga na anapojimwagia tone la mwisho mwili wake unaanza kung'ara kama wa mwanamke. Mwanamke kwa mara ya kwanza anamshika mkono na huku akitabasamu anamkaribisha katika upya wao ili waanze maisha mapya yenye hisia zilizochujwa na fikra pevu zilizokomazwa na wakati. Wanakumbatiana na kuwa kama taa mbili katika mwanga mmoja. Vifua vyao vinapoachana wanaongozana hadi kwenye msingi wa chemchemi. Wanakuwa kama sayari mbili zinazotoa mwanga usio na joto kuelekea umbali usiojulikana. Msimulizi anapotaka kujua au huyu ni yule mwanamke aliyekutana naye mara kwa mara mwanamke anamwarifu kuwa huyo mwanamke alikuwa mkewe aliyekufa miaka mingi iliyopita.

Mwanamke anamwarifu kuwa safari yao ni moja na walipoachana njia panda alichukua njia ya mkato na kuandaa makazi yao mapya. Wanapoenda kulala, mvua inaanza kunyesha baada ya muda mfupi na wanalala kama watoto yatima wasiokuwa na hatia wala dhambi ya asili. Wanapoamka mvua ilikuwa imeanza kukatika. Wanaenda kumjulia hali mzee kwenye gofu na wanapofika wanakuta kibanda chote kimeanguka. Huyu mwanamke anamwambia msimulizi asipate taabu kwa sababu mzee hawezi kuwa ameangukiwa na gofu alilojua siku zake za kuanguka. Wanapomtafuta kwenye mabaki ya gofu hawampati na wanamtafuta kanisani, msikitini na mbuyuni lakini hawamwoni. Wanakata tamaa wanapomkosa ndani ya magofu mengine na wanarudi nyumbani huku wakicheza na vijitunda vidogovidogo. Wanachoka na kuketi chini ya mti mmoja kupumzika. Mwanamke anakaa juu ya mapaja ya msimulizi na wanabadilishana wanapochoka. Wanaposimama wanaona nyuki maelfu wamekumbatiana kama furushi moja na wametulia. Mwanamke

anakimbia nyumbani na kuleta sufuria ya asali na asali inajaa haraka. Wanapoenda nyumbani nyuki wanawafuata lakini hawaumi na ni kama wanawasindikiza kwa nyimbo za mbawa zao. Wanapofika nyumbani wanakula asali na kupumzika kitandani huku wamekumbatiana. Wanaamka mchana kabisa na kwenda kwenye chemchemi na masufuria. Wanapofika wanacheza mchezo wa kumwagiliana maji. Baadaye wanachota maji moto na kukogeshana. Wanapomaliza wanakaa kwenye msingi hali wameshikana mikono wakitabasamu. Sasa ni kama wako *status nascendi;* wamezaliwa upya na ni tegemeo la taifa jipya la binadamu na wajibu wao ni kuhakikisha binadamu anabaki katika sura ya dunia. Kung'ara kwao kunamulika njia ya wakati ujao. Usiku wanasimuliana maafa yaliyopata ulimwengu lakini wanakubaliana maelezo yao kwa vizazi yaanzie kwenye chemchemi. Wanapoamka ndege wa asubuhi wanashangilia utukufu wao.

Asubuhi wanakata shauri kuvinjari mazingira yao. Huku wameshikana mikono, wanavuka bonde na kupanda kilima kilichokuwa na msitu mzito hadi wanaposhuka kuelekea kwenye bonde jingine. Upande mwingine wa kilima wanakuta ziwa dogo lenye maji safi. Upwa wake una mchanga mwingi na mweupe sana. Wanacheza mchangani na wanapochoka wanaanza kuimba wimbo mpya wa historia ya kuzaliwa kupya kwa karne. Wanafundishana wimbo kwa sauti zinazoingiliana vizuri na wanapochoka wanashikana mikono.

Wanapoanza safari ya kurudi nyumbani wanapotea njia. Wanapoona ndizi wanakula na baada ya shibe mwendo unakuwa mzito na giza linaanza kuingia. Hawafiki nyumbani kwa sababu ya kupotea njia na wanang'oa majani ya kujifunika. Wakiwa katika hali hii, ndege mmoja anatua kwenye mti uliokuwa karibu na kuimba;

*Utukufu ndani ya utukufu*

*Ni mimi mwimbaji mashuhuri*

*Ni mimi mwalimu wa kuruka*

*Na mwigo wa urembo*

*Heshima iliyoje kwangu*

*Kuongoza utukufu kama huu*

*Ni fuateni enyi mwanga wa mbalamwezi*! (uk119).

Anatangulia mbele akirukaruka toka mti hadi mti akiimba wimbo huohuo na wao wanamfuata gizani. Wanafika kwenye chemchemi, wanaenda nyumbani na kuchukua masufuria ya kukogeshana. Wanaukumbuka wimbo uliowaongoza gizani na hakuna chochote kinachoweza kulinganishwa na maisha haya kwani ni matamu mno. Wanakumbuka wema wa mzee na mwanamke anasema labda mzee yu hai.

Anamkumbusha msimulizi kuhusu vurumai zake wakati wa Ngoma Kuu. Anamwambia kuwa vurumai zake zimeishia kwenye ukingo huu wa amani ya kinjozi. Anaendelea kumwambia kuwa haya ni maisha baada ya vurumai na kuwa maisha yaliyokwisha yalianza hivi hadi kufikia vurumai. Maisha hayo yalianzia katika ndoto za mzee na yakawa mabaya zaidi lakini haya mapya yanaanzia katika ndoto ya utupu kwenye chemchemi na kuimarishwa na kutoweka kwake. Uzee wake uliruhusu kubomoka na kukataliwa kwa misingi iliyopita na sasa wana nafasi ya kuweka misingi mipya. Hii ndiyo sayansi isiyofuata ujenzi wa tofali juu ya jingine. Sasa wako paradiso mahali pa amani inayotokana na wao wawili. Wanabebana kuelekea nyumbani.

Mwanamke halali vizuri na hataki wakumbatiane. Mwishowe anasema makosa ni yaleyale na hawezi kupata usingizi kwa sababu huo hukuwa mwanzo mzuri. Anamwamrisha msimulizi waende kwenye chemchemi wakakoge.

Wanapofika anamwambia msimulizi kuwa mchwa ukikaribia kuangamia huota mbawa. Anapokosa kuelewa anaambiwa kuwa ataelewa wakati atakaposikia jinsi mkombozi wa pili wa kike alivyouawa. Anasimulia jinsi mkombozi wa pili alivyouawa na msimulizi anaposhikwa na usingizi anachukua sufuria, akalijaza maji na kumwambia aoge. Anamwambia ajitazame kwenye kifua chake na anaona alama nyeusi upande wa kushoto na sehemu hiyo ya mwili ilikuwa imeacha kutoa mwanga. Anapojimwagia tone la mwisho anaaza kung'ara tena na mwanamke anamkumbatia kwa furaha. Msimulizi anamhakikishia kuwa ajali nyingine haitatokea. Wanarudi nyumbani huku wamekumbatiana na mwanamke anamwambia walale na waote juu ya utupu na nafsi zao. Wanalala wamekumbatiana na wanasahau kufunga dirisha. Wanaamshwa na wimbo wa ndege yuleyule aliyewaongoza njia. Amesimama dirishani akisifia utukufu wao na anafanana na aliyekuwa kwenye njia panda.

Matunda ya kila aina sasa yameiva. Wanakula mengine na mengine wanachezea. Siku moja wanazunguka magofu na kuingia katika chumba ya Padri. Wanakizunguka chote isipokuwa chumba kimoja kilichokuwa kimefungwa. Wanavunja mlango na kupata kuwa kilikuwa maktaba ndogo na mlikuwa na vitabu vya kutosha. Vitabu vitatu vilikuwa juu ya meza na ni kama Padri alivitumia sana. Vitabu hvi ni Biblia, Kurani na Kamusi. Wanapumzika baada ya kupitia vitabu vyote. Mwanamke anasema kuwa vitabu hivyo havina maana kwao kwa sababu wao wametakasika na ulimwengu waliomo. Uchafu umeondolewa na mvua ilionyesha na kuondoa uchafu wote wa

nyuklia na kutu iliyozuia mioyo yao isidunde. Wao ni watu wapya ingawa wana kumbukumbu za ulimwengu uliopita.

Ili kumbukumbu hizi siziwatawale, wanavichoma vyote na wanabomoa magofu yote. Wanapobomoa kanisa msimulizi anakitafuta tena kile kitabu cha *Das Kapital* lakini hakioni. Baada ya kukamilisha kazi yao wanakubaliana kutotumia moto tena ili ujuzi huu usahaulike kabisa. Msimulizi anatoa wazo kuwa wafaa waanzishe lugha mpya na mwenzake anakubaliana naye. Hii ni lugha ambayo haina cha mtu na kitu, haina maneno kama '*nyuklia*' na '*vita*'.Wanataka kuunda lugha ambayo misingi yake ni kuwako. Wanaishi hivyo hadi siku moja wanaposikia mlio wa simba bondeni karibu na mto. Mwanamke anasema waende wakawalaki kwani wanyama wamerudi katika upya wao. Wanakimbia bondeni na katika jua la machweo wanaona wanyama wote wakiwa pamoja wakila majani hata chui na simba. Twiga na ngamia wanatazamana kwa tabasamu. Simba na Kifaru wanapimana nguvu na wanyama wadogowadogo wanachunga pembeni. Wanatembea bila uoga huku wakiwapapasa manyoya. Wanafurahia uzuri wa wanyama hawa. Mwanamke anamwonyesha kwa mkono wake juu kilimani na wanaona watoto wawili wamekaa. Wanakaa kama wachungaji wakiwa uchi na wanang'ara kama wao. Wanyama wanajitolea kuwapeleka hadi juu ya kilima. Wanapowafikisha kilimani wanarudi bondeni mbio. Wanatazamana na ni dhahiri kuwa hawa watoto ni mapacha, wa kike na wa kiume. Msimulizi anapowatazama, mwanzoni wanafanana na mzee. Anapowatazama mara ya pili anaona wao ni kama yeye na mara ya tatu wanafanana na mwenzake. Wanatazamana wote wanne na kukumbatiana hali wakitabasamu. Wanapomaliza wanasimama mmoja akitazama kaskazini na mwingine kusini na mmoja akitazama mashariki na mwingine magharibi. Kwa pamoja wote wanainua mikono yao juu kama ishara ya

amani. Panakuwa na mianga minne juu ya kilima inayomulika pande zote za dunia. Msimulizi anapotazama chini ya kilima anaona mzee akitambaa polepole kwa magoti huku amebeba kitabu na wanyama wote wanacheka.

**4.2 MAANA YA ANWANI**

Neno *Mzingile* linaashiria dhana ya jambo lisilokuwa na mwanzo wala mwisho bayana. (Chuachua 2010) katika kufafanua neno hili anasema, neno *Mzingile* linasawiri *mkanganyo* au *utata* fulani. Katika riwaya ya hii, Kezilahabi ametuchorea picha ya kusongwasongwa kifikra kunakotokana na kutofahamu chanzo na mwisho wa maisha. Sehemu ya mwisho ya riwaya ya *Mzingile* ni kana kwamba inatoa suluhisho kuhusu matatizo yanayomkumba mwanadamu ulimwenguni, hivyo kuleta amani. Safari katika riwaya hii inaonyesha hali ngumu na vikwazo za kimaisha anavyokutana navyo mwanadamu.

Kulingana na Madumla na Mlacha (1995), Kakulu ni mhusika jumai; ni wahusika wengi ndani ya mmoja Mhusika wa aina hii amejitokeza kwa mara ya kwanza katika riwaya ya Kiswahili kupitia riwaya za Kezilahabi *Nagona* (1990) na *Mzingile* (1991). Mhusika huyu amechorwa kama mtoto, mzee, kiongozi mungu na yuko kila mahali.

Riwaya ya *Mzingile* inaweza kufasiriwa kama hadithi inayohusu utafutaji wa maana ya maisha. Kutambua mahali pa kuweka riwaya ya *Mzingile* (1991) katika kazi za Kezilahabi huleta taswira ya mwendelezo wa riwaya ya *Nagona*(1990).

Riwaya ya *Mzingile* ni riwaya pacha na riwaya ya *Nagona* kwa kuwa zote zimeandikwa na mtunzi mmoja katika kipindi kisichozidi miaka miwili na zinafanana

sana kifani na kimaudhui. Hata hivyo,utafiti wetu umeonelea ni muhimu kuchambua riwaya hizi kila moja wakati wake kwa sababu hizi ni riwaya mbili tofauti kulingana na mwandishi na pia kulingana na wakati zilipoandikwa, *Nagona* (1990) na *Mzingile* (1991).

Mzingile ikiwa na maana ya matata mengi au mchanganyiko wa mambo inaonyesha ukweli wa jina hili. Kezilahabi haonyeshi tu safari iliyopinda lakini anatoa taswira ya umbo la utungo wake kulingana na maudhui mbalimbali. Karibu katika kila sura Kezilahabi anabadilisha mtazamo wa masimulizi yake na anaachia hadhira yake kujua ni wakati upi katika wendo wa hadithi anafafanua. Ni dokezo dogo tu limetolewa ili kuangazia maana yake yote na kuongoza msomaji katika mchanganyiko huu.

Riwaya ya *Mzingile* ina ngano, hadithi ya mafumbo, ubunifu wa sayansi na utaratibu wa uhalisia (Gromov 1998). Katika mtazamo mpana Wamitila anatoa wazo kuwa *Mzingile* ni riwaya ya metafizikia ikilinganishwa na kazi zake za hapo awali. Katika muktadha huu metafizikia ni kujihusisha na jambo lililoko katika ng'ambo ya pili au mbele , jambo lililo kule au huko lililopita uhalisia wa dunia. Kezilahabi amefuata njia ya kifalsafa kuonyesha utafutaji na maana ya maisha lakini anatumia dunia halisi kueleza mtazamo wake wa kifalsafa.

Kuna mipango ya mitindo mbalimbali katika riwaya hii. Mpango wa kwanza ni ule wa sanaa ya jadi. Hii ni kwa sababu Kezilahabi ametumia elementi za elimu na mila za jamii ya Kiafrika kutoka dhana za mithiologia hadi misuko ya ngano. Mithiologia anayotumia Kezilahabi ni kutoka kwa jamii yake ya Wakerewe. Isitoshe, riwaya hii imejaa taswira za mithilogia kutoka kila sehemu ulimwenguni kwa mfano, maisha kusawiriwa kama mkufu , ujuzi kama mwanga na mengine mengi.

Mtindo wa pili wa riwaya hii ni ule wa hadithi ya mafumbo na mtindo wa sayansi, jamii ya kufikirika na kutofikirika au uhalisia. Mitindo hii yote imesukwa pamoja huku ikileta mkusanyiko unaotatiza.

## 4.3 FUMBO LA UHAI NA KIFO

Uhai na kifo ni mambo yanayomtatiza sana Mwafrika. Dhana hizi zimesawiriwa vyema katika riwaya ya *Mzingile*. Waafrika ni watu wanaothamini sana uhai na kukihofia kifo. Jambo linalotishia uhai linapotokea mwafrika hufanya kila jitihada kuliepuka. Majanga yanayotishia uhai pamoja na matukio yanayotokea ni mambo ya ajabu ambayo sio rahisi kuaminika katika ulimwengu halisi.

Maudhui ya uhai na kifo yameendelezwa katika riwaya ya *Mzingile* kama yalivyoendelezwa katika riwaya ya *Nagona*. Mwandishi ametumia ishara mbambali kimafumbo ambazo ni za ulimwengu wote. Kazi hii imesheheni taswira, ishara, na mafumbo mbalimbali ili kuleta maudhui haya miongoni mwa mengine. Riwaya ya *Mzingile* imesawiri maisha katika mtazamo wa dhihaka na kejeli kwa kutumia mtindo wa uhalisiamazingaombwe. Mwandishi katika riwaya hii anayaona maisha kama duara. Senkoro (1995) anasema kuwa Kezilahabi anayaona maisha katika mzunguko ambao jana na leo huunganishwa na kesho haipo kwani leo hujengwa katika msingi wa jana. Dhana ya uhai na kifo imesawiriwa kupitia ishara mbalimbali katika riwaya ya *Mzingile*.

## 4.4 ISHARA

Hizi ni picha au taswira anazopata msomaji wakati wa kuisoma kazi yoyote ya fasihi. Riwaya ya *Mzingile* imesheheni taswira mbalimbali ambazo zinafafanua zaidi dhana

ya uhai na kifo katika jamii. Baadhi ya ishara ambazo Kezilahabi ametumia ni pamoja na;

### 4.4.1 ISHARA YA MWANGA

Kulingana na nadharia ya kikale, mwanga huashiria hali ya matumaini, nuru na kufanya upya. Mwandishi anasema,

> *"Ulimwengu unahitaji mwanga mpya!" Kichaa alipiga kelele na kisha akaongezea, "lakini hiyo haitakuwa kabla ya uharibifu na maafa !"Tulikuwa kilabuni tukinywa pombe. Watu walicheka. Mimi pia nilicheka, lakini maneno yake yaliamsha ari ya kutaka kujua asili ya mwanga. Nilitazama sayari na nyota nikafurahia wingi wake usiotoa joto. Halafu nikafikiria jua na sayari zinalolizunguka daima* (uk 8).

Ulimwengu unahitaji kupata nuru na matumaini mpya. Yale ya zamani yanahitaji kusahaulika kabisa na kuanza ulimwengu mpya usiokuwa na maafa na maovu mbalimbali. Uhai katika ulimwengu hauna mwisho kwani unafananishwa na sayari. Ni duara na duara haina mwanzo wala mwisho. Kwaa makabala wa nadharia ya Kikale Kezilahabi anasema,

> *Nyimbo za ndege wachache ziliniamsha asubuhi. Kulikuwa na uhai mahali fulani katika msitu. Ndani ya nyumba kulikuwa na mwanga wa kutosha sana. Nyumba yenyewe ilikuwa gofu lililokuwa na kuta mbovu na mashimo kila mahali. Mashimo hayo mabovu ndiyo yalipitisha mwanga mwingi* (uk 101).

Mwanga hapa unaashiria uhai na matumaini. Nyumba yenyewe ni gofu lakini bado kuna uhai katika ile nyumba kwani uhai hauna kikomo. Ule ubovu wa nyumba na mashimo ndiyo unaleta mwanga mwingi hivyo wafu ndio huleta uhai wa milele. Uhai unapatikana kila mahali.

### 4.4.2 ISHARA YA MZEE

Kwa mujibu wa nadharia ya Kikale, Carl Gustav Jung anasema kuwa huyu ni mhusika wa kutathmini, ana mawazo, ujuzi, utambuzi, hekima na uwezo wa kuhisi mambo haraka. Ana ukarimu na huwa tayari kusaidia kila wakati. Sifa zake za "kiroho" zinadhirishwa na mambo haya yote. Huyu mzee kulingana na nadharia ya Kikale ana uwezo wa kuonyesha jambo la asili linalotatanisha kama uhai na kifo. Msimulizi anasema,

> *Yasemekana Kakulu alipojiona mzee aliwateua wazee watano, mmoja kutoka kila kijiji. Huko alikaa nao kwa muda wa mwezi mmoja, aliwafunza historia, Mila na desturi, dawa, unajimu na mengine mengi. Alipoona wamekomaa aliwaongoza hadi chini ya mlima mkubwa. Alipanda nao hadi kwenye kilele cha mlima. Kwa mara ya kwanza wakaiona nyumba yake ndogo. Wakiwa juu mlimani aliwaonyesha kwa fimbo yake nchi iliyokuwa chini* (uk5).

Huyu ni mzee mwenye hekima, anawafunza wazee wengine historia ya jamii yao pamoja na mila na desturi ambazo zinafaa kufuatwa. Pia anawashauri kuhusu mambo mbalimbali kuhusu maisha na jinsi ya kulinda nchi yao. Mzee anabaki kuwa tegemeo la watu wa kijiji hiki na wanaanza kumtolea sadaka ili awaletee mvua hivyo mavuno mengi. Mwishowe, anabakia kuwa kisasili na anaishi katika jamii yao daima. Mzee ni mhusika mwenye uwezo wa kuhisi jambo haraka na kila wakati yuko tayari kusaidia. Kwa mkabala wa nadharia ya Kkikale Kezilahabi anasema,

> *Nilipomkaribia nilimwona akitega sikio moja upande wangu. Nilipomwangalia vizuri niliona alikuwa kipofu. Alikuwa ameshikilia fimbo yake mkononi. Alipoacha kusikia hatua zangu alisema, "Najua umesimama na unanitazama. Mimi ni mboni kati ya giza na mwanga . Nilikuwa sukutegemei wakati huu. Umefika mapema kidogo. Mwendo wenu ulikuwa wa kasi sana"* ( uk43).

Hata kama mzee amepoteza uwezo wake wa kuona, anamhisi msimulizi na anajua analofanya. Hata anapokuwa mkongwe bado anajua ya kwamba ana jukumu la kuongoza jamii yake. Mzee anawakilisha mambo yaliyofichika na ya kukata tamaa na yeye ni mboni kati ya matumaini na kuzaliwa tena. Fimbo anayotumia mzee ni dira ya kuongoza jamii yake.

### 4.4.3 ISHARA YA MAJI

Kwa mujibu wa nadharia ya Kikale mithiolojia kutoka Afrika zinasema kuwa dunia ilikuwa ziwa kubwa na uhai ulitoka hapa. Kulingana na nadharia ya Kikale, maji ni sitiari ya uhai na hivyo maisha. Ni ishara ya uumbaji, kufa na kuzaliwa tena. Jung anasema kuwa maji ni ishara ya mtiririko wa mpito wa wakati milele. Msimulizi anasema,

> *Uogaji wangu haukuwa kama wa ndege. Sikuwa na haraka maana sikuwa najua umbali wa kule nilikokuwa nakwenda na sikujua ningefika lini. Baada ya kuvua nguo zote nilijitumbukiza majini, nikajinyoosha kwa muda hadi mapafu yalipohitaji hewa tena. Nilipotoka majini nilisugua mwili mzima kwa mchanga mwororo.*
>
> *Nilijitumbukiza tena majini, nikaondoa uchafu uliokuwa umekokomolewa na mchanga. Nilijisikia mtu mwenye nguvu mpya. Nilikaa majini kwa muda* (uk12).

Maji ni ishara ya uhai na msimulizi anawakilisha mwanadamu. Hana haraka ya kutoka katika maisha halisi ya hapa duniani na kuanza mengine mapya. Mwanadamu anapokosa nguvu na kufa hatimaye anapata uhai lakini katika umbo lingine kupitia ishara hii ya maji.

Jung anasema ni mabadiliko ya muhula mzima na kupata umbo la uungu. Kwa mkabala wa nadharia ya Kikale msimulizi anaendelea kusema,

*Baada ya mto hakuna kitu kingine isipokuwa kina cha fikra safi katika upweke. Umekwisha ingia katika duara. Karibu!* (uk 14).

Mwanadamu anapokufa anaanza maisha mapya ambapo ni tofauti na maisha ya watu wa dunia halisi. Anakuwa ameingia katika duara la uungu.

### 4.4.4 ISHARA YA MWANAMKE

Kwa mujibu wa nadharia ya Kikale, mwanamke huashiria fumbo la uhai, kifo na mabadiliko. Katika riwaya ya *Mzingile* kuna mwanamke mwenye nafsi na nguvu zote. Huyu mwanamke ana uzuri wa kifalme na ni mrembo. Katika Jungian *anima,* (Stevens 1999) anasawiri mwanamke kama kiumbe chenye umbo la binadamu lenye ufunuo au uungu. Kezilahabi anasema,

*Siku chache baadaye nilijiona nashuka ngazi zilizoteremka chini kwenda mahali nilifikiri kulikuwa na chemchemi. Mbele yangu kulikuwa na mwanamke ambaye alikuwa na debe tupu. Watu tuliongezeka kadri tulivyoshuka ngazi. Kulikuwa na taa za umeme zilizomulika njia. Tulipofika chini kulikuwa na uwanja uliokuwa umejaa watu, wanawake kwa wanaume. Tulianza kuvua nguo na kuanza kuoga maji yaliyomwagika toka juu kama mvua. Sote tulipiga kelele."Wokovu!" Ghafla nilijiona sina vidole vya mguuni, halafu vya mkononi pia vikadondoka. Nilipowatazama wale wengine, wao pia hawakuwa na vidole. Nilipojaribu kujisugua mwili nilibandua ngozi na nyama yake. Mifupa ya mikono yangu ilianza kuonekana. Sote tulikuwa mifupa iliyosimama na kutembea. Tuliogopana, tukaanza kukimbia ovyo na kugongana.....Niliona watu waliokuwa na michirizi ya machozi*

*wamenizunguka. Kulikuwa na shimo karibu nami. Baadhi ya watu walikuwa wameshikilia mchanga viganjani mwao wakinitazama kwa mshangao mkubwa* (uk30-31).

Mwanamke ni kiumbe ambacho kina uwezo wa kujaza ulimwengu. Hata kama hapo mwanzoni yeye huwa peke yake, ana uwezo wa kujaza dunia kwa kupata wanadamu wa jinsia zote hivyo yeye ni chanzo cha uhai na bila yeye wanadamu hawangekuwepo. Pia kutokana na dondoo hili ni dhahiri kuwa kuna uhai baada ya kifo. Wanaokufa wanaendelea kuishi katika umbo linguine na matendo yao ni kama ya wanadamu halisi. Waliokufa ni viumbe vikamilifu kama watu waishio maisha halisi hapa ulimwenguni. Kwa mujibu wa nadharia ya Kikale Kezilahabi anasema,

*Tuanze misingi mipya! Ni kichaa, kipofu, mwotaji na mwanamke wawezao kuvunja misingi hii mibovu! Wao ndio watakaowavusha walimwengu katika mito na milima! Mbele ya utashi hakuna lisilowezekana!* ( uk34).

Mwanamke ana uwezo kuliko kiumbe chochote kingine duniani. Anaweza kuumba na kuumbua hivyo kuvusha mwanadamu hadi ng'ambo ya pili ambako hakuna kingine isipokuwa utashi ambapo mwanadamu huongozwa na hamu kubwa ya kutaka kujua kitu fulani. Mwanamke anawaelekeza njia wanaopatwa na mambo magumu maishani na pia waliopotea.

### 4.4.5 ISHARA YA GIZA

Kwa mujibu wa nadharia ya Uhalisiamazingaombwe, giza huwakilisha vurumai, fumbo, mambo yaliyofichika, kifo, ushahidi wa hekima, kutojifahamu, uovu, na huzuni. Msimulizi anasema,

*Nilipoamka kulikuwa bado na giza. Nililala tena. Nilipoamka giza lilikuwa bado kutoweka. Usingizi ulipokwisha hali ya giza ilikuwa ya kutisha. Katika giza hilo nene niliendelea kugonga. Nilianza kuwa na wasiwasi kama giza litakwisha na mwanga kutokea tena. Niliendelea kugonga bila kukata tamaa. Wakati ulipita. Mwishowe mlango ulianza kulegea* (uk18).

Giza hutisha na huogofya kwa sababu ni mambo mengi yanayoweza kufanyika wakati kama huu lakini hatimaye mwanga hupatikana. Msimulizi ana matumaini kuwa giza litakwisha na ataweza kumwona mwenye nyumba iliyokuwa imejengwa juu ya mwamba.

### 4.4.6 ISHARA YA RANGI NYEUSI

Vazi jeusi kulingana na nadharia ya uhalisiamazingaombwe, linawakilisha fumbo la kuweko kwa mwanadamu. Katika jumba ambalo wanaume wameenda kuburudishwa na wasichana wachanga, onyesho la mwisho linachezwa na Afrika, kwa mkabala wa nadharia ya uhalisiamazingaombwe, anatwambia holi zima linapata kichaa hata kabla hajaingia anasema,

*Alivaa vazi jeusi toka blauzi hadi kiatu. Muziki wa kuingilia ulipolia aliingia kwa utaratibu bila kucheza. Alishika kipaaza sauti na kwa sauti nyororo akasema.*

*"Mimi ni mwanzo na mwisho wenu. Mlikuja kupitia kwangu na mtaondoka kupitia kwangu. Kunivunjia mimi heshima ni kunivunjia heshima ya utu wenu. Mimi ni tumaini la mwisho la heshima, utu na uhai wa binadamu"* (uk73).

Hakuna anayejua Afrika atacheza rekodi gani; ni yeye tu anayejua. Vivyo, hivyo mwanzo na mwisho wa mwanadamu umezingirwa na rangi nyeusi au giza na hakuna

anayejua linalofanyika kabla na baada ya kufa, ni fumbo kubwa kwa wanaoishi katika ulimwengu halisi.

### 4.5 HITIMISHO

Sehemu hii imebainisha matumizi ya ishara mbalimbali katika kusawiri dhana ya uhai na kifo katika riwaya ya *Mzingile*. Uchanganuzi umeonyesha kuwa hata kama uhai wa mwanadamu hufika kikomo hapa ulimwenguni huo sio mwisho wake kwani anaendelea kuishi tena katika umbo lingine. Kezilahabi ametumia ishara hizi kufafanua fumbo linalotatanisha jamii mbalimbali ulimwenguni. Hili ni swala kuu linalowatatanisa wanadamu kote ulimwenguni. Mwandishi katika riwaya hii amefafanua kuwako kwa maisha ya mwanadamu kabla na baada ya kifo.

Baadhi ya ishara zinazojitokeza katika riwaya ya *Mzingile* ni ishara ya mzee, mwanga, mwanamke, giza na rangi nyeusi. Maudhui mengine katika riwaya ya *Mzingile* ni kama vile, siasa, teknologia mpya, ushirikina miongoni mwa mengine.

Sura itakayofuata tumejadili mhutasari wa utafiti, changamoto za utafiti, mapendekezo ya utafiti, mchango na matokeo ya utafiti. Aidha tumetoa mapendekezo ya utafiti unaoweza kuendelea kufanywa katika uwanja huu wa riwaya za Kiswahili.

# SURA YA TANO

# HITIMISHO, MATOKEO NA MAPENDEKEZO

## 5.0 UTANGULIZI

Katika sura zilizotangulia tumechunguza jinsi dhana ya uhai na kifo inavyofasiriwa ulimwenguni kote na hatimaye ufasiri katika riwaya teule. Katika sura hii tumejadili muhtasari wa utafiti wetu, changamoto tulizopitia, mchango,mapendekezo ya nini kifanyike katika tafiti zijazo na maoni ya jumla kwa wataalamu wa fasihi.

Utafiti huu umechunguza dhana ya uhai na kifo katika riwaya ya *Nagona* na *Mzingile* kupitia ishara mbalimbali kama vile, ishara ya mzee, ishara ya mwanamke, ishara ya mwanga ishara ya duara, ishara ya giza ,ishara ya msitu na ishara ya rangi nyeusi.

## 5.1 MUHTASARI WA UTAFITI

Tasnifu hii imegawanywa katika sura tano. Katika sura ya kwanza tulifafanua istilahi, usuli wa mada, ufafanuzi wa suala la utafiti, sababu za kuchagua mada, nadharia zilizotumika pamoja na njia za kukusanya na kuchanganua data. Katika sura ya pili tulijadili maisha, uandishi na tajiriba ya Kezilahabi na jinsi alivyoathiriwa na falsafa mbalimbali.

Sura ya tano imeonyesha majumuisho ya ripoti yote ya utafiti, Sura ya tatu na ya nne ndizo zimebeba kiini cha utafiti wetu kwani data tulizokusanya zimewasilishwa hapa na matokeo ya utafiti kujadiliwa kwa kina. Sura ya tatu imechanganua riwaya ya *Nagona* na ya nne riwaya ya *Mzingile*. Mwisho wa sura ya tano tumeorodhesha marejeleo.

Utafiti umebainisha kuwa neno "*Nagona*" si la Kiswahili bali limetokana na lugha ya kwanza ya mwandishi. Kwa ujuzi na uzoefu aliokuwa nao mtafiti, *Nagona* ndiye "*paa*" aliyekuwa akisakwa na mhusika mkuu "*Mimi*" katika riwaya nzima. Huyu *paa* sio mnyama bali ni binadamu msichana. Aidha, tuliona kuwa neno *Nagona* linasawiri dhana ya ukweli kuhusu maisha. Mwandishi anasema kuwa ukweli umejificha mahali palipo wazi na hivyo mwanadamu lazima atapitia mitego midogomidogo kuufikia ukweli huo. Mwandishi katika riwaya ya *Nagona* ametumia ishara zilizobainika ili kuzisawiri falsafa alizosomea katika ulimwengu halisi, kujipambanua kipekee kifasihi na kufafanua dhana ya kuwako kwa maisha baada ya kifo.

Mhusika "*Mimi*" ametumika kueleza asili ya kuwepo kwa wanadamu ulimwenguni. Katika kujaribu kueleza dhana ya chanzo cha kuwako kwa watu, mwandishi ametumia hadithi moja ya "hadithi kuu" ipatikanayo katika Biblia ya Adamu na Eva ambao waliishi katika utupu. Wakati "*Mimi*" anazungumza na babu yake, mwandishi anajaribu kueleza asili ya kuwako kwa wanadamu katika uso wa dunia.

Safari katika riwaya ya *Mzingile* imetumika kama ilivyotumika katika riwaya ya *Nagona*. "*Mimi*" anapitia vikwazo na changamoto kadha wa kadha zinazosawiri changamoto katika maisha halisi ya mwanadamu. Hii ina maana kuwa maisha yamejaa vikwazo ambavyo lazima mwanadamu afaulu ili aweze kufikia maisha mapya. "*Mimi*" katika riwaya ya *Nagona* anasafiri kumsaka paa (Nagona) ambao ni ukweli katika maisha na katika *Mzingile* alikuwa safarini kupeleka taarifa kuhusu kifo cha mtoto wa mzee.

Kakulu katika riwaya ya *Mzingile* ni mhusika jumai ambaye ni wahusika wengi ndani ya mmoja. Mhusika jumai amejitokeza kwa mara ya kwanza katika riwaya ya Kiswahili kupitia riwaya za Euphrase Kezilahabi *Nagona*(1990) na *Mzingile* (1991) Mlacha na Madumulla (1991). Huyu mhusika amechorwa kama mtoto, mzee, kiongozi ,Mungu na yuko kila mahali kila wakati wowote ule. Riwaya ya *Nagona* na *Mzingile* ni riwaya fupi lakini tata kuliko riwaya zote ambazo ziko katika ulingo wa fasihi ya Kiswahili. Ni riwaya zinazomtaka msomaji sio tu kutafakari, bali awe na usuli wa falsafa na misingi ya nadharia fulani za kifasihi (Madumla 1993).

Utafiti huu pia umegundua kuwa mwandishi wa riwaya hizi ameathiriwa sana na Shaaban Robert ambaye ni gwiji wa fasihi ya Kiswahili. Aidha, maudhui katika riwaya ya *Siku ya Watenzi Wote* (1968) ya Shaaban Robert imemwathiri mwandishi wa riwaya ya *Nagona* na *Mzingile* kwa kiasi kikubwa. Kezilahabi ameleta mabadiliko katika fani na pia maudhui katika uandishi wake. Katika riwaya hizi mwandishi ametumia ishara na taswira nyingi sambamba na sitiari kuu ya safari ambayo ndiyo mwimo wa hadithi. R. Chuachua (2010) amejadili taswira hizi na ameangalia kufanana na kutofanana kwa maudhui kati ya Shaaban Robert na Kezilahabi. Ameangalia pia jinsi Shaaban Robert amemuathiri Kezilahabi katika ujenzi wa taswira.

Kezilahabi amefanikiwa kwa kiasi kikubwa kwani riwaya zake za mwanzo kama vile *Rosa Mistika* ziliandikwa ili zisomwe na watu wa kada zote lakini riwaya ya *Nagona* na *Mzingile* ziliandikwa ili zisomwe na wasomi wa elimu ya juu tena waliobobea katika fasihi. Mwandishi amefanikiwa kugawa hadhira yake na kila moja hupata maudhui kulingana na kiwango cha taaluma na uelewa wake.

## 5.2 CHANGAMOTO ZA UTAFITI

Riwaya za *Nagona* na *Mzingile* ni kazi za majaribio kwa sababu hazina mtiririko wa matukio ambayo msomaji anaweza kuyafuata tangu mwanzo hadi mwisho na vimejengwa kwa visa vya kiajabuajabu ambavyo havishikamani kiploti. Mtririko na msuko unaopatikana katika riwaya haupo katika riwaya ya *Nagona* na *Mzingile*. Mandhari ipo nje ya ulimwengu tunaoufahamu. Hali hii inaifanya riwaya hizi ziwe ngumu kueleweka. Mandhari halisi husaidia kufahamu jamii iliyoandikiwa na hivyo kung'amua maudhui kwa urahisi.

Masimulizi ni kupitia vijihadithi vifupivifupi ambavyo havina uhusiano wa moja kwa moja, hivyo inakuwa vigumu kupata ule mwendelezo wa hadithi. Pia wakati katika riwaya hizi umerudishwa nyuma sana kabla na baada ya mwanadamu kuwepo katika uso wa dunia na pia umesukumwa mbele sana ambapo binadamu anayeishi katika ulimwengu halisi hawezi kufikia kabla ya kufa. Kigezo hiki cha wakati kufanywa *kale-kesho* kilidhihirisha ugumu huu. Isitoshe, riwaya hizi zimejaa fantasia na falsafa na ni kama riwaya moja kwa sababu riwaya ya *Mzingile* ni mwendelezo wa hadithi katika riwaya ya *Nagona* lakini utafiti wetu ulizichukulia kama riwaya mbili tofauti.

Mtafiti amekumbana na masuala kadhaa yaliyopunguza mwendokasi wa ukamilishaji na mchakato wa utafiti na hatimaye uandishi wa ripoti. Masuala haya ni pamoja na ugumu wa kupata marejeleo faafu maktabani hivyo mtafiti alipotoka mara kadha wa kadha. Pia, sababu za kibinadamu kama vile hali ngumu ya kiuchumi zilididimiza mwendo wa mtafiti.

Changamoto hizi zimekabiliwa kwa njia tofauti kulingana na wakati, rasilimali na uzito wake. Kwa mfano, suala la kukosa marejeleo faafu yaliyo katika maunzi ngumu lilitatuliwa kwa kupanua eneo la utafiti. Tumetumia mtandao na hivyo kuweza kupata marejeleo kutoka makavazi mbalimbali ya idara za Kiswahili. Pia wahadhiri wasaidizi walinipa moyo kwa kuniongoza vilivyo.

## 5.3 MCHANGO WA UTAFITI

Mchango mkuu wa utafiti huu ni kutoa mapendekezo yatakayoongoza washikadau wa fasihi ya Kiswahili. Aidha, kutokana na matokeo, utafiti umedhihirisha kuwa kifo sio mwisho wa uhai. Isitoshe, wasomi wa riwaya za Kiswahili watapata mwelekeo mpya kuhusu dhana ya uhai na kifo. Utafiti umepata mtazamo mwingine tofauti kuhusu dhana ya uhai na kifo. Mchango mwingine wa utafiti huu ni kuwa hakukuwa na kazi iliyoangazia dhana ya uhai na kifo jinsi utafiti huu umefanya. Utafiti huu kwa hivyo ni miongoni mwa kazi za kwanza za E.Kezlahabi za hivi karibuni.

Utafiti huu utakuwa wa manufaa kwa watakaopenda kuzungumzia kazi nyingine za mwandishi huyu. Utafiti pia umeshirikisha nadharia mbili za uhalisiamazingaombwe na vikale na hivyo kubainisha namna zinavyoweza kuhakiki utanzu wa riwaya.

## 5.4 MATOKEO YA UTAFITI

Utafiti umebainisha kuwa maisha ya mwanadamu sio mstari mrefu ambao una kikomo bali maisha ya mwanadamu ni mviringo; ni duara. Mwanadamu anapokufa haangamii lakini anaendelea kuishi katika umbo lingine ambalo linajumuisha maisha matamu yasiyokuwa na matatizo ya dunia halisi. Kwa hivyo kutokana na utafiti huu

maisha ya mwanadamu hayana mwisho na wakati anapotoweka kutoka ulimwengu halisi anaanza maisha mapya.

Riwaya hizi zimelijadili swala gumu kuhusu kweli kamilifu ambayo imo katikati mwa duara ya maisha. Pia, zina miketo ya kifilosofia, dini, saikolojia na maneno ya mitume. Miketo hii imepachikwa kimbambizoviraka.

## 5.5 MAPENDEKEZO

Baada ya kukamilisha mchakato wa utafiti na mjadala juu ya data zilizokusanywa kuhusiana na tatizo la utafiti, mtafiti ameona ni vyema kufanywa kwa tahakiki ya riwaya ya *Nagona* na *Mzingile* kwa kiwango cha kuweza kusomwa na kueleweka na wengi ili kuweza kuongeza idadi ya wasomaji na hivyo kuwezesha ujumbe kuwafikia wengi. Hii ni kwa sababu wanaosoma riwaya hizi na kuzielewa ni wataalamu wa fasihi pekee.

Tulikitafiti kipengele cha uhai na kifo pekee kwa sababu ya wakati na malengo yetu. Kuna vipengele vingine ambavyo vinahitaji utafiti kama, kimya cha usomaji,usimulizi katika riwaya ya *Nagona* na *Mzingile*, wahusika, unafiki, mapinduzi na vurumai baadhi ya vingine na vyote viahitaji utafiti wa kina

## 5.6 HITIMISHO

Utafiti huu kwa jumla umejikita katika kutafiti na kujadili fumbo la uhai na kifo katika riwaya za Prof. Euphrase Kezilahabi *Nagona* na *Mzingile*. Utafiti huu kwanza umeonyesha jinsi dhana ya uhai na kifo imefasiriwa katika jamii mbalimbali ulimwenguni. Aidha, utafiti huu umeonyesha maudhui ya dhana ya uhai na kifo katika riwaya teule na umeyajadili kwa kina kupitia taswira mbalimbali..

**MAREJELEO**

Abrams, M. (1993) *A grossary of Literary Terms.* Fort Worth. HBS.

Alembi, E. (2003). *The Oral Poetry of the Abanyole Children: Context,Style and Social Significance*. Tatu.

Barley, N.(1997). *Grave Matters. A Lovely History of Death Around the World.* New York. Henry Holt and Company.

Bertoncini,E.(1989). *Outline of Swahili Literature. Prose Fiction and Drama*. Leiden: Brill.

Bertoncini, E. (1992). "*Stylistic Approaches to E. Kezilahabi's Novels and Poetry*" APP 31:5-6

D'Haen, T.(2005). *Magic Realism and Postmodernism .Decentering Priviledged Centers*. London. Duke University Press.

Gromov, M.(2002). *Postmodernist Elements in Recent Swahili Novels*. Nairobi. (Hakijachapishwa)

Kezilahabi, E.(1974). *Kichwamaji.* East Africa Publishing House. Dar es Salaam.

__________(1975). *Dunia Uwanja wa Fujo*. Dar es Salaam.East Africa Literature Bureau.

__________ (1979). *Gamba la Nyoka*. Arusha. East Africa Publishing House.

__________ (1981). *Rosa Mistika.* Nairobi.Kenya Literature Bureau.

__________(2011). *Nagona*. Dar es Salaam. Dar es Salaam Press.

__________(2011). *Mzingile*. Dar es Salaam, Dar es Salaam University Press.

Khamis, S. (2003). *Fragmentation, Orality and Magic Realism In Kezilahabi's Novel Nagona* In Nordic Journal Of African Studies.

Khamis, S.(2007).*Vionjo vya Riwaya Mpya Ya Kiswahili*,University of Bayreuth,

Germany (Makala katika mtandao).

Mbiti, S.(1969). *Africans and Philosophy*. London. Heinman.

Miruka, O.(2001). *Oral Literature of the Luo*. Kenya. East African Educational Publishers Ltd

Mlacha S.A.K na Madumulla, J.S (1991). *Riwaya ya Kiswahili*, DUP, Dar es Salaam

Mose, N. (2005). *Taashira ya kifo katika tamthilia ya Mukwava wa Uhehe, Kilio cha Haki, Amezidi na Visiki* (Tasnifu ambayo haijachapishwa Chuo Kikuu cha Kenyatta)

Mohamed, S. 2001). *Babu Alipofufuka*. The Jomo Kenyatta Foundation. Nairobi.

Mohamed. S.2006). *Dunia Yao*. Oxford University Press. Nairobi.

Northrop, F.(1947). *Fearful Symmetry. a study of William Blake*.Canada Princeton University press.

Northrop,F. (1957). *Anatomy of Criticism: Four Essays*. United States of America. Princeton University Press, Princeton, New Jersey.

Northrop,F.(2001). *The Archetypes of Literature. The Norton of Anthropology.Theory and Criticism*. New York. Ed.Vincent B.Leitch.

Oestigaard, T. (2004). *Death in the World . H uman Responses To The Inevitable*. Center for Development Studies. Norway. University of Bergen.

Senkoro, F. (2008). *Uhalisia Mazingaombwe Katika Fasihi ya Kiswahili: Istilahi mpya Mtindo Mkongwe,* Idara ya Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam

Shaaban, R. (1992). *Siku ya Watenzi Wote*. Evans Brothers limited

Schroeder, S. (2004). *Rediscovering Magical Realism in the Americas*. Westpot Praeger.

Strecher, M. (1999). "*Magical Realism and the Search for identity in the Fiction of*

*Murakami Haruki", Journal of Japnese Studies*, Juzuu 25/2.

Wafula, R. na Njogu, K (2007). *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi.* The Jomo Kenyatta Foundation, Enterprise Road, Industrial Area, Nairobi, Kenya.

Wamitila, K.(1997). *Contemptus Mundi and Carpe Motif in Kezilahabi's works.* Juzuu 60.

Wamitila, K.(1999). *Nagona and Mzingile Metapysics.* Kiswahili juzuu 60.

Wamitila, K. (2004). *Mayai Waziri wa Mayai na Hadithi Nyingine.* Focus Publishers.

Zamora, P. & Faris, B.(2005). *Magical Realism Theory, History Community.* London. Duke University Press.